Kikao cha Tisa - Tarehe 09 Oktoba, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani Hati ya Hotuba ya ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa mwaka 2016/2017 naomba kuwasilisha Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Mhe. Waziri wa Afya.

Mhe. Waziri wa Afya: Asante Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hati mezani ya Taarifa ya Utekelezaji wa Magizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii wa Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Afya. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Mhe. Naibu Spika, naomba kuweka mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa mwaka 2016/2017 naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: nakushukuru sana Ali Suleiman Ali. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii naomba kuweka hati mezani kuhusu Ripoti ya Wizara ya Afya ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.
Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana kwa niaba ya Mwenyekiti.

MASWALI NA MAJIBU

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nimepata ombi kutoka kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ambaye ana swali la kwanza 79 lakini vile vile swali namba 74 analo swali ambalo

ameuuliza Wazira wa Ardhi na Maji na kutokana na dharura muhimu ambayo aliyonayo ameniomba kwamba swali lake la 74 lije baada ya swali 79. Kwa hiyo, naomba ridhaa yenu nimempe nafasi hiyo, ili aweze kutimiza malengo mengine ambayo alikuwa anayo ili tuweze kuendelea na maswali kama *order paper* inavyotutaka.

Nam. 79

Malipo ya Ada ya Ulinzi katika Mashamba ya Miwa ya Kiwanda cha Sukari Mahonda

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza**:**

Kuna taarifa kuwa Mwekezaji wa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda amekuwa akilipa kiasi cha shilingi za Kitanzania milioni 11.5 kwa Vikosi vya Idara Maalum za SMZ kwa ajili ya ulinzi wa mashamba ya miwa. Hata hivyo, bado hujuma za kuchomwa moto mashamba hayo zimekuwa zikitokea mara kadhaa.

(a) Je, ni vikosi gani ambavyo vinalipwa fedha hizo kwa ajili ya ulinzi wa mashamba hayo.

(b) Je, ni kwa nini hujuma dhidi ya mashamba hayo zinatokea wakati serikali kupitia Vikosi vya Idara Maalum inapokea ada ya malipo ya ulinzi kwa ajili ya mashamba hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 79 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Kikosi cha Valantia Zanzibar, ndicho kinacholipwa fedha hizo kwa ajili ya huduma ya ulinzi wa mashamba ya Kiwanda cha Sukari Mahonda.

(b) Mhe. Naibu Spika, Kikosi cha Valantia Zanzibar kimeanza kulinda Novemba, 2016 ambapo tangu hapo imetokea hujuma ya moto mara moja tu hujuma hiyo ilitokea tarehe 27 Januari 2017. Hata hivyo, hujuma hizo zimepunguwa sana kulinganisha na kabla ya KVZ kuanza ulinzi huo ambapo hujuma hizo zilikuwa zikitokea mara kwa mara.

Pia, Kikosi cha Valantia Zanzibar kimemshauri mwekezaji wa kiwanda hicho kutafuta *Air Drones*, kuongeza minara na kufanya doria ya magari angalau mara mbili kwa siku. Aidha, Kikosi cha Valantia kimemshauri Mwekezaji wa Kiwanda kujenga uhusiano mwema na majirani wanaozunguka maeneo hayo kwa madhumuni ya kuimarisha ulinzi na usalama wa mashamba hayo ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Mhe, Naibu Spika, na hapa ndipo nilipomwambia Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwamba wawekezaji wanapata shida

alipojibu swali namba 82 akasema wawekezaji hawasumbuliwi, lakini sina tatizo na utendaji wa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

a) Kimsingi Mhe. Waziri swalai la msingi lililohusu Kiwanda cha Sukari cha Mahonda mwekezaji amekuwa akilalamika kwa muda mrefu pamoja na maagizo ya Mhe. Rais hivi juzi nimesikia katika vyombo vya habari ni lini muwekezaji huyo atakabidhiwa nyumba zake zile ile apete kuondosha matatizo yake aendelee na shughuli zake.

b) Kwa kuwa kuna wanyama wa ngo'mbe mle ndani hula miwa michanga na vikosi jukumu lao kulinda ni sababu gani za msingi tukiachia moto kutokutokea, lakini vile vile jukumu la wanyama wanaoharibu mule ndani ikiwemo ng'ombe kula miwa michanga wamechukua hatua gani kwa muwekezaji huyo ili kumpa moyo zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mjumbe arejee swali b.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, rudia swali b.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, mle ndani kulikuwa na mifugo ya wanyama, yaani ng'ombe huingia na kula miwa michanga na jukumu la vikosi ni kulinda eneo lote lile pamoja na kuliwa na ile miwa. Hivi wamechukua hatua gani ile miwa hivi sasa isipate kuliwa na wanyama, yaani ng'ombe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika kwa idhini nako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, kama sikosei wiki iliyipita Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alijibu swali kuhusu muwekezaji huyu kukabidhiwa mali ambazo zimo ndani ya mkataba zikiwemo nyumba. Sambamba na hilo kama sikosei juzi Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alisema tayari nyumba 11, amesha ziko tayari na hivi karibuni anatarajiwa kukabidhiwa. Kwa kweli serikali iliunda kamati maalum kwa ajili ya kushughulika na shughuli hizi ikiwemo ardhi, suala la nyumba na mali nyengine.

   Hivi karibuni tuu kamati iliyoundwa itakamilisha kazi yake na itaweza kupeleka taarifa serikalini na hatua mbali mbali zitachukuliwa zikiwemo za kukabidhiwa nyumba ambazo mmiliki anatarajiwa azipate.

b) Kuhusu suala la ufungaji wa ng'ombe ndani ya mashamba ya miwa Kikosi cha valantia Zanzibar kimepewa jukumu la ulinzi, ili hujuma zisifanyike wakiwepo hao wafuga ng'ombe. Kwa hiyo, kinachofanya Kikosi cha Valantia kupitia askari waliopo kuchukua hatua kwa wale ambao walikuwa wanatabia ya kuweza kufanya shughuli zao ndani ya mashamba ya miwa ya Kiwanda cha Sukari Mahando.

   Kwa hivi sasa wimbi hilo la ufungaji wa ng'ombe, wimbi la upitaji katika maeneo ya mashamba ya miwa, limepungua sana baada ya serikali kuchukua hatua ya kuweka ulinzi

madhubuti, ili kumuwezesha muwekeza aweze kufanya shughuli zake vizuri, ili na yeye apate faida na serikali iweze kupata faida. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa kauli yake njema kusema ujirani mwema wawekezaji ni jambo muhimu, ili pawe na maendeleo ya kushiriki pale panapo tokea janga Mwenyezi Mungu atunusuru tupate kusaidiwa.

Je, kwa kuwa taaluma hiyo Mhe. Waziri ilitoa kwa muwekezaji huyu vipi maendeleo yaliopatina kutokana na agizo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu mama, kwamba faida kubwa imepatikana kwa muwekezaji huyu hasa kutokana na ile kadhia ya moto ambayo ilikuwa ikitokea. Lakini faida nyengine ni ile ya kupunguza hasara kwa kiasi kikubwa wakati kila mara miwa ilikuwa ikichomwa moto, sasa miwa hii haichomwi moto, yaani faida iliyopatikana ni kwamba muwekelezaji atakuwa na nafasi nzuri sasa ya uzalishaji badala ya ile nafasi aliyokuwa hapo nyuma.

Nam. 74

Utekelezaji wa Ahadi ya Kupelekea Maji Safi Michamvi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kazi kubwa ya kuimarisha miundombinu ya maji safi na salama kwa wananchi. Hivi karibuni Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ameahidi kupeleka miundombinu ya maji safi Michamvi, ambapo kwa miaka mingi wananchi wake wanahangaika na maji chumvi.

Je, ahadi hiyo na maneno hayo mazuri kwa watu wa Michamvi yatatekelezwa lini kwa vitendo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoun swali lake Nam.74 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira imekuwa jitihada mbali mbali za kuwapatia wananchi wa Michamvi huduma ya maji safi na salama baada ya kisima kilichokuwa kinahudumia hapo awali kupoteza uwezo wake. Miongoni mwa juhudi

hizo ni pamoja na ufungaji wa mitambo ya kuchuja maji ya chumvi na kuwa ya kunywa kwa kushirikiana na Kampuni ya *UST* ya Ujerumani kwa ajili ya wakazi wa vijiji cha Michamvi Pingwe na Michamvi Kae.

Aidha, katika kutafuta njia ya uhakika serikali kuipitia mradi wa *Ras- el–Khaimah* imechimba visima na kujenga tangi katika eneo la Bwejuu, na pia wizara yangu imeandaa makisio ya gharama za kukamilisha kazi zilizobaki ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.8 zinahitajika. Kwa kweli, mara tu fedha hizo zitakapopatikana wizara yangu itakamilisha kazi hiyo katika kipindi kifupi kadiri iwezekanavyo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayuob: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Lakini Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, namuomba sana awaombe radhi wananchi wa Michamvi kwa jibu hili na nitumie Kanuni ya 59 (3). Naomba kunukuu Mhe. Naibu Spika.

> "Mjumbe yoyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kwa sababu za msingi maelezo anayotowa ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au kubahatisha sasa Spika au Mjumbe mwengine yoyote anaweza kumtaka mjumbe huyo aseme na atoe uthibitisho"

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nikilia sana kwa suala hili nilikuomba kabla ya kuuliza swali nyongeza awaombe radhi wananchi wa Michamvi kwa majibu haya ambayo ya kukatisha tamaa na ya kuwavunja moyo, waombe radhi kwanza, ili niulize swali la nyongeza kwanza.

Omba radhi kwanza Mhe. Naibu Spika, hii Mhe. Naibu Waziri. Ah! ananijibu kitu ambacho hakiekei siku zote nilikuwa nikilia humu kupiga kelele kwa swali hili, halafu anakuja nijibu swala hili na kuwaambia kuna maji. Kwa kweli kama huo mradi mimi nimetia pesa si kidogo labda tuwaulize Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) shilingi ngapi nimetumia kule kwenye maradi huu. Kwa hiyo, anapingana na aya ya Mwenyezi Mungu inayosema "*Wajaalna maii kuli shainn hai"* na tumejalia kila kitu kwa maji. Mhe. Naibu Spika, nakosa usingizi na yeye anafanya mas-hara humu ndani.....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, nimekupa nafasi kuuliza swali la nyongeza, na wala sijakupa nafasi useme hayo unayoyazungumza sasa hivi. Mhe. Mjumbe, naomba uulize swali la nyongeza. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayuob: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwa hivi sasa waathirika wakubwa ni watu wa Michamvi na maji, serikali ndio wananchi, wananchi ndio serikali. Hivyo, atapeleka lini huduma ya maji ya magari kwa ajili ya kuwanusuru wananchi wale, ikiwa tumezoea huko mwanzo mwaka hata mwaka msimu wa Ramadhani yanapelekwa magari ya maji wiki mara moja. Kwa hivyo, ni lini hivi sasa watapeleka maji kwa dharura ukizingatia serikali ndiyo wananchi, wananchi ndiyo serikali wakiwemo wananchi na wa Michamvi.

Lakini la pili ni sababu gani za msingi nimetumia nguvu kubwa na Mamlaka ya Maji wanajua kule na hakuna kilichoonekana niliambiwa miezi sita katika huu mradi wa maji yataapatikana maji, ni sababu gani ya msingi, ili maji hayo yatapatikane.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza naomba afahamu kwamba serikali inawajaali wananchi kama au kuliko ambavyo anavyowajali yeye. Hivyo, ndiyo maana imekuwa ikifanya jitihada na yeye ni shahidi na naomba athamini jidihada hizo kwa vile anaziona, ikiwepo kupeleka maji kwa dharura kwa gari kwa kushirikiana na wahisani mbali mbali. *(Makofi)*

Lakini pia tumesema hapa kwamba kuna mradi ule ambao unabadilisha maji ya chumvi kuwa ya kunywa. Vile vile, kuna huu mradi ambao utagharimu bilioni 1.8 kwa ajili ya wananchi wa Michamvi.

Kwa kweli, mara nyingi amekuwa akizungumzia Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mhe. Naibu Spika, naomba nimwambie kwamba utelekezaji wa ahadi ni wa miaka mitano, moja kati ya eneo muhimu sana ambalo serikali inajali ni wananchi wa Michamvi na ndio maana inatafuta bilioni 1.8 kukamilisha ule mradi wananchi wa Michamvi wapate maji. *(Makofi)*

Sasa ni lini serikali itapeleka maji kadri hali itakavyokuwa inaruhusu si leo si jana kadri hali itakavyokuwa inaruhsu tunakuwa tunapeleka na yeye Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimeshaahidi, lakini pia na yeye naomba tukamatane mkono kwa sababu na yeye anajukumu hilo hilo pia la kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ahsante sana. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayuob: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu swali la pili hakunijibu hakusikia nafikiri swali la pili nilitaka kujua ni lini atapeleka maji kwa dharura kwa wananchi wa Michamvi muda huu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, jibu swali hilo ni lini utapeleka maji ya dharura.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Naibu Spika, maji ya dharura tunakuwa tunapeleka na tutaendelea kupeleka. Kwa hivyo, naomba nimwambie kwamba tukitoka hapa ili aone, kwa sababu tunaweza tukapeleka akaja akasema hajapelekwa, tutawasiliana naye kusudi ahakikishe kwamba tumepeleka ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 39

Utekelezaji wa Sheria za Dini na Ndoa kwa Wanafunzi wa Umri Mdogo

Mhe. Shaib Said Ali (Kny. Mhe. Suleiman Sarhan Said) - Aliuliza:

Baadhi ya wananchi wanaonekana kutokujua baadhi ya sheria za ndoa hasa kuhusiana na umri wa wanafunzi kustahili kuolewa kwa sheria za dini na zile za serikali.

(a) Je, mwanafunzi akifikia umri wa miaka mingapi kidini ni halali kuolewa na miaka mingapi kiserikali anakuwa halali kuolewa.

(b) Je, mwanamke akifikia umri wa miaka mingapi ana uhuru wa kuolewa bila idhini ya baba yake au walii wake kama hawataki kumuunga mkono kwa mume amtakaye.

(c) Je, kama mzazi baba au walii wapo lakini hawataki kumuoza mwanamke kwa sababu yoyote ile. Je, serikali inaweza kumuozesha mume mwanamke bila idhini ya wazazi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 39 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa miongozo ya Dini ya Kiislamu, mwanafunzi akifikia umri wa kubaleghe (miaka tisa hadi kumi na mbili) anaweza kuolewa lakini dini haimzuii baba kumsubiria mtoto wake kama anayo masomo ya lazima hadi kufikia miaka 16-18 kulingana na hali ya mwanafunzi na hali ya maumbile na wala Uislamu haukuweka kikomo cha umri wa kuolewa.

Mhe. Naibu Spika, ama kwa upande wa serikali Sheria Nam.6 ya mwaka 1982 ya Elimu, kifungu cha 20(3) kinaeleza kwamba mwanafunzi hastahiki kuolewa mpaka amalize elimu yake ya msingi na kati.

(b) Mhe. Naibu Spika, hakuna umri unaomruhusu mwanamke/mtoto wa kike kuolewa bila ya idhini ya walii wake.

(c) Mhe. Naibu Spika, mamlaka inayohusika na mambo ya ndoa kama Afisi ya Kadhi ya Wilaya au Afisi ya Kadhi Mkuu, zina mamlaka ya kumuozesha binti ambaye baba au walii hawataki kumuoza mwanamke bila ya kuwa na sababu zinazokubalika kidini. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali fupi la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri umekiri kuwa Afisi ya Kadhi ya Wilaya na Afisi ya Kadhi Mkuu ina uwezo wa kumuozesha binti huyo mume bila ya wazee wake au walii wake kukubali.

a) Je, ni wanawake wangapi waliolewa kati ya mwaka 2016/2017 hadi sasa.

b) Je, wizara yako ina mpango gani wa kufanya utafiti na kuwajua wazee hawa waliokuwa hawataki kuwaozesha watoto wao waume na kuwafanyia suluhu, ili ndo zao ziwe za kuridhiana kati ya mwana na baba au walii wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi swali lake la awali linahitaji takwimu, kwa hivyo nimwambie kwamba swali hilo tutalijibu kwa njia ya maandishi kwa sababu linataka kufanya utafiti wa kutosha.

b) Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kusema kwamba walii wanapokuwa hawataki kuwaozesha watoto wao kama nilivyosema nilivyojibu kwamba Afisi ya Kadhi ya Wilaya au Afisi ya Kadhi Mkuu wana mamlaka ya kumuozesha. Ni kweli wana mamlaka na mzee anaweza akafika kwenye hizi mamlaka kama mzee atakuwa na sababu ya msingi kwamba mtoto wangu sitaki aolewe kwa sababu mume anayetaka kumuoa ni mlevi. Hapo Kadhi anaweza akakubaliana na mzee wa mtoto kwamba kweli mzee ana sababu ya msingi.

   Lakini walii aende moja kwa moja kusema kwamba mimi mtoto wangu huyu sitaki aolewe na mtu fulani kwa sababu pengine sababu za kisiasa, hivyo dini haitambuwi hilo kwa hivyo Sheikh anaweza akaenda kinyume na *interest* za huyu mzee au yale matakwa ya huyu mzee kwamba mtoto wake hataki kumuozesha eti kwa sababu ya kisiasa, dini haitambui hiyo. Kama sababu ni ya msingi pengine mwanamke anataka kuolewa na mwanamme mgonjwa hapa sababu ipo kwa maana Sheikh au Kadhi moja moja anaweza kusema asiweze kukubali kuolewa. Nashukuru sana ahsante. *(Makofi)*

Nam. 24

Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar

Mhe. Shaib Said Ali (Kny. Suleiman Sarahan Said) – Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuiletea Zanzibar na wananchi wake maendeleo imeanza maandalizi katika uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

(a) Je, serikali imejipanga vipi kwa mikataba madhubuti ukizingatia ni suala jipya kwa Zanzibar.

(b) Serikali imetafuta wataalamu wa nchi gani wa kutusaidia kufunga mikataba madhubuti.

(c) Je, serikali imejipangaje katika suala la wataalamu wetu wa ndani. Katika maeneo tofauti tofauti ya mafuta na gesi asilia kama vile wahandisi wa mafuta na gesi na wanasheria wa sekta hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia ya Zanzibar imetoa muongozo wa kuandaa Mikataba ya Mafuta na Gesi Asilia (*PSA*) itakayotumika katika kuendesha

shughuli za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta ama Gesi Asilia Nchini. Hivi sasa Rasimu ya Mkataba (*MPSA*) tayati imeshaandaliwa na iko tayari kutumika kwa majadiliano na Makampuni yatakayoendesha shughuli za Mafuta na Gesi Asilia.

(b) Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatumia wataalamu wake wa ndani katika mijadala ya Mikataba ya Mafuta na Gesi Asilia. Wataalamu hao wamepata mafunzo na mbinu za kufanya mijadala kwa kupitia mafunzo mbali mbali ya ndani na nje ya nchi.

(c) Mhe. Naibu Spika, wizara tayari imechukua jitihada za ziada katika kuwaorodhesha wanafunzi wanaosoma masomo ya Mafuta na Gesi Asilia katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Aidha, wizara tayari inaendelea na taratibu za uajiri wa vijana waliomaliza masomo yao katika fani za Mafuta na Gesi Asilia wakiwemo Wahandisi na Wanajiolojia. Aidha, jitihada za kuwahamasisha vijana wanaojiunga vyuoni kuchukua fani mbali mbali zinazohusiana na Mafuta na Gesi Asilia kama vile "*Petroleum Law, Petroleum Economics na Health and Safety*" zinaendelea ili taifa liweze kujipatia wataalamu wa kutosha. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 38

Uwiano wa Mgao wa Fedha katika Skuli za Msingi

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa utaratibu uliojiwekea wa kutoa shilingi 500,000/= kwa skuli za msingi, Unguja na Pemba, kwa ajili ya kutanzua mambo yao mbali mbali.

Je, wizara katika mgao wa fedha hizo, imezingatia uwiano wa skuli hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 kama hivi ifuatavyo: -

Mhe. Naibu Spika, wizara ilianza kutoa fedha za ruzuku kwa skuli za serikali kuanzia mwaka 2015-2016 bila kuzingatia uwiano katika skuli. Hata hivyo, wizara imebaini kwamba ugawaji huo unahitaji kuzingatia uwiano katika skuli zetu. Kwa hivyo, kwa mwaka 2017-2018, wizara itagawa fedha hizo kwa kuzingatia vigezo vikuu vitatu vikiwemo idadi ya wanafunzi katika skuli, idadi ya madarasa na idadi ya mikondo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, bado naipongeza serikali kwa nia njema ya kuhakikisha kwamba wanagawa mgao huu ili kuondoa matatizo ya hapa na pale. Lakini Mhe. Naibu Spika, swali langu kwa kuwa mpango huu umeelekea katika skuli zetu za msingi tu. Je, Mhe. Naibu Waziri atatueleza nini juu ya skuli za sekondari ambazo kwa mfano wenzetu hawa wanalazimika kulipa umeme na mambo mengineo kila mwezi. Kwa mfano, skuli

yangu ya Kwarara ambayo ina mahitaji makubwa ya matumizi ya umeme na fedha nyingi zinatumika kulipa umeme huo, wizara ina mpango gani kwa sekondari kama hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Kwa kweli, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia msaada wa *World Bank* imekubali kugharamia matumizi ya namna hii katika skuli za sekondari na kila mwanafunzi atapata dola 15, na mradi huo tunakusudia kuanza Machi, 2018. Na kwa maana hiyo zaidi ya milioni tatu na kadhalika zimeshawekwa kwa ajili ya mpango huu na zipo na wizara sasa hivi inaandaa utaratibu wa kutayarisha *manual* namna ya kuzitumia fedha hizo na baadaye tutatoa mafunzo kwa Walimu Wakuu na baadaye tutaaza kutumia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako umesema kwamba mmeanza kutoa ruzuku katika maskuli, ni skuli ngapi zimepata ruzuku hizo na ni aina gani ya ruzuku ambazo skuli hizo zimepata.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Ni kwamba ruzuku hii imetolewa kwa skuli zote za msingi za Unguja na Pemba, kama skuli 277 hivi na hii ni ruzuku kwa ajili ya matumizi ya skuli ya mambo madogo madogo kama ukarabati wa mdogo mdogo, umeme, maji na kadhalika.

Nam. 88

Kesi za Udhalilishaji Mkoa wa Kaskazini Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Taarifa za hivi karibuni kupitia vyombo mbali mbali vya habari ikiwemo Gazeti la Zanzibar Leo la tarehe 22/07/2017, zimeonesha ongezeko kubwa la vitendo vya udhalilishaji kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambapo katika kipindi cha mwezi Januari hadi Juni mwaka 2017 matukio yapatayo 36 yameripotiwa Polisi.

Je, kwa nini matukio hayo yameongezeka pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na serikali kukabiliana na vitendo hivyo, hasa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhana Wataala*, ambaye ni yeye anaendelea kutupa pumzi zake na tukaweza kukutana asubuhi hii katika Baraza lako tukufu tukiwa na afya njema.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Naibu Spika, sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu tulizozipokea kutoka Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba kuanzia mwezi Julai hadi Disemba, 2016 jumla ya matukio 98 ya udhalilishaji yalipokelewa na kuanzia Januari hadi Juni 2017 jumla ya matokeo 198 yamepokelewa. Kuongezeka kwa matukio haya pia kunaashiria kuongezeka kwa mwamko wa wananchi kuripoti matukio ya udhalilishaji. Pia, masuala ya kuporomoka kwa maadili yamekithiri na hasa talaka za kiholela zinazopelekea watoto kukosa haki zao za msingi na hatimaye kujiingiza katika matendo yanayohatarisha maisha yao na kudhalilishwa. Matumizi mabaya ya teknolojia ya habari na mawasiliano pia yanachangia katika kuongezeka kwa matukio hayo.

Mhe. Naibu Spika, kazi ya kupunguza matukio haya si ya wizara yangu peke yake bali ni ya kila mmoja wetu hasa sisi Waheshimiwa Wawakilishi ambao moja kwa moja tunaishi na jamii. Ni wajibu kukaa na wazazi na familia kusaidiana katika malezi bora ya watoto wetu. Wizara itaendelea na jukumu lake la kuratibu na kuelimisha jamii kwa njia mbali mbali pamoja na kusimamia utekelezaji wa mpango kazi wa miaka mitano. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwanza naomba ku-*declare interest* mimi ni Mjumbe halali wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii.

a) Pamoja na jitihada zinazochukuliwa na viongozi wetu wakuu wakiwemo Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein ni lini wizara itakaa kidhati kabisa kwa ajili ya kutathmini Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu tumechoka na matatizo haya, lakini inaonekana miongoni mwenu wizara mnashindwa kusimamia majukumu yetu. Ni lini mtakaa kujitathmini hiki ndicho na hiki sicho, lakini inaonekana bado jitihada za viongozi wetu wizara mnashindwa kuzisimamia. Lini mtakaa kutathmini wenyewe ndani kwa ndani kabla ya kuchukua hatua nyengine.

b) Ulipokuwa unajibu maswali ya kuporomoka kwa maadili mmechukua hatua gani kuelimisha jamii kuhusu kuporomoka kwa maadili hayo. Maadili yanazidi kuporomoka lakini inaonekana mnashindwa kusimamia dhamana zenu kutoka Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, mimi ni mjumbe halali wa kamati hii chini ya Mwenyekiti wangu makini Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, naomba kumuhakikishia Mhe. Mwakiilshi kwamba wizarani tukaa vikao mbali mbali baina ya mimi Naibu Waziri, Katibu Mkuu na hata watendaji wote pamoja na wizara nyengine ambazo zinahusika kwa njia moja au nyengine ili kuona kwamba tatizo hili la udhalilishaji watoto linaondoka na kumalizika kabisa. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tunakaa na tutaendelea kukaa kujadili kwamba suala hili linaondoka na kadhia hii inaisha katika nchi yetu. Lakini kama nilivyojibu

katika swali langu mama kwamba kazi hii sio ya wizara peke yake, bali inahitaji nguvu zetu sote wananchi hasa sisi wawakilishi ambao tuko katika majimbo na tunaishi na jamii ni vizuri kuwaelimisha watu wetu kuhusiana na suala hili. Ahsante mheshimiwa.

b) Kuhusu wizara inachukua juhudi gani kuona kwamba maadili yanavurugika. Naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, kwamba tunachukua juhudi mbali mbali za kuelimisha jamii kupitia redio, matangazo mbali mbali na hata tukishirikiana na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ambao wao ndio wadau wakubwa wa vyombo vya habari katika kushirikiana kulitokomeza suala hili. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi ya leo kuamka salama. Lakini la pili nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake sahihi aliyojibu yanayotokana na swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi. Mhe. Mwakilishi nataka nimuhakikishie kwamba serikali hii iko makini sana kwa sababu imeunda Kamati Maalum ya Mawaziri akiwemo Waziri wa Katiba na Sheria, Waziri wa Afya, Waziri wa Kazi na Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na wengineo pamoja na Waziri wa Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali, lakini pia kuna maeneo mbali mbali Mahakama, *DPP* na Mwanasheria Mkuu pamoja na maeneo mengine yote yanayohusika na masuala haya hii nikuonesha kwamba kwa kiasi gani serikali hii inajali na inatambua ukubwa wa tatizo hili. Kwa hivyo, napenda nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba serikali hii inafanya kazi vizuri na tunashirikiana vizuri hakuna matatizo. *(Makofi)*

Nam. 118

Baraza la Vijana

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma - Aliuliza:

Katika bajeti iliyopita 2017/2018 Baraza la Wawakilishi Zanzibar limepitisha jumla ya shilingi milioni mia moja kwa ajili ya Baraza la Vijana Taifa pekee, na kusahau kuwa kuna Mabaraza mengine takriban 384 ya shehia na Mabaraza 11 ya Wilaya zetu ambayo hajayapangiwa hata robo ya bajeti.

Je, wizara inawaambia nini vijana wale waliojikusanya kwa hiari yao na kuonesha jitihada zao kwenye Shehia na Wilaya zetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 118 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Baraza la Vijana Zanzibar limeundwa kwa mujibu wa Sheria Namba 16 ya mwaka 2013, ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2005. Pia ni utekelezaji wa Ibara 131(b) ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015 – 2020, ambayo Mhe. Rais

Wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein aliinadi wakati wa Kampeni zake za kugombea Urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, nakubaliana na hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba kikao cha Bajeti ya 2017/2018 Baraza la Wawakilishi lilipitisha jumla ya shilingi milioni mia moja (100,000,000/=).

Hakuna mgao wa fedha hizo kwa Mabaraza ya Wilaya na Shehia, fedha hizo zitatumika kwa mujibu wa Mpango Kazi wa Baraza la Vijana uliopangwa kuanzia ngazi ya Taifa hadi Shehia. Mpango Kazi huo, unakusudia kuwaunganisha vijana na fursa mbali mbali pamoja na kuwapatia mafunzo ya uongozi, ujasiriamali na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, wizara inawataka vijana kuibua miradi mbali mbali na kufuatilia fursa serikalini na sekta binafsi ili kupata kipato na kwa wale waliojikusanya. Kwa wale waliojikusanya wizara itawaunga mkono kwa kuwaunganisha na fursa mbali mbali. Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuwasaidia vijana hao katika maeneo yao na natoa wito na kuwaomba kuendelea kuwasaidia pale hali inaporuhusu ili kujenga mustkabali mwema kwa vijana wetu hawa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Salma Mohammed Mwinjuma: Mhe. Nabu Spika, kutokana na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ametwambia kwamba, hakuna mgao wa fedha yoyote katika Mabaraza ya Shehia wala Wilaya na badala yake watazingatia mpango kazi ambao tayari wameshauona wao unafaa kwa vijana wetu.

(a) Je, Mhe. Waziri katika huo mpango kazi ana vigezo gani vya kuzingatia ili kuona vijana wetu tunawasaidia.

(b) Anawaambia nini wale ambao tayari walikuwa na mpango wao kazi katika shehia zao, wilaya na hata taifa tukiona kwamba mpaka sasa bado hawajasaidiwa. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, naomba arudie tena lile swal la mwanzo kwanza.

Mhe. Salma Mohammed Mwinjuma: Mhe. Nabu Spika, Nimemuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba, katika jibu lake mama amesema kwamba hakuna fedha yoyote itakayogaiwa kupitia Mabaraza ya Shehia na Wilaya zake, badala yake wataangalia mpango kazi.

(a) Je, katika huo mpango kazi kuna vigezo gani ambavyo wamevizingatia.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika ahsante sana, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Vigezo ambavyo tumezingatia kwa vijana hao na tukaweza kuwapatia mkopo ni kutokana na msururu mzima wa maendeleo kutokana na vile vikundi vyao ambavyo wamejikusanya na kuona zile juhudi zao ambazo wanazifanya. Kwa maana hiyo, vikundi hivi tunavipa kipaumbele na wizara tukaweza kusaidia kuweza kupata mgao ule.

Swali la (b) kidogo naomba alirudia tena Mhe. Salha Mohammed samahani.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Mhe. Naibu Spika, narejea kwa mara nyengine tena kwa umakini zaidi. Mhe. Naibu Waziri nimemuuliza ya kwamba hawa ambao tayari ameshajikusanya wana mipango yao kazi wamejiwekea wanahisi itakuwa ina tija kwao. Watawasaidia nini kama wao wizara.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salha Mohammed swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa hawa vijana ambao tayari wamejikusanya kama mwanzo wizara ilivyoweza kuwasaidia na wakaweza kujikusanya na mpaka hapo walipofikia niwaombe kwamba, wizara itaendelea kuwasaidia na kuhakikisha kwamba yale malengo yao waliyojipangia yanafanikiwa. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuniona kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini napenda nimuulize swali lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Naibu Spika, tangu kupitisha bajeti ya Baraza la Vijana sasa hivi ni mwezi wa tatu, ni miezi mitatu tayari. Je, katika hii miezi mitatu ambayo tayari tumeshaitumia au imeshapita ni mara ngapi au ni miezi mingapi ambayo tayari wameshapatiwa hiyo bajeti yao vijana ili kuendelea na kazi zao ndani ya mawilaya lakni pia kusaidia huko kwenye shehia. *(Makofi)*

(b) Mhe. Naibu Spika, hii bajeti haitoingizwa kwenye shehia wala wilaya. Je, anahisi hii miradi ambayo wanawaambia hawa vijana waibue au wainue, anahisi watajisaidia vipi vijana hawa wakiwa hawana nyezo yoyote, hawana usaidizi wowote wala elimu yoyote kuhusu hii miradi ambayo wanatakiwa wafanye. Kama wizara kuna hatua gani ambazo watazichukua kwanza kuwafahamisha hawa vijana, kuwaelimisha ili wajue wapate hizo mbinu baadae ndio wawape na hiyo mikakati mingine mipango kazi waliyoiandaa sijui ni ipi wameandaa hiyo mipango kazi yenyewe. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Kama alivyouliza kuhusu bajeti katika hii miezi mitatu ambayo tumeipitisha ni kwamba wameweza kusaidiwa vipi katika miezi mitatu hii. Nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba swali lake hili linahitaji takwimu kwa hivyo swali hili nitamjibu kwa maandishi.

Swali la (b) lilikuwa refu mno naomba alirudie tena.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hidaya Ali Makame, naomba urudie swali lako la (b).

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize kwamba wametwambia kuwa hizi fedha hazitoingizwa kwenye wilaya wala shehia fedha hizi moja kwa moja zitakwenda taifa, lakini huko taifani pia hazijafika. Ndio swali langu nililouliza la (a) kwamba Je, wamepewa miezi mingapi sio takwimu ya kwamba shilingi ngapi aa.

Hili la (b) nimeuliza kwamba, humo ndani ya shehia ambamo wanatakiwa wafanye kazi ili waende huko kwenye wilaya na taifa, huko kwenye taifa hakuna elimu yoyote ambayo wizara wanaitoa. Je, ni hatua gani ambazo watazichukua ili kuanza kuwapatia elimu hawa vijana ili waweze kuibua hiyo miradi yao. Na hiyo mipango kazi iliyoandaliwa na wizara ni ipi na ipi ili waweze kupambana nayo wafikie hivyo vigezo vya kuweza kupewa hizo fedha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame kama ifuatavyo.

(a) Kuhusu fedha ambayo amesema imetiliwa taifa na mabaraza ya wilaya au shehia hayafaidiki na fedha hiyo wakati na wao wanahusika na kwamba ni mipango gani inayofanywa na Baraza la Taifa. Nimhakikishie kwamba kuna shehia ambazo tayari Baraza la Taifa linashuka kule ili kuwashajihisha vijana wale na miradi yao wanayoendeleza. Ikiwa kwa upande wa kwake Mhe. Mjumbe anahisi kwamba jambo hili halijafika, basi naomba Mheshimiwa tuonane ili tumpe waratibu wetu waendelee kufuatilia suala hili.

(b) Kuhusu mipango gani ambayo Baraza la Taifa linaichukua ili kushajihisha wale vijana walioko katika shehia. Kwanza nataka nimwambie Baraza la Vijana la Taifa linaratibu kuwajengea uwezo viongozi wa Mabaraza ya Vijana Wilaya ambao wanapatiwa mafunzo ya aina mbali mbali. Vile vile viongozi wa Mabaraza ya Vijana wanapata fursa ya kushiriki katika mikutano, makongamano mbali mbali ya kitaifa na hatimaye Baraza la Vijana wa Wilaya yanapatiwa fursa ya kuunganishwa kimasoko na utaalamu wa bidhaa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 101

Kushuka bei kwa Zao la Mwani

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Wananchi wengi wa Zanzibar wanaoishi ukanda wa bahari wanategemea kilimo cha mwani hasa akinamama, lakini kwa bahati mbaya zao hilo limeshuka bei, kiasi cha Wakulima hao kukata tamaa.

Je, wizara ina mpango gani wa kutafuta masoko ya zao hilo la mwani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu:

Mhe. Naibu Spika ahsante sana, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 101 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, wananchi wengi wa Zanzibar wanaoishi ukanda wa bahari wanategemea kilimo cha mwani hasa akinamama.

Mhe. Naibu Spika, wizara inawasiliana na watu na taasisi mbali mbali ili kuangalia uwezekano wa kununuliwa kwa mwani wa Zanzibar kwa bei ambayo itakuwa na maslahi na tija kwa wakulima.

Mhe. Naibu Spika, wizara inatafuta wawekezaji ambao watawekeza katika usarifu wa zao la mwani ili kupata bidhaa ambazo zinaweza kutumika katika soko la ndani na nje ya Zanzibar. Aidha, wizara inahamasisha jamii kutumia mwani kwa matumizi ya chakula na matumizi mengineyo ili kupata soko la ndani kwa mwani wetu ambao kwa kiasi kikubwa unasafirishwa nchi za nje.

Mwani wa Zanzibar unasafirishwa kupelekwa katika nchi za Marekani, Denmark, China, Vietnam, Philippines, Chile, Ufaransa, Korea na Malaysia. Pia wizara yangu itaendeleza mashirikiano na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na taasisi nyengine katika kutafuta masoko ya zao la mwani. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanakidhi haja kutokana na hali ikifuatwa. Lakini pamoja na kutueleza kwamba, kuna mpango mzuri wa matumizi ya chakula kwa mwani, ambapo kapendekeza hapa kwetu Zanzibar utumiwe kwa wingi ili wananchi wapate faida ya kujua mboga mboga zinazotokana na mwani.

Je, wizara ina mpango gani wa makusudi kuanzisha eneo maalum la kuuza huu mwani wa chakula ambao wananchi watakwenda kupata mahitaji yao na kujaribu na kuona ladha yake, ili wajitokeze kwa wingi kwenda kununua.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyogeza.

Mhe. Naibu Spika, suala la mauzo ya mwani kila yanapofanyika maonesho basi wauzaji hao wanakuwepo. Vile vile nipende sana kuwakaribisha wananchi kesho katika Maonesho ya Chakula watakuwepo wauzaji hawa wa mwani karibuni sana. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona tena kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye kutia moyo, lakini napenda nimuuliza swali dogo la nyongeza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika mkoa ambao wakulima hawa wanapatika ukiwemo ni Mkoa wa Kaskazini Unguja. Lakini katika vijiji ambavyo vilikuwa vinalimwa mwani mwingi pia ikiwemo ni jimbo la Nungwi na wakiwemo na wazaliwa wa Nungwi. Lakini kinamama hawa sasa hivi

hawaoneshi moyo wa kuulima huu mwani kutokana na changamoto mbali mbali ambazo zinajitokeza.

Je, kama wizara inachukua hatua gani kuweza kuwarudishia nyoyo zile za kuulima huu mwani wakauthamini na kuona kama ni kilimo chengine ambacho kitawaletea mahitaji na baadaye soko lake litakua, ili kuweza kuendeleza na mahitaji yao na maisha yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Hidara Ali Makame swali lake la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, mwani ni chakula, mwani ni *salad*, mwani ni kila kitu. Tumeshauri na pia tunapendekeza wakulima walime mwani mnene ambapo mwani huo una bei kuanzia shilingi 800 mpaka shilingi 1,000 kwa kilo na ule mwani mwembamba ndio hauna soko ambao bei yake mara kwa mara inashuka kutokana na uzalishaji mwingi wa ule mwani duniani.

Vile vile, tunashauri wakulima hawa walime mwani kwa *plot* pengine kama mkulima mmoja ana *plot* sita, alime *plot* mbili halafu zile nyengine nne aachane nazo alime mbili tu, kila unapokuwa kidogo ndivyo bei inapokuja juu. Kwa hivyo, labda tusaidiane Mhe. Mwakilishi katika kutoa taaluma hii, mwani mnene ni mwani ambao ni mzuri zaidi na una soko zaidi kuliko mwani mwembamba.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba mwani mnene ndio wenye bei zaidi yaani wenye tija na kuacha ule mwani mwembamba kwamba hauna bei. Lakini sasa wakulima wengi kwamba mwani huu mnene ndio wenye bei lakini kuna baadhi ya maeneo haukubali kabisa. Je, wizara yake ina mpango gani wa kufanya utafiti, ili kuhakikisha wale wakulima waondokane na yale maeneo yaliyokuwa hayakubali ule mwani ili kufika kule kwenye maeneo ya bahari kupanda mwani mnene unaokubali katika maeneo yale.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, utafiti tunaweza kuufanya lakini pale fedha itakapoturuhusu. Kwa kweli, utafiti una gharama zaidi na hautakuwa utafiti wa siku moja au mbili ni utafiti ambao utakuwa wa muda mrefu. Kwa hivyo, namuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba, tutakaa kitako tuzungumze na wataalamu wafanye utafiti huo, ili tujue vipi tutawasaidia wakulima hao wa mwani. Ahsante.

Nam. 109

Marufuku ya Matumizi ya Msumeno wa Moto kwa Watu Binafsi

Mhe. Suleiman Makame Ali (Kny. Mhe. Omar Seif Abeid) - Aliuliza:-

Kwa kuwa serikali imepiga marufuku matumizi ya msumeno wa moto kutumika kwa watu binafsi kwa ajili ya kukata miti ili kunusuru nchi yetu kuwa jangwa. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa msako wa kuikamata misumemo hiyo, bado shughuli za kukata miti kwa "*chainsaw*" zinaendelea pamoja na ukweli kwamba misumemo hiyo imepungua sana.

(a) Je, ni misumemo mingapi ya moto iliyokamatwa kwa upande wa Unguja na Pemba, na misumemo mingapi imechomwa moto kwa Unguja na Pemba.

(b) Je, ni misumemo ya moto mingapi iliyokamatwa ambayo haijachomwa moto na wapi ilipo kwa upande wa Unguja na Pemba.

(c) Askari ambao hufanya doria kusaka misumeno hiyo baada ya kuikamata huipeleka wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 109 kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, tangu kuanza kwa operesheni ya kukamata misumeno ya moto, jumla ya misumeno 279 imekamatwa Unguja na Pemba. Misumeno 169 imekamatwa Unguja na 110 imekamatwa Pemba. Kati ya misumeno 279 iliyokamatwa, misumeno 154 imeharibiwa kwa kuchomwa moto. Misumeno 85 imechomwa moto Unguja na misumeno 69 imechomwa moto Pemba.

(b) Mhe. Naibu Spika, kati ya misumeno 279 iliyokamatwa, misumeno 125 haijachomwa moto. Misumeno 84 imehifadhiwa katika maghala ya serikali kwa Unguja na Pemba ambapo Unguja ipo misumeno 60 na Pemba ipo misumeno 24. Misumeno 27 kati ya 60 iliyopo Unguja imehifadhiwa katika ghala la Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ambapo misumeno 33 imehifadhiwa katika ghala ya Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka. Misumeno yote 24 iliyopo Pemba imehifadhiwa katika ghala la Wiraza ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka. Aidha, misumeno mengine 41 imegawanywa katika vikosi mbali mbali vya Ulinzi na Usalama kwa matumizi ya dharura inapojitokeza.

(c) Mhe. Naibu Spika, misumeno yote ya moto inayokamatwa na askari wetu wa doria huwasilishwa Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka na baadaye huhifadhiwa ghalani baada ya kuwekwa kumbukumbu katika vitabu maalumu ikisubiri maamuzi mengine ya serikali.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kuna misumeno imekamatwa Unguja na Pemba mingne imechomwa moto na mengine bado. Je, badala ya hii hukumu ya kuchoma moto na tunaona kwamba mazingira kila siku yanapotea kwa kukatwa miti ovyo, kuna hukumu gani nyengine badala ya kukamatwa misumeno yao ya moto wale wanaofanya uharibifu wa mazingira wale wanaokata

miti ile badala ya kuzuiliwa misumeno yao wana hukumu gani nyengine wanayopewa kupitia wizara hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi : (anaendelea) kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi napenda kumjibu Mhe. Suleiman Makame suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kama nimemsikia vizuri naomba nimjibu na kama itakuwa vibaya basi atanambia.

Mhe. Naibu Spika, hawa wanaokamatwa na misumeno ya moto mara nyingi huwa hatuwapati tunapata ile misumeno tu wao wenyewe wanawahi kupigia na kuitupa chini ile misumeno ya moto. Lakini zaidi kama tutabahatika tutawakamata basi tutawapeleka Mahakamani kwa kuwashitaki na mahakama itaamua yale maamuzi yake. Ahsante.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha sana. Mimi nina suala dogo nataka nimuulize suala dogo sana.

Mhe. Waziri unapohifadhi kosa huzaa janga na hatimaye huzaa maafa. Je, kuna sababu gani za msingi zinazopelekea misumeno hiyo ikahifadhiwa baada ya kuchomwa moto yote kuondoa majanga haya yaliyotukabili. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi : Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi napenda kumjibu Mhe. Shaib Said Juma swala lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Maneno yako unayoyasema nayazingatia lakini vile vile ukumbuke kwamba misumeno hii hii naisaidia serikali kwa asilimia kubwa sana kwani pale miti inapofikia kuwa imezeeka na inataka kukatwa au kupunguzwa matawi ndio misumeno hii hii ambayo tunaitumia. Ahsante sana.

Nam. 68

Kero ya Moshi wa Taka za Hospitali ya Mwembeladu

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Kny. Mhe. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza**:**

Hospitali ya Wazazi ya Mwembeladu ipo katika eneo ambalo ni karibu na makaazi ya watu ambapo kumekuwa na kero kubwa wanayopata wakaazi wa jirani na Hospitali hiyo kwa moshi unaotokana na kuchomwa takataka zinazozalishwa katika Hospitali hiyo.

(a) Uongozi wa Hospitali unajua kuhusu tatizo hilo na kero wanayoipata wananchi.

(b) Je, Wizara itachukuwa hatua gani ya kuhakikisha uchomwaji wa taka hizo hauleti athari kwa wananchi wa eneo la Mwembeladu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyo jirani na Hospitali ya Mwembeladu wanakabiliana na changamoto ya moshi unaotokana na kuchomwa kwa taka katika hospitali hiyo.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, napenda kuchukua nafasi hii kulieleza Baraza lako tukufu, pamoja na wananchi wanaoishi jirani na Hospitali ya Mwembeladu, kuwa taka zinazochomwa katika hospitali hiyo ni taka za kawaida sio taka hatarishi, hivyo nawaomba wananchi wasiwe na khofu na moshi huo.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile pahala wanapokaa binadamu japo kwa muda mfupi kwa mazingira yetu hapaachi kutengeneza taka, Hospitali ya Mwembeladu huwa inatengeneza taka zinazotokana na mazingira ya kawaida, yaani taka nyepesi na taka zinazotokana na mazingira ya huduma ikiwemo huduma ya uzazi hasa kwa vile hospitali hii inashughulikia wazazi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, taka hizi zinazochomwa katika hospitali ya Mwembeladu ni zile taka zote ambazo ni nyepesi na hazitokani na huduma zinazohusiana na uzazi. Taka nzito zinazohusika na uzazi, pamoja na mambo mengine pamoja na baadhi ya vitendea kazi, hospitali ina utaratibu maalum wakuzipeleka katika Hospitali ya Mnazimmoja kuziteketeza kupitia, mashine ya *Ocodas* zilizofungwa katika mradi wa *ORIO*.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa nafasi katika Hospitali ya Mwembeladu, pia mazingira ya hospitali hiyo kubanana sana na makaazi ya wananchi, wizara yangu imeona haja ya kuondoshea ghofu wananchi wa Muembelandu kwa kuanza na hatua ya kujenga tanuri kubwa katika Hospitali ya Mmazimmoja upande wa Kizingo, ili taka zote zinazotokana na kutoka katika Hospitali ya Muembeladu zipelekwe huko na kuchomwa kwa utaratibu maalum. Muembeladu hapatachomwa tena taka kwa wakati huu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuniona pamoja na jibu la serikali lenye ukakasi naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa majengo yote ya Wizara ya Afya na kwa kutambua moshi una athari kubwa imepiga marufuku wananchi wote kuvuta sigara katika majengo yale. Je, ni taratibu gani zitachukuliwa sasa kuondosha kabisa taka ambazo zinachomwa ndogo ndogo katika Hospitali ya Muembeladu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed swali la nyongeza kwa niaba ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, naomba asifananishe moshi ya sigara uliopigwa marufuku na moshi wa takataka za kawaida kama nilizoziainisha. Kwa kweli, moshi huu ni sawa na moshi ambao hatuwezi kuuepuka wa majumbani kwetu na katika mazingira yote hayo. Kwa hiyo, kwa njia yoyote vile hatuwezi kuepuka kuwa na moshi katika mazingira yetu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nimesema katika jibu langu la msingi kwamba Hospitali ya Mmazimmoja Wizara ya Afya tuna utaratibu maalum wa kujenga tanuri kubwa na tumo katika utaratibu huo. Mhe. Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe waniamini kwamba wizara imo katika utaratibu maalum wa kujenga tanuri kubwa katika eneo la upande wa Kizingo, ili kuchoma choma katika taka taka zote kwa wakati huu litakapomalizika tanuri hiyo nawaahidi kwamba Hospitali ya Mwembeladu haitachoma taka hata moja. (*Makofi*)

Nam. 134

Huduma ya Sehemu ya Kujisaidia (Choo) katika Jengo Linalotoa Huduma ya Vipimo ya (MRI) Hospitali ya Mnazimmoja

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma (Kny. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa) - Aliuliza**:**

Tuishukuru serikali yetu na mpendwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutuletea huduma ya MRI katika Hospitali ya Mnazimmoja, na kuondoa adha ya watu kusafiri nje ya nchi kufuata huduma hiyo. Lakini tatizo linalojitokeza kwa wale wanaohudumiwa wakiwekewa dawa na wakihitaji kujisaidia hakuna pahala pa kujistiri mpaka utoke nje ya jengo.

(a) Waliobuni mradi ule na wasimamizi hawakujua kwamba watu wakifanyiwa kipimo hicho watahitaji kujisaidia.

(b) Wizara itachukua hatua gani ya kuhakikisha kwamba katika kitengo hicho kunakuwa na sehemu ya kujisaidia ili kuepusha usumbufu kwa mgonjwa kutoka nje ya jengo kwenda kwenye choo cha jumla nje ya jengo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 134 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, ni kweli chumba cha uchunguzi wa *MRI* hakuna choo karibu yake. Hii imetokana ya kuwa mashine hiyo imejengwa katika sehemu iliyokuwa kiwanda cha dawa na sehemu hiyo hakukuwa na vyoo karibu. Hata hivyo, Uongozi wa Wizara ya Afya umebaini kasoro hiyo na wataalamu wa majenzi wanaangalia njia sahihi ya kujenga choo sehemu hiyo bila ya kuathiri utendaji wa *MRI* ambayo inatumia nguvu za sumaku, yaani *Electromagnetic Reathonex Energy* kutokuathirika kwa mpango huo . Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 37

Utumiaji wa Alama za Barabarani kwa Madereva wa Vyombo vya Usafiri na Askari wa Barabarani

Mhe. Shaib Said Ali (Kny. Mhe. Suleiman Sarhan Said) - Aliuliza**:**

Kumekuwa na tabia ya baadhi ya madereva wanaoendesha vyombo vya usafiri wa barabarani kuendesha vyombo hivyo kwa mazoea badala ya kuongozwa na alama za barabarani ambazo hazipo au hazionekani vizuri na Polisi kwa mazoea nao hukamata madereva na kuwafungulia kesi zinazohusiana na ama mwendo wa kasi au kupitiliza kiasi cha mwendo kilichowekwa au makosa mengine kuhusiana na alama nyengine kutofuatwa kabisa.

(a) Je, serikali wanalijua hilo kuwa barabara zake hazina alama za kutosha za kuongozea madereva na watu wengine watumiao barabara hizo.

(b) Je, polisi anafuata sheria gani na anazijuaje alama ambazo hazipo, na akaweza kumkamata dereva na kumshitaki kwa kutenda kosa.

(c) Je, polisi anapomkamata dereva kwa matatizo kama hayo, kuwa hatuoni kuwa tunamuonea dereva huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 lenye vipengele (a), (b) na (c) lakini kabla naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mambo mengine ujenzi wa barabara huzingatia zaidi usalama wa barabara, usalama huo ni pamoja na uwekaji wa alama mbalimbali zinazompa tahadhari dereva na hata anaeenda kwa miguu. Mhe. Naibu Spika, sambamaba na uwekaji wa alama hizo, wizara kwa kushirikiana na polisi hutoa elimu kuhusiana na alama hizo, lakini baadhi ya watu wachache kwa makusudi huzihujumu alama hizo ama kwa kuziharibu, kuzigonga na hata kuzikata kwa misumeno na kuzichukua na hivyo kukosekana kwa alama za kumuongoza dereva na mtumiaji mwingine wa barabara.

Kwa upande mwingine madereva wengi huwa hawazingatii alama zilizowekwa barabarani na hivyo kuendesha vyombo vya moto kwa mwendo wa kasi kwa makusudi na matokeo husababisha ajali ambazo husababisha majeruhi na vifo.

Mhe. Naibu Spika, alama za mwendo wa juu wa kasi kwa mujibu wa barabara zetu hapa nchini ni kilomita 60 na 80 kwa saa kwa maeneo yasiyokuwa na msongamano wa makaazi ya watu kwa maeneo ya msongamano wa watu ni kati ya kilomita 20 hadi 50 kwa saa. Alama nyingine ni kwa ajili kwa watu wakuvuka barabara, alama ya madaraja, alama ya taa za kuongoza gari kwenye makutano, mistari ya kugawa barabara nk. Alama zote hizo huwekwa kwa ajili ya kuzingatia usalama wa watumiaji barabara.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Kweli serikali inajua kama barabara nyingi hazina alama za kutosha za kuongozea madereva na watumiao barabara;

(b) Polisi anajua kutokana na mambo yafuatayo:-

i) Kwa kujua kiwango cha mwendo uliowekwa kwenye alama iliyokuwepo ambayo ilihujumiwa kitu ambacho kisheria haimhalalishii dereva kufanya kosa;

ii) Uzoefu wa muda mrefu wa kutambua mwenendo wa kiwango cha mwendo unaokubalika kwenye eneo husika la barabara kwa ajili ya usalama wa watu wengine wanaotumia barabara;

iii) Dereva kuendesha mwendo wa kasi bila kuzingatia usalama wa barabara licha ya kutokuwepo alama pahali hapo hasa maeneo ya msongamano wa watu;

iv) Baadhi ya madereva kupuuza alama zilizopo kwa kujifanya hajaziona nk

(c) Sidhani kama polisi anaweza kumkamata dereva kwa kumuonea ni lazima atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria za Usalama Barabarani. Mbali ya alama za barabarani, Jeshi la Polisi limepewa mamlaka ya kulikagua gari ili kujiridhisha kama ni salama kwa matumizi ya barabarani na watu wanaotumia gari hilo akiwemo na dereva, hivyo yamkinika pia polisi akabaini kuna makosa ya kiusalama kwenye gari na ndipo anapochukua hatua za kisheria na kwa maadili ya kazi zake hatakiwi kumuonea mtu kwani mwisho wa siku hutakiwa kumfikisha kwenye vyombo vya sheria ili haki itendeke. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swala dogo la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba alama nyingi katika barabara nyingi hazima alama hizo ambazo zinaleta usumbufu kwa madereva na abiria.

Je, Mhe. Naibu Waziri ana mpango gani kwa wizara yake kuweka alama hizo ili kuondosha usumbufu huo kwa wananchi wetu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Shaib Said Ali kama ifuatavyo:

Ni kweli tunakiri kwamba hizo alama zipo na sisi tutaendela kila hali ya fedha inaporuhusu kuzitia alama hizo. Lakini licha ya hizo kama nilivyosema mwanzo madereva wanapokuwa kwenye vyuo vya kushomeshea udereva huwa wanafahamishwa zile alama zote *speed* yake ngapi na ngapi katika mji na kutokuwa katika miji.

Kwa hiyo, dereva aliyepitia katika skuli hizi za udereva lazima atakuwa anazijua hizi alama, lakini na sisi tutaendelea kulifanyia kazi hilo suala. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na mimi ningependa nimuulize suala dogo tu la nyongeza Mhe. Naibu Waziri na nategemea majibu yake yatakuwa pia madogo na mafupi.

Mhe. Naibu Spika, kwa miaka mingi sana sasa kwa barabara yetu inayotoka mjini kuelekea Mkoa wa Kaskazini ambayo inatumika sana na wageni pamoja na Wazanzibari watu tafauti. Lakini kuna madaraja yale ya Zingwe zingwe pamoja na Kitope ambayo nyakati za mchana na usiku hazina vile vyuma vya pembeni kuzuia pamoja na alama za muonesha kwamba pale pana madaraja ambayo ni membamba.

(a) Sasa Mhe. Naibu Spika, nataka Mhe. Naibu Waziri anijibu swali langu kwa ufupi sana. Watu wangapi wanatarajia wao wageni na rai mpaka wafe ndio wataweka zile alama pamoja na vyuma ili kulinda maisha ya watu anijibu kwa namba.

(b) Katika Jimbo langu la Tunguu eneo la Dunga Mitini ile ni *T-junction* na pamekuwa sasa magaari mengi yanayopita kutoke M genihaji pamoja na kutoka Dunga Kinyongo mpaka kuelekea upande wa Dunga Kiembeni yanapita kwa kasi kubwa sana pamoja na magari ambayo yanatokea mjini. Kwa hivyo, nataka nifahamu kitu kimoja kwa kuwa eneo lile sasa lishakuwa hatarishi hakuna hata zile *speed bams* nataka nifahamu je wanhitaji ajali ngapi zitokee na watu wangapi mpaka wafe ndio wataweka zile *speed bams* kulinda maslahi pamoja na maisha ya binaadamu hasa Wazanzibari wanaoishi hapa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Simai Mohamed Said unamwambia Mhe. Naibu Waziri ajibu kwa ufupi wewe mwenyewe unauliza maswala kwa urefu. Mpe raha ajibu anavyotaka mwenyewe Mhe. Waziri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said kwa ufupi sana tena si kama yeye alivyoniuliza.

Mhe. Naibu Spika, sisi serikalini tunajali maisha ya binaadamu na tutahakikisha kwamba tunaendelea kuwalinda binaadamu wetu na pale ambapo sasa alama zitakuwa zipo tutahakikisha tunaziwekea alama na yale madaraja kama ulivyosema karibuni tutayajenga kupitia barabara ile ya Kaskazini. Kwa hivyo, naomba avute subira. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

UTARATIBU

Mhe. Naibu Spika: Nakusikiliza wewe sema tu hiyo shida yako.

Mhe. Simai Mohamed Said: Suala langu la b hakunijibu la Dunga Mitini.

Mhe. Naibu Spika: Suala halikujibiwa?

Mhe. Simai Mohamed Said: Amejibu swala moja tu amejibu suala la Kaskazini la Dunga mitini kwenye *T-junction* hakujibu.

Mhe. Naibu Spika: Haya Mhe. Naibu Waziri, naomba ujibu swali la Mhe. Simai Mohamed Said.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nilimjibu maswali ya a na b kwa pamoja. Lakini nitamjibu tena.

Kama nilivyosema kwamba pale hali inaporuhusu tutaendelea kuweka alama lakini kama nilivyosema mwanzo tu sehemu zenye msongamano dereva hatakiwi kuendesha mwendo wa kasi zaidi ya *speed* 50. Kwa hiyo, hilo anatakiwa dereva yeyote aliye makini alijue hilo kwa dereva asiyejua unamakini huo basi nina imani hajapita katika chuo kapata leseni kwa njia isiyo halali. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kujibu suala dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swala dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri umesema kwamba unahitaji bajeti ili kuweza kufanya kazi hii yaani kuweka alama barabarani. Lakini kuna baadhi ya barabara kama mfano ya Chake- Mkoani barabara hii haina alama za barabarani. Je, ni bajeti kiasi gani inahitajika ili kuhakikisha kwamba alama za barabarani zinawekwa kuondoa ajali za mara kwa mara zinazotokea barabarani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake kama ifuatavyo:-

Nyote mnajua kwamba barabara ya Mkoani- Chake ilijengwa na Prismor hapo kabla nasikia iko alama. Lakini kwa bahati mbaya kama nilivyosema mwanzo katika swali mama kwamba wananchi wanazichukuwa zile alama. Lakini kama nilivyosema tutaendelea kuhakikisha kwamba pale ambapo alama zile hazipo basi tutazeweka ili isiwe sababu ya madereva kuvunja sheria za usalama barabarani. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 56

Ununuzi wa Kifaa cha Kukokotea Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba

Mhe. Suleiman Makame Ali (Kny. Mhe. Omar Seif Abeid) – Aliuliza**:**

Kwa kuwa siku ya tarehe 29 Juni, 2017 ndege ya Kampuni ya *"Zan Air"* ilipata pancha muda mfupi tu baada ya kutua kwenye Uwanja wa Ndege wa Pemba na ikaendelea kubaki kwenye njia hiyo ya kurukia na kutulia ndege kwa muda mrefu hadi ilipoletwa tairi ya akiba kutoka Dar-es-Salaam jambo ambalo lilisababisha ndege nyengine zisiweze kutua kutokana na kukosekana kwa chombo cha kukokotea ndege inapopata tatizo kama hilo.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuweka kifaa au chombo ambacho kinaweza kuzikokota ndege pindi zinapopata hitilafu na kupisha ndege nyengine zikaweza kutua na kuruka katika uwanja huo bila ya matatizo.

(b) Je, wizara haioni kwamba kuwaachia wamiliki wa ndege zitakazopata ajali kama hizo ambazo zinazuia ndege kutoa huduma kunasababisha hasara kwa Mamlaka husika na usumbufu mkubwa kwa abiria ambao wanategemea wapate huduma za usafiri kwa muda waliopangiwa.

(c) Je, chombo kama hicho kipo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kazi za kuondoa ndege uwanjani inapopata hitilafuni ni ya mwenye ndege mwenyewe na iInahitaji utaalamu ambao waendesha kiwanja katika kiwanja (*ZAA*) lakini kule Pemba hawana.

(b) Suala la hasara ni kwa Mamlaka kuwawekea utaratibu wa muda kwenda kuondoa ndege yao na ikiwezekana kuwapa adhabu wakishindwa kutekeleza kwa wakati.

(c) Chombo hicho katika Kiwanja cha ndege cha Pemba hakipo kama nilivyosema mwanzo isipokuwa katika Kiwanja chetu cha *Abeid Amani Karume International Airport* hapa Unguja vipo na vinasimamiwa ma Kampuni husika. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba chombo cha kukokotea ndege uwanjani Pemba hakiko. Je, huoni kwamba ni athari inapotokezea tatizo hilo na ni lini kitapelekwa chombo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli hicho kifaa wanacho mashirika machache na hapa Zanzibar wanacho *Zan Air* na *Tropical*. Lakini kwa mujibu wa miongozo yetu ambayo inatokana na Sheria za *TCAA* vile vile na Kanuni zake ni kwamba, *operator* au yule mwenye ndege ndiye anatakiwa kile chombo kuwa nacho na pale asipokuwa nacho, basi anakwenda kwa wataalamu husika wa mashirika mengine, ili apate kuondosha ile ndege inapopata hitilafu yoyote. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, katika ripoti yao Mhe. Naibu Waziri walipowasilisha Barazani waliongea mambo mengi kuhusu masuala ya viwanja vyetu vya ndege hasa Unguja pamoja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, moja ambalo linaendana sambamba na suala lake hili, nataka nifahamu suala la *ILS*, ambayo ni *Instrumental Land System* kwa upande wa Pemba uwanja huu. Je, serikali ina mpango gani ili kuhakikisha kwamba kutokana na kukua kwa suala la usafiri baina ya Unguja na Pemba pamoja na Pemba na Tanga, wataweza kuweka suala la chombo kizima hiki cha *ILS*, ili kuhakikisha kwamba uwanja wetu huu pia unatambulikana kimataifa. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako, napenda kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, hiki chombo tayari kwa kupitia *TCAA* watatupatia katika bajeti ya mwaka huu. Hivi karibuni nilikuwa pamoja na Kamati ya Ardhi na Mawasiliano na wakatuhakikishia kwamba katika bajeti hii hiki chombo kitaletwa na kitafungwa hapa Uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea na hoja za serikali, naomba nitoe matangazo mawili ambayo nimeletewa hapa na nimetakiwa niyatoe na hasa kwa sababu Waheshimiwa Wajumbe wengi sasa hivi wanaondoka. Kwa hivyo, nitakuwa siwatendei haki kama hawakupata hizi taarifa.

Waheshimiwa Wajumbe, tangazo la mwanzo ni kutoka kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, anatoa mualiko kwa Waheshimiwa Wawakilishi wote, kwamba Mwenge wa Uhuru leo utalala Pongwe Pwani. Kwa hivyo, anatutaka tujumuike kwa pamoja na gharama za chakula na malazi ni juu ya uongozi wa Jimbo la Chwaka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tangazo jengine ni kuhusu taarifa ya michezo *league* ya *PBZ* Mkombozi *Cup*. Tunajulishwa kwamba Timu yetu ya Baraza la Wawakilishi, ambayo inajumuisha Waheshimiwa Wajumbe pamoja na watendaji wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, jana iliwaendesha mchakamchaka vijana wa Mhe. Rashid Ali Juma, yaani Timu ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kuwafunga goli moja bila. Mchezo huo ulichezwa katika uwanja wa timu ya Malindi. *(Makofi)*

Pia goli hilo la ushindi limefungwa na mshambuliaji wetu wa hatari ambaye ni Fundi Mitambo wetu Ndugu Fuad Rashid. Nyota wa mchezo wa jana alikuwa ni Rais wa Wafanyakazi wa Baraza la Wawakilishi Ndugu Ali Pandu Ali. *(Makofi)*

Kwa matokeo ya ushindi wa jana Timu ya Baraza la Wawakilishi imeshajiwekea *point* tatu. Mchezo unaofuata tunategemea kucheza na *ZECO* Jumapili ijayo katika uwanja wa Ziwani. Kwa taarifa hii Waheshimiwa Wajumbe na wafanyakazi pamoja na mashabiki wote wa Timu ya Baraza la Wawakilishi, tunajulishwa kwamba mazowezi yataendelea tena kesho katika uwanja wa River Tiba Uwanja wa Ndege wakati wa saa 7:15 mchana. Tunaombwa shime kuhudhuria kwa wingi, ahsanteni sana.

HOJA ZA SERIKALI

Ripoti yaWizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa kabisa naomba kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa hoja, ushauri, maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wizara yangu ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Muumba wa yote, mwenye kuneemesha neema kubwa hapa duniani na mwenye kuneemesha neema ndogo kesho twendako, kwa kutujaalia uzima, hekima, busara na afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kila siku ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Aidha, tunamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze ili tuweze kujadili mambo muhimu ya maendeleo ya taifa letu na kutekeleza kazi ya kuwatumikia wananchi kwa hekima, busara, uwadilifu na mafanikio yenye ufanisi mkubwa kabisa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukrani hizo kwa *Allah*. Sasa naomba nitumie fursa hii ya pekee kumpongeza kwa dhati ya nafsi yangu na kwa niaba ya wizara yangu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake bora na mahiri, wenye busara na hekima ambao umeleta maendeleo endelevu yaliyo makubwa kwa wananchi wa Zanzibar kwa kipindi chote cha uongozi wake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa juhudi zake kubwa za kumsaidia na kumshauri vyema Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza nchi na kuleta manufaa yanayoonekana wazi, kwa wananchi wa ndani na nje ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vile vile bila ya kupitikiwa napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumpongeza kwa dhati kabisa Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, na yeye tunamuombe kwa Mwenyezi Mungu amjaalie uwezo, hekima na busara katika kuiongoza vyema kamati yetu ambayo Mhe. Spika, na uongozi wake mmeichagua kwa makini kabisa.

Aidha, naomba kuwapongeza wajumbe wote wa kamati yetu ambao kwa umoja wao hutusaidia kwa kiasi kikubwa kabisa katika kutoa miongozo na ushauri juu ya kutatua changamoto za wizara yangu kwa lengo la kufikia malengo tuliyojipangia.

Mhe. Naibu Spika, madhumuni ya ripoti hii ni kutoa taarifa ya utekelezaji wa hoja, maoni na ushauri wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ambayo waliyatoa wakati walipotembelea taasisi za wizara katika kuangalia utekelezaji wa taasisi hizo

kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kama ilivyopitishwa na wajumbe kwenye bajeti hiyo na maagizo yaliyotolewa na serikali kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ilipokea jumla ya hoja kumi ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii zinazohusiana na taasisi tano ndani ya wizara yangu, ambazo ni Shirika la Utangazaji Zanzibar, Kampuni ya Usambazaji Maudhui, Kamisheni ya Utalii, Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale, pamoja na Baraza la Taifa la Michezo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, tulifuatilia kwa kina ushauri, maoni na miongozo yote iliyotolewa na kamati pamoja na maagizo kutoka serikalini na kuchukua hatua za utekelezaji kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa hoja ushauri na maoni ya kamati kwa sekta ya habari.

Hoja ya 1. Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kufuatilia kwa karibu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali suala la *AGAPE* na hatima yake kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ilifuatilia kwa kina masuala yote ya *AGAPE* yanayohusu madai kwa pande zote mbili, ukamilishaji wa vifaa vya miundombinu pamoja na mikataba ya ununuzi wa vifaa na umiliki wake. Suala hili napenda kuwajulisha wajumbe kwamba limekamilika na limemalizika kabisa.

Hoja ya 2. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, kuangania namna gani serikali itaweza kuwapa kifuta jasho watumishi wa *ZMUX*, yaani Shirika la Maudhui waliofanyakazi katika kipindi ambacho *AGAPE* aliondoka na wao kulazimika kumaliza kazi zote zilizowachwa.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kwa vile hakukuwepo na mkataba wa makubaliano na kuziogopa sana Kamati za Baraza la Wawakilishi, kwa kazi kati ya *AGAPE* na Watumishi wa Kampuni ya Maudhui, yaani *ZMUX* katika kumalizia kazi ambazo *AGAPE* ameziacha, kumepelekea kuwa vigumu kabisa kwa wizafa yagu pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, kupata njia ya kisheria kwa jinsi gani ya kuwafanyia malipo kwa watumishi hao.

Hata hivyo, Wizara yangu ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo inaendelea kuwapa motisha mbali mbali wafanyakazi wetu hao kwa kazi nzuri tena ya kizalengo wanayoifanya.

Hoja ya 3. Mhe. Naibu Spika, tulitakiwa Shirika la Utangazaji Zanzibar kuhakikisha kuwa linakuwa na utaratibu maalum unaoeleke kwa waunganishaji wa taarifa za habari, yaani *video editors*, kuhusisha habari za kutoka Unguja na Pemba, ili kutatua changamoto iliyopo ya kutoonekana kwa baadhi ya wakati habari kutoka Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa hoja hii Shirika la Utangazaji lilikamilisha ufuatiliaji wa hoja hii. Pia limeandaa utaratibu maalum wa uunganishaji wa taarifa za habari, yaani *video editors*

katika kupata habari za kutoka Kisiwani Pemba, ambapo habari hizo hutumwa kwa njia ya mtandao na kujulisha kwa simu wakati habari hiyo imeshatumwa na kuthibitisha kupokewa kwake.

Hoja ya 4. Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kuhakikisha kuwa *studio* za *ZBC* Pemba zinafanyiwa kazi ipasavyo, kwa kuwepo watumishi wanaotumia vifaa vya kisasa pamoja na vipindi mbali mbali viwe vinatayarishwa Pemba. Hii itasaidia kuwapa ujuzi watumishi waliopo, lakini pia itawasaidia katika kuwajengea uwezo wao wa kazi na kwa wakati mmoja.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa hoja hii ni kwamba *ZBC* imeweka utaratibu wa kuwafundisha wafanyakazi wa Pemba kuja kujifunza katika *studio* za *ZBC* Unguja, na pia katika utekelezaji wa hoja hii tumeandaa utaratibu maalum wa kuwapeleka kwenye mafunzo waandishi na tunatarajia kuwaajiri mafundi wenye sifa na wazalendo wa Televisheni Zanzibar hivi karibuni.

Katika Sekta ya Utalii

Hoja ya 1. Kuongeza fungu la bajeti katika Kamisheni ya Utalii kwenye programu ya utangazaji na uhamasishaji wa utalii, ili wageni wengi zaidi na wa kiwango cha juu kuja kutembelea nchi yetu na kuipatia serikali mapato yanayotokana na sekta hii ya utalii ambayo kwa sasa inaongoza.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wake. Fungu la Bajeti ya Kamisheni ya Utalii kwenye programu ya utangazaji na uhamasishaji wa utalii limeongezwa kutoka shilingi milioni 208,505,000 mwaka 2016/2017 hadi kufikia shilingi milioni 366,590,000 mwaka huu wa fedha 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 76.

Hoja ya 2. Kumfungia Ndugu Peter Obama wa Kiwengwa pamoja na wawekezaji wote wenye vitendo vinavyofanana na Peter Obama vya kuwasumbua wananchi kwenye maeneo yao, hadi pale atakapokidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria zetu.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji katika hoja hii. Kamisheni ya Utalii imeufungia mradi wa Masai na Simba, unaomilikiwa na ndugu Peter Sipano kutokana na mradi huo kutofuata taratibu za kisheria za usajili. Kamisheni ya Utalii ilimtaka ndugu Peter Sipano kufuatia taratibu zilizowekwa za usajili wa miradi ya utalii. Baada ya kupata barua ya kufungiwa kwa mradi wake ndugu Peter Sipano, aliwasilisha ombi la kuanzisha mradi wa kulaza wageni, lakini hadi kufikia mwisho wa utekelezaji wa mwaka 2016/2017 hajatimiza masharti yaliyowekwa ya uanzishwaji wa mradi kama huo.

Hoja ya 3. Kuanzisha *database* itakayosaidia kuelewa hoteli zote na nyumba zinazolaza wageni ili kodi stahiki ziweze kukusanywa, *database* hiyo iwe na taarifa zote za hoteli ikiwemo idadi ya vyumba na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa hoja hii Kamisheni ya Utalii imetengeneza mfumo wa *database* wa uwekaji wa taarifa za miradi ya utalii, ikiwemo nyumba za kulaza wageni kazi inayoendelea ni kufanya uhakiki wa taarifa za miradi ya nyumba za kulaza wageni na kuzisajili katika mfumo mpya uliyotengenezwa.

Hoja ya 4. Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kubuni njia muafaka na nzuri zaidi katika ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo ya kihistoria, ili kuhakikisha kuwa yanayokusanywa mapato ndio halisi.

Utekelezaji wa hoja hii Mhe. Naibu Spika. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale imeandaa mafunzo maalum kwa wakusanyaji wa mapato wote waliopo katika maeneo ya kihistoria ambayo yanaingiza mapato. Pia kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo yote ya kihistoria ambayo yanaingiza mapato ili kuongeza nguvu ya ukusanyaji wa mapato.

Vile vile, idara itahakikisha maeneo yote ya kihistoria ambayo yanaingiza mapato yanakuwa na risiti maalum zinazoonesha kima cha viingilio katika maeneo hayo. Pia idara itahakikisha maeneo yote ya kihitoria yanapata vitabu vya mahudhurio, ili wageni wote wanaotembelea waweze kuwekwa katika kumbukumbu zao.

Aidha, idara kuhakikisha mapato yote yanakusanywa katika maeneo yote ya kihistoria yanapelekwa benki kwa mujibu wa taratibu ziliopo, haraka tena iwezekanavyo, ili fedha za serikali zisikae mikononi kwa muda mrefu pamoja na kuwahimiza watumishi wetu waliopo katika maeneo yote ya kihistoria wanafuata kanuni za utumishi, likiwemo suala zima la kuwa waaminifu na kujiepusha na masuala ya rushwa.

Hoja ya 5. Mhe. Naibu Spika, inatakiwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kuhakikisha kuwa majengo yote ya asili ya Mkamandume na mengineyo, wakati yanapojengwa au kukarabatiwa usipotezwe uhasilia wake, kwani ile ndio historia yenyewe hapa Zanzibar.

Utekelezaji wake Mhe. Naibu Spika. Jukumu la kuhakikisha kuwa majengo yote ya kihistoria hayapotezi asili yake wakati wa matengenezo, ni moja ya mambo ambayo yanasimamiwa kwa vizuri na Idara ya Makumbusho ndani ya wizara yangu. Jambo hili linasisitizwa na sheria ya uhifadhi wa mambo ya kale, sheria na kanuni za taasisi mbali mbali za kimataifa kama *UNESCO* na *World Monument Fund*.

Sekta ya Michezo

Hoja ya 1. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kuhakikisha kwamba Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar linatengewa fedha maalum kwa ajili ya kuvisaidia vyama vyengine vya michezo viliopo Zanzibar, hasa pale inapotokea ushiriki kwenye mashindani ya nchi za nje.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa agizo hili ni kwamba Idara ya Utamaduni na Michezo, inautaratibu wa kuvitengea fedha vyama vya michezo ili kuziwezesha timu kushiriki katika mashindano ya kimataifa. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 idara iliwatengea fedha jumla ya shilingi milioni 76,766,702, kwa ajili ya kuziwezesha timu zetu kushiriki mashindano ya nchi za nje. Idadi ya timu tulizoziwezesha kushiriki mashindano ya kimataifa jumla ni tano. Nazo ni:

1. Timu ya wabeba vyuma vizito nchini Jordan.
2. Zanzibar *Queen* nchini Uganda.
3. Timu ya Viziwi nchini Kenya. na

4. Timu ya Judo *Eleven East African Judo Champion Ship* hapa Zanzibar na
5. Timu ya *Netball, East African Netball Association* nchini Kenya.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na kufungwa bao moja timu yetu ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, naipongeza sana Timu ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hitimisho. Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumaliza naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru watendaji wa Wizara yangu kwa mashirikiano wanayoendelea kutupa pamoja na Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Chum Kombo Khamis, katika kuteleza hoja tunazozipokea kutoka kwa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi, Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii na utekelezaji wa shughuli za kawaida za wizara pamoja na maendeleo. *(Makofi)*

Shukrani maalum ziwaendee Katibu Mkuu ndugu Omar Hassan Omar King, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Amina Omar Issa na watendaji wote wa Wizara yangu ya Hbari, Utalii, Utamaduni na Michezo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mwisho naomba kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu hususan waliomo humu ndani na wale ambao hawapo, kwa kunisikiliza kwa utulivu pamoja na wananchi wote hasa na wajimbo la Amani ambao hivi sasa wapo makini kutusikiliza kipi tunavyokitekeleza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya uwasilishaji huo sasa naomba Wajumbe wako waipokee, waijadili na kushauri katika kuimarisha utekelezaji kazi wa Wizara yangu, Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri, naomba utoe hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Sasa, naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Mhe. Naibu Spika, Kwanza kabisa naomba kuchukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa ukarimu wake wa kutupa uhai, afya njema na nguvu, tukaweza kukutana tena katika Chombo hiki muhimu katika nchi yetu kwa lengo la kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote kwanza niombe tu kwa heshima kabisa kumpongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi zake njema ambazo anazifanya na sisi kama wasaidizi wake ili kuleta maendeleo katika nchi yetu. Lakini pongezi rasmi kwamba tunampongeza Kamati kwa kumteua Dkt. Vuai Lilla kuwa Katibu Mtendaji wa

Kamisheni ya Utalii ya Zanzibar. Tunaamini uteuzi huu Mhe. Naibu Spika, utaleta faraja na nguvu za kazi kuhakikisha kwamba utalii unakua katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa maelekezo ya Kanuni ya 108(15) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi,Toleo la 2016 naomba kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi imepitia Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yetu ya Mwaka 2016/2017 kwa Wizara ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, katika Kipindi cha kazi cha mwaka 2016/2017 Kamati yangu ilitoa Maagizo kumi na Moja (11) kwa Wizara ya Habari, Utalii Utamaduni na Michezo. Kamati inaamini kwamba uchache wa Maagizo haya unatokana na kwamba, masuala mengi yaliyojitokeza wakati wa kazi za kamati yalikuwa yakitolewa ufafanuzi wa kina na wahusika, pamoja na ushirikiano mzuri uliopatikana kati ya watendeji wa wizara hii pamoja na wajumbe wa kamati yangu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inazidi kusisitiza kwa watendaji wa mawizara kushirikiana na kamati zote za Baraza la Wawakilishi na kuwapatia Waheshimiwa Wajumbe wako, taarifa zote muhimu wanazozihitaji zinazohusiana na utendaji wa taasisi zao kwa lengo la kuhimiza uwazi na uwajibikaji katika taifa letu.

Sekta ya Utali

Mhe. Naibu Spika, katika agizo kwanza kwa wizara hii linalohusiana na kuongeza fungu la bajeti ya Kamisheni ya Utalii, Kamati imeridhika kwa kuongezwa kwa fungu hilo kutoka shilingi 208,505,000 mwaka wa fedha uliopita hadi kufikia shilingi 366,590,000 kwa mwaka huu wa fedha wa 2017/2018 ikiwa ni ongeeko la asilimia 76. Kamati inamini kwamba ongezeko hilo litasaidia kwa kiasi kikubwa kwenye Programu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii kama alivyokwisha kueleza Mhe. Waziri wa masuala ya utalii.

Ni mategemeo ya mamati yangu kwamba, kutakuwa na ongezeko kubwa la watalii hapo baadae kwa kuwafanya wavutike zaidi na warudi tena katika visiwa vyetu na hatimae nchi yetu kupata pato kubwa zaidi linalotokanana na sekta hii ya utalii.

Mhe. Naibu Spika, Kuhusu Kadh-ya ya Ndugu Peter Sipano Obama ya Mradi wa “Masai na Simba” huko Kiwengwa. Kamati inaunga mkono hatua zinazochukuliwa na Kamisheni ya Utalii na tunazidi kushauri kufuatiliwa zaidi muwekezaji huyo, huku Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Wilaya zikishirikishwa kikamilifu katika hatua zote zinazoendelea.

Sekta ya Habari

Mhe. Naibu Spika, Kuhusiana na suala la *AGAPE* na *ZMUX*. Kamati yangu inazidi kuisisitiza wizara na serikali kwa ujumla kuwa waangalifu wakati wa ufungaji wa mikataba pamoja na kuwashirikisha wanasheria wetu kwa kuangalia maslahi ya taifa, matakwa ya kisheria pamoja na maslahi na matakwa ya kitaalamu, ili kujiepusha na matatizo yanayoweza kujitokeza hapo baadaye.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa *ZBC***.** Kamati yangu inaridhishwa na mfumo ulipo hivi sasa wa utoaji wa taarifa za kutoka mikoa yote ya Zanzibar. Aidha tunazidi kutoa pongezi zetu kwa *ZBC* kwa kuzipa umuhimu habari za vijijini ikiwemo matangazo ya kila siku ya moja kwa moja kutoka Pemba. Lakini pia tunaipongeza *ZBC* hii Redio kwa kuanza Kipindi Maalum cha Michezo kutoka saa 2.15 hadi saa 3.00 usiku, tunaipongeza sana na wanamichezo naamini wameridhika na hilo.

Vile vile, kamati imeridhika na utaratibu uliowekwa na *ZBC* kwa kubadilishana watendaji kati ya Studio ya Karume *House* Mnazimmoja na Mkoroshoni Pemba ikiwa ni njia moja wapo ya kubadillishana uzowefu.

Kamati inazidi kuipongeza tena *ZBC* kituo cha Dar-es-Salaam kwa jinsi wanavyotowa kipaumbele kwa waheshimiwa kutoka Zanzibar wakati wanaposhiriki katika matukio mbali mbali huko Tanzania Bara.

Sekta ya Michezo

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inaunga mkono utaratibu ulielezwa na Mhe. Waziri wa kuvisaidia vilabu vinavyoshiriki katika mashindano ya kimataifa. Kamati inapenda kuchukua fursa hii kuviomba vilabu na wanamichezo kwa ujumla kuongeza bidii michezoni ili kuhakikisha visiwa vyetu vinazidi kutajika katika ulimwengu wa michezo ikiwa ni njia moja wapo ya kuitangaza nchi yetu kiutalii.

Sekta ya Utamaduni

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu, inawashauri watendaji wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kuyatumia ipasavyo mafunzo wanayoyapata juu ya ukusanyaji wa mapato katika maeneo yao ili kuondokana na dhana iliyopo ya kushuka kwa mapato hayo katika sekta hiyo.

Aidha nikiwa namalizia katika Wiara hii ya Habari, Utalii Utamaduni na Michezo, nizungumzie kidogo juu ya agizo linalohusiana na suala la utunzaji wa majengo ya kihistoria. Kamati yangu inasisitiza juu ya kuongeza juhudi ya kuyalinda na kuyahami ikiwezekana hata kwa kuingia ubia ili kulinda historia yetu pamoja na kuongeza mapato ya idara hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia hotuba yangu kamati yangu inazidi kusisitiza kwa wizara hii kuzidi kushirikiana na kamati yangu, ili kufanikisha vizuri majukumu tuliyopewa na Baraza letu tukufu.

Aidha Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wafanyakazi wote kwa kutupa mashirikiano mazuri katika ziara zetu siku hadi siku, kuanzia Unguja, Pemba hadi Bara, tunachukua fursa hii maalum kutoa wito tu kwamba tuongezee bidii, ili ufanisi upatikane zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano yao waliyonipa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi hii, kwa ruhusa yako naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Mwenyekiti
2. Mhe. Salha Mohammed Mwin'juma - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Maryam Thani Juma - Mjumbe
4. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Mjumbe
5. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Mjumbe
6. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
7. Mhe. Mussa Foum Mussa - Mjumbe
8. Ndg. Himid Haji Choko - Katibu
9. Ndg. Mussa Issa Mussa - Katibu
10. Ndg. Amina Abeid - Mkalimani

Nimalizie kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu mkubwa.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana, Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii.

Waheshimiwa Wajumbe, tunao wachangiaji watatu na mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Simai Mohammed Said, atafuata Mhe. Rashid Makame Shamsi na wa mwisho atakuwa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Simai Muhammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona. Nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii leo ya kufika hapa na kuwa mzima wa afya, lakini pia niweze kutoa mapendekezo au maoni ili kuichangia hii ripoti yetu juu ya Taarifa ya utekelezaji wa hoja maoni na ushauri wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 katika Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Naibu Spika, tangu wiki iliyopita hapa tumekuwa tunajadili ripoti tofauti za mapendekezo kutoka maagizo ya kamati huzika za Baraza, lakini pia ripoti ambazo sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuweze kuzichangia. Katika ripoti zote zilizokuja hii ndio ripoti fupi kabisa katika zote iliyosomwa leo na Mhe. Waziri ina kurasa kumi (10).

Lakini pia katika hotuba zote zilizosomwa wenyeviti wa Kamati ripoti hii iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa kamati husika ndio fupi katika zote, sasa hapa kuna mawili moja kwamba wizara inafanya kazi vizuri sana, au la pili kamati imepitia juu juu haikuingia kwa undani kabisa kufanya kazi ambazo tunahisi. Nasema hivyo kwa sababu ya vitu viwili, wizara hii ina mambo mengi sana ni mnyororo ni habari sehemu kubwa, tunapoongelea kuhusu habari tunaangalia habari za *print medium* ambayo ni kwenye maandishi ya magazeti, na kuna *electronic medium* ambazo sasa kuna mambo mengi ndani yake.

Lakini pia kuna utalii ambao ni uchumi wetu wa nchi hii, lakini humo ndani pia kuna utamaduni ambao unagusa wananchi lakini pia na vivutio vyetu, halafu kuna michezo. Sasa ukiangalia

nahisi kuna mambo mengi tungeweza kuyapata kwa undani kabisa katika maagizo. Kwa hivyo, niseme tu kwamba nishauri kamati kwa miezi ya mbele watakavyokwenda basi wajitahidi sana kuingia kwa undani kabisa, ili na sisi tuweze kupata mengi zaidi katika kuyachangia.

Mhe. Naibu Spika, nianze tu kwa kusema kwamba katika ripoti hii nitachangia kwa ujumla kwa sababu inabidi niingie na undani nitoke niingie nitoke, ili niweze kumsaidia Mhe. Waziri na wizara katika mambo hayo ambayo yanawagusa.

Suala la kwanza nitaanza na jimboni kwangu Bungi. Mhe. Waziri kuna wafanyakazi Bungi wamefanya kazi kwa miaka saba lakini wameondoshwa kazini na barua waliyopewa haina mwelekeo mzuri. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri tunachokuomba uingilie ili tuhakikishe kwamba hawa watu ambao wamefanya kazi kwa zaidi ya miaka saba juu ya ulinzi na kulinda kadhia ile baada ya kupelekwa wapiganaji wetu, basi na wao haki yao itambulike au waheshimike na wapate kile wanachostahiki.

Lakini pia niseme kwamba kwenye ripoti hii ningependa nione suala zima la Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati linapokuwa katika *in session*, mbona hatuoni vipindi katika *ZBC* vikirudiwa ambavyo vinaunganishwa kama vile wanavyofanya *TBC* ama vile ambavyo tunahisi sisi vinatugusa kwa upande wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, nahisi watu kutoka Zanzibar au Wazanzibari wanakosa kupata taarifa za moja kwa moja kwa yale mambo ambayo yanayotugusa.

Sisi kama Baraza la Wawakilishi tuna wabunge watano tumewachagua lakini tunapata tabu sana kujua katika kazi zao wanavyozifanya tupate kuziona *live* wanapozungumza au katika zile *record* ambazo tunaziona katika *ZBC* au marudio.Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo nataka tuone waandishi kutoka *ZBC* wanahusika na wanafanya kazi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Lakini nataka niongelee katika hoja ya tatu juu ya mapato na maeneo ya malazi kwa kuweka huo mfumo wa *Database System* kutambua hoteli ziko ngapi, Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nachangia juzi nilisema kwamba kuna huu mtandao unaitwa *Air BMB* ukenda katika mtandao huo sasa hivi kwa nyumba ambazo ziko *registerd* Zanzibar zinafika hata vyumba 2000, vyumba 2000 maana yake ni hoteli zaidi ya 3 au 4, sasa hawa wageni wanaokwenda kulala maeneo haya mimi sikatai mtu akodishe nyumba yake ili apate riski, lakini pia ni vizuri tukawatambua hawa wagei wapi wanalaza na kama hizi nyumba kweli watu wanastahiki. Nasema hivyo kwa sababu mbili.

(i) Usalama wa mgeni unakuwa haupo ikiwa mwanaume ikiwa mwanamke haupo.
(ii) Serikali inapoteza pato kwa mfumo huo kwa sababu hatujui.
(iii) Tunaifanya Zanzibar kuwa lile lengo tunalotaka twende nalo wanauza bei kwa bei ya chini lakini huduma inayotolewa haiendi sambamba.
(iv) Tunakuwa hatujui hali halisi tuna vitanda vingapi Zanzibar na ni muhimu kujua vitanda vyetu tunavyo vingapi na vyumba vingapi, ili tunakwenda sambamba na uchumi wetu tunavyotaka jinsi uende.

Sasa suala la *Air BMB* vitu viwili kuna nchi nyingi sana zinapingana nao mfumo huu. Kwa hivyo, tangazo litoke rasmi kwa serikali na ni marufuku kwa huu mtandao au watu wote ambao

wanataka nyumba zao zisajiliwe ili zitambulika basi masheha wote wajue katika maeneo yote husika.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano leo unakuta mtu analala Fuoni mgeni usiku anachukua *Taxi* kula sasa anafika je kule anarudi vipi. Sasa tuna maeneo tumeya-*allocate*, kwa ajili ya watalii na kuna maeneo tumeweka kwa ajili mtu anweza kukosdisha nyumba yake. Hivyo ni vyema mfumo huu wote tuuangalie upya, basi nashauri hili tuliangalie kwa umakini sana.

Eneo la tatu ambalo nataka nichangie humu ni sehemu za mambo ya kale na amesema Mhe. Waziri wataweka masuala ya tiketi na vitabu na daftari la wageni kuweza kuwatambua, naona mfumo huo umepitwa na muda. Mhe. Naibu Spika, huo mfumo ndio ulioko hivi sasa. Kwa maana hiyo, nashauri kwa yale maeneo ambayo tunaweza kuyaratibu vizuri tuanze kuweka kamera, ili tuone idadi ya watu ambao wanaingia na kutoka.

Lakini pia sasa hivi ukienda Tanzania Bara kama unakwenda Ngorongoro au Manyara unakata tiketi ya kadi yako kutoka mjini inakupa nafasi wewe kuingia maeneo yote. Kwa hiyo, tuwe na *electronic ticket*s, mtu kama anasema nakwenda kutembelea Maruhubi anataka kutembea pango la Mangapwani, anataka kutembelea katika makumbusho yetu unakuwa umesha kata yale maeneo sehemu moja unalipia, ukiondoka unaonesha tu kule, na wala kule eneo isiwe pahala pa kulipia pesa na tuweke kamera kwanza tutapata kujua ni vivutio vipi ambavyo wageni wanaingia na idadi yao.

Vile vile, katika hiyo bei itakayowekwa iwe kuna bei kwa ajili ya wanafunzi Wazanzibari, *East African* pamoja na Afrika na Ulaya kwa ujumla.

Ningependa nione kwenye ripoti hii lakini nisikitike tena sikuiona mwaka ujao Mhe. Naibu Spika, tutakuwa tuna kombe la Dunia 2018 lakini *Link ya Sport Tourism* na Sera ya Serikali pia Utalii kwa Wote, lazima ni nafasi kubwa ya kujitangaza kwa upande wa visiwa vyetu na nchi yetu. Mhe. Naibu Spika, ningependa nione kwamba Wizara ya Utalii kwa kutumia Kamisheni wanapika mkakati mzuri na *TTB*, ili kuhakikisha kwamba wale wageni ambao watakwenda kushiriki katika Kombe la Dunia ile tunaita *out bownds* ambayo Watanzania kampuni za *Tourism* watakuwa wanauza hizi *holl days* kuondoa wageni hapa au Tanzania kwenda kushiriki katika Kombe la Duni.

Kwa kweli, kuna kupokea na kuna kutoa sasa *in bownds* na *out bownds* lakini kuna suala zima la kutangaza tunanua ndege zetu sisi za *Air Tanzania*, sasa tunaangalia vipi katika mfumo huu hasa lazima masuala haya yaanze kuzungumzwa hivi sasa, ili tujue wapi tunapokwenda huko tutakuwa tumejipangaje. Kwa hivyo, Kombe la Dunia ni kitu kikubwa sana nashauri wizara ianze kujipanga sasa hivi pamoja na pacha wake ambayo ni wizara ya Jamhuri ya Muungano suala zima la utalii, ili waweze kwenda sambamba katika mfumo huu wa Kombe la Dunia.

Lakini pia katika data ambazo wageni tunaopokea kuna kitu *VFR*, *Visiting Friends and Relatives* Zanzibar tunapokea sana wageni sasa hivi ambapo mbali tunaita sisi *Diaspora* tunatumia neno moja *Diaspora*. Lakini *VFR* wanatoka Tanzania Baraza wanatoka Kenya, wanatoka Muscat, wanatoka Marekani wanatoka Uingereza wanatoka maeneo mengi, kwenye kadi za kupokea wageni *Airport* tuweke *VFR,* ili tuanze kujua *Visiting Friends and Relatives*

tunakuja kutembelea ndugu na jamaa hawa ni wangapi, ili takwimu zetu zianze kukaa vizuri kwa sababu hawa wanaokuja hapa pia ni wageni hasa katika kadi ambazo ndio za Kamisheni zitumike sehemu ya *VFR* na hili ni muhimu kwa ajili ya namba zetu.

Mhe. Naibu Spika, nililiongea hapa suala la *green seasons* ambayo nikasema utalii wa kijani. Kwa hivyo, ningependa nione hapa baada ya kutoa mawazo hapa kwa sababu, tunakuwa tunatumia nguvu sana Waheshimiwa Wajumbe kubuni mawazo, lakini hatupati majibu kutoka wizara. Kwa mfano, hapa nilizungumza hapa kwa upeo sana suala la *green seasons* tuna msimu minne tunakotoka katika miezi ya mvua kwenye Machi, Aprili na sasa hivi tuna mvua za vuli lakini tunapokwenda katika mvua zile za Machi, walioita ile ni msimu wa mvua ni Wataliana, walipokuja hapa Zanzibar.

Kutokana na hali hiyo, lazima tuigeuze tuite *the green seasons unless* kuna mtu anaweza kuja na neno jengine jipya, lakini tunaposema msimu uko chini au *low seasons* maana yake tunajipiga risasi wenyewe tunawaambia wageni wasije. Sasa mbona kamati na wizara hawajaongelea katika mawazo haya tunayoyabuni ili tuone undani umeingiwa. Mhe. Naibu Spika, ningependa nione Mhe. Waziri, vitu kama hivi vinazungumzwa kwa upana katika sekta ya utalii ambayo mi mnyororo. Lakini pia Mhe. Waziri na Kamati ingependa pia wafanye ziara katika *Terminal II* kwani ile itakuwa ni sehemu moja kubwa sana ya watalii kuingia. Hivyo, kama kuna ushauri wowote tuanze kuupata, ili katika awamu hii tunayokwenda nayo tuwe pamoja.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tumekwenda na kamati yetu tulipofika pale tu, nimeona *arrivalist* ndogo kwa mujibu wa wageni watakaoingia pale wataishia kama sasa hivi, kwa sababu ukiangalia haifiki hata *three hundres square meters*, hivyo kama kuna ndege mbili kubwa zikija za *Air-Bus* hapatoshi, naamini jambo kama hili linamgusa na yeye pia sababu yeye ni Waziri wa Utalii. Kamati pamoja na wizara walikuwa waende waangalie maeneo yote haya kwa undani kabisa, ili kuja kuishauri wizara.

Hata hivyo, Mhe. Waziri japo kuwa hasimamii suala la uchumi lakini suala la utalii ni mnyororo inagusa maeneo yote kila wizara itakuna nao ukenda afya kuna utalii, ukenda wizara ya mawasiliano kuna utalii, ukenda kwa Mhe.Wizara kaka angu Mhe. Haji Omar Kheir kuna utalii kila pahala. Kwa hivyo, maeneo yote haya yeye anakuwa beki 5 anacheza, hivyo lazima angalie kama *center half* anakwenda sambamba mpaka katika wingi wake wa kushoto na namba 7 kule ili tuweze kupiga goli la uhakika kwa kupitia Messi ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Pemba, ndugu zetu kutoka Pemba hasa wanafunzi ambao ni wanawake hawajui kuogelea, michezo ya kumuonesha mwanafunzi katika kuogelea tutafutie mpango mzima ili waweze kujimudu, kwa sababu kujifunza kuogelea ni sehemu moja muhimu kwa binaadamu mbali kwa maisha yake kwa ajili ya afya, lakini kumsaidia yeye mwenyewe ili awe na uwezo kumsaidia pale panapotokeza hatari, kama bahari. Kwa kweli, kwa Mzanzibari yoyote, kwa sababu sisi tumezungukwa na visiwa lazima pawe pana mtu anajua kuogelea baharini.

Kwa hivyo, nashauri wizara ianze kujipanga kwa Mashindano haya ya Kuogelea na kuwa kuwa na *swimming pool*, aidha katika kambi za KMKM au mashuleni lakini pajenge *pool* ambazo za *Olympic size*, ili wakinamama hasa vijana wetu katika mashule waweze, kwa sababu vijana wa

kiume wanaogelea kokote lakini wanawake wanahitaji mavazi yao kujistiri, hatuna bahari tukasema hapa ni kwa ajili ya kina dada, hakuna bahari tukasema sasa hivi ni kwa ajili ya Wazanzibari kustarehe nimezungumza sasa katika suala la *public beach* miaka zaidi ya saba, kwamba maeneo yote tunatoa kwa utalii.

Mhe. Naibu Spika, juzi tumeona na tunampongeza sana Mhe. Said Bakhressa kwa jinsi Wazanzibari walipokwenda kule Fumba wakaona mandhari nzuri, lakini hadi leo hatuna bahari yetu wenyewe tukenda tukaogelea tukajifunza na akinamama. Hivyo, ni vyema tuangalie mfumo huu na waziri hapa nilimuona Mhe. Waziri wa Ardhi, kwa hiyo angalie eneo gani waliokuwa *allocated* kwa ajili ya kinadada wajifunze kuogelea, na hili linagusa wizara hii na pale pia wakinamama watakwenda na biriani yako kula na wapate kukaa kwa raha na kustarehe hasa siku za Jumapili. Wengi tunajua maeneo tuliyokuwa nao *Prison Island* kisiwani, Makunduchi.

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka zama zako ulikuwa ukenda zako Chwaka, Mangapwani unakwenda kule unapumzika vizuri, lakini siku hizi hayapo, lazima tuyaangalie Mhe. Naibu Spika, vitu kama hivi. *(Makofi)*

Lakini kwenye suala la ajira juu ya tangazo zima alilotangaza Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto tarehe 30. Mhe. Naibu Spika, mimi ni mdau wa sekta hii, ni Mlezi wa Jumuia ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii. Naamini agizo hili lina nia njema kwa upande wa serikali, lakini kuna athari nyingi pia zimejitokeza katika sekta ya utalii, hasa katika wale wafanyakazi ambao wanamaliza mikataba yao wanaondoka zao na wale ambao walikuwa *day work* sasa hivi wakifagia, wakisafisha maeneo ya bahari, kubeba mizigo hasa kiwango ambacho kimepandishwa kutoka 7,000/- mpaka 25,000/- kimekuwa kina ukakasi na ugumu kwa maeneo mengi hasa katika mahoteli.

Mhe. Naibu Spika, lazima wizara yako Mhe. Naibu Spika, kufanya utaratibu maalum, kuangalia uwezekano wa kujua athari ambazo zimeingia, mimi ninazo takwimu zangu mwenyewe ambazo nafanya kwa utafiti wangu na naweza kuthubutu mbele yako kwa sababu sio ambazo za uhakika. Lakini kwa kupigia watu kuwauliza ni watu karibia zaidi ya 2,000 mpaka 3,000 Mhe. Naibu Spika, wameshatoka katika sekta ya utalii kupoteza kazi zao, hawa wana *include day workers* na wale ambao wamemaliza mikataba, na kwa wale ambao wanataka waingie panakuwa pagumu na kila miezi itakapoenda wale waliokuwa wanamaliza wanatoka.

Kwa hivyo, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo iangalie kwa ukubwa hasa kwa pia kwa upande wa Pemba. Pemba tunazo hoteli tatu kuna Manta kuna Theayana halafu Misali na Fungu Lagoon. Lakini kwa uchumi wa Pemba na kwa jinsi viwango hivi vilivyotangazwa itakuwa ni vigumu sana kutekelezwa na huku tunataka Pemba pia kwenda kujengwa, hasa Wizara ya Fedha na Mipango nayo iangalie, sana kwa sababu hata hiyo miradi ambao utakuja kuekwezwa Zanzibar ya utalii na kufungua hicho kisiwa cha Pemba patakuwepo na ugumu sana.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa sekta nzima ya ujenzi imeathirika kutokana na agizo hili, na niseme naona tabu sana lakini kwa kweli kuna hatari ya watu wengi na hili jambo kuumiza hata Ilani yetu ya CCM. Naomba kushauri Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ametangaza na wewe

umekaa kimya kwa sababu mnasema ni *collective responsibility*. Lakini Waziri wa Kazi ndie mwenye dhamana aliyopewa, sasa wewe kama waziri wa utalii unatakiwa ulinde sekta yako na ufanye utafiti wa kina wa undani kwa sababu hawa wenye mahoteli wanakuwa wagumu sana kukwambia wangapi washachinja.

Lakini, ukweli wanapotoka hawakwambii kwa sababu mtu anaona tabu lakini agizo hili, limefanyika watu wanatoka na ni wengi na malalamiko yapo. Mhe. Naibu Spika, naomba kushauri Mhe. Waziri katika sekta ya utalii na sekta ya ujenzi kwa kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, ufanywe utaratibu naamini katika bajeti ya 2018 humu ndani na sisi tutakuwa na taarifa za kutosha na ziada.

Nimalizee Mhe. Naibu Spika, juzi Ijumaa nilifanya ziara kwenye uwanja wa Mnazimmoja, kuangalia lile bomba la maji lililotengenezwa kwa mradi wa *ZUSP* nilipokwenda kule mbele nikagundua kwamba yale maji sasa yanakuwa yanakwamba kule mbele, na niseme ile paipu maji iliyotengenezwa haiendi na Mhe. Naibu Spika. Kwa kweli, nimepiga picha ambayo ni hii hapa unaona kabisa kwamba hapaendi maji na ule mchango unajaa hasa sijui kwamba ilikuwa ni lengo lake mvua inaponyesha Mnazimmoja yanatakiwa yale maji ya yende kule baharini. Kutokana na hali hiyo, nashauri kama mchanga umeziba kule mbele, basi Mhe. Waziri akaangalie kwa sababu yale malengo tuliyokuwa tumeyakusudia tuweze kuyafikia kwa kupitia wizara husika na yeye pia katika kuangalia vijana wake au vijana wetu wa Zanzibari wanatumia viwanja kwa ajili ya michezo.

Mhe. Naibu Spika, namalizia mwisho ningependa nitoe mawazo juu ya taarifa ya habari. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi taarifa ya habari inasomwa saa 1.00 usiku wengine wanasoma saa 2.00 wengine wanarudia saa 3.00 ndugu zetu kutoka Kenya wana ya Kiswahili na Kiingereza, wanaanza na Kiswahili lakini saa 3.00 kuna Kiingereza. Nashauri tutafute utaratibu kuwauliza Wazanzibari kwa kupitia kutumia kampuni ya Simu ya *ZANTEL*, wangependa taarifa ya habari isomwe saa ngapi, saa 1:00 - 1:30 saa 2:00 - 2:30 saa 3:00, kwa sababu wakati wa saa 2:15 kuna wakati mwengine wanakuwa kwenye swala na wengine tunajua tukitoka kwenye swala, ushamaliza kusali unapita Barazani kutia *story* sasa huwa tunakosa muda wa kupata taarifa ya habari kuangalia. Kwa hiyo unaweza kutumia *ZANTEL* watu wakatuma ujumbe mfupi, kutoa mapendekezo yao ili tuweze kujua.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, naona unaanza kujivuta mbele kwa malengo kutaka kunijuulisha kwamba muda wangu umemaliza, nikiri kweli umemaliza muda. Nichukue nafasi hii kukushukuru sana Mhe. Naibu Spika, Mwenyezi Mungu, azidi kutulinda na muongozo wako unapokuwa mzuri na nimshukuru Mhe. Waziri kwa jitihada anavyoshirikiana yeye na Naibu Waziri wake na wizara nzima ya Wizara hii ya Habari, Utalii na Michezo, ili kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba. *(Makofi)*

Lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri huyu kwa kitu kimoja kipekee alichokuwa nacho sifa kwamba anashirikiana sana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hasa *backbanchers* utakapokwenda kwenye mkahawa anakunywa sisi na chai pamoja, tunapotoka nje anakuja kukaa na sisi pamoja anapokea ushauri ni mahusiano mazuri kabisa anaonesha kwamba hajitengi na sisi na Mhe. Rais wa Zanzibar hajakosea. *(Makofi)*

Baada ya hapo niseme naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Said, kwa mchango wako mzuri kabisa. Mhe. Simai Mohammed Said umenitaja umesema enzi za zamani nilikuwa naenda Chwaka sio Chwaka tu karibu Unguja nzima mpaka kisiwani tulikuwa tunakwenda na shahidi wangu Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaye Mhe. Haroun Ali Suleiman, maana sehemu nyengine tulikuwa tunaenda pamoja. *(Makofi)*

Kwa kweli, Mhe. Mjumbe kuna suala moja ambalo naona umeligusia sana ni suala zima la wanawake kupata sehemu ya kuogelea na nakuunga mkono sana kwa hilo. Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu tumekuwa na changamoto kubwa mimi sasa hivi nafanya mazoezi, na ningewaomba wanawake wengi kufanya mazoezi pwani kwenda kuogelea, lakini tunapata shida tunaogelea na mitandio yetu na mabuibui yetu kwa sababu hatuna eneo maalum la kukogea wanawake.

Sasa nakupongeza sana Mhe. Mjumbe kwa sababu hilo suala ni kweli liko hai na wanawake wengi wanashindwa kutumia *beach* zetu ambazo Mwenyezi Mungu katujaalia tumezaliwa katika maeneo mazuri na wajibu wetu kuzitumia. Kwa hiyo, ningekuomba sana Mhe. Waziri, hili ulisimamie ili angalau wanawake wakienda katika baadhi ya maeneo kwa ajili ya kuogelea na kuogelea ni afya kwa sababu ni mazoezi moja katika mazoezi mazuri sana. Hivyo tungekuomba Mhe. Waziri namuunga mkono sana Mhe. Simai Mohammed Said. tunaendelea. *(Makofi)*

Sasa nampisha Mhe. Rashid Makame Shamis.

Mhe. Rashid Makame Shamis: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniruhusu na mimi kuweza kuichangia taarifa hii ya utekelezaji ya hoja za kamati katika Wizara hii ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Awali pamoja na shukrani kwanza nikupongeze kwa msisitizo huu ambao umeumaliza kusema juu ya kuwa na maeneo mazuri ya kuogelea kwa wanawake.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe fursa hii vile vile, na kuwapongeza sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo na Naibu wake Mhe. Chum Kombo Khamis kwa utekelezaji na utendaji lakini vile vile, niwashukuru watendaji wote wa wizara hii kwa ripoti hii ambayo imekuwa ni fupi lakini ni nzuri. Pia nichukuwe fursa kuishukuru Kamati ya Wanawake, Habari na Utalii chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Suleiman Ali, na nimalizie kumshukuru Mhe. Simai Mohammed Said ambaye amenitangulia katika kutoa michango yake juu ya taarifa hii ya Wizara hii Habari, Utalii na Michezo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika kuchangia kwenye ripoti hii ya utekelezaji nije katika sekta ya habari, ukurasa wa tatu. Mhe. Naibu Spika, katika hoja inayohusiana na *AGAPE*, kwanza nishukuwe fursa hii kushukuru uongozi wa wizara hii kwa umakini na hadi kufikia kumaliza mzozo ule kati ya Wizara yake na *AGAPE*. Suala la *AGAPE* ni suala ambalo limeshamiri sana katika bajeti zilizopita lakini tushukuru sana kwamba suala lile sasa limemalizika na niseme tu

shukrani za pekee kwamba sasa tunapata vigamuzi vya *ZMUX* ambavyo tunavitumia majumbani kwa kweli tuwashukuru sana wenzetu kwa juhudi walizozichukua. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vile vile kwa kuweza kufikiria kuwapa motisha wale wafanyakazi ambao walikuwa wanafanya kazi na *AGAPE* kwa kweli suala la kufikiria kuwapa motisha, ni suala zuri sana, kwa sababu wametumika na kutokana na mizozo ya kimikataba pengine wamekosa haki ambazo walikuwa wanastahiki kuzipata, kwa hiyo wizara kuweza kufikiria suala la kuwapa motisha naliunga mkono na ni suala zuri sana. Sana Mhe. Naibu Spika, nafikiri suala hili la *AGAPE* liwe ni darasa tosha na ile mikataba yetu mengine ambayo unaingia na kampuni mbali mbali, ili kuepusha mizozo na migongano ambayo wakati mwengine sio ya ulazima.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nielekee sasa katika ukurasa wa tano katika suala zima la mafundi ambalo hoja ilikuwa ni *ZBC* Pemba, lakini imehusisha vile vile suala zima la mafunzo na mafundi, Jawabu ambayo imetolewa na wizara ilikuwa pia imetaja juu ya utaratibu mzima wa kuwapeleka kwenye mafunzo waandishi na tunatarajia kuajiri mafundi wa *TV* hivi karibuni.

Mhe. Naibu Spika, kuna wafanyakazi ambao wanamaliza muda wao na wengine wameshamaliza ambao wengine ni mafundi mahiri, ambao tuliowatarajia au tuliowategemea sasa ni suala zuri. Jawabu zuri ambalo tumeliona hapa lakini hoja yangu tu, ni mafundi wangapi ambao tunatarajia kuwaajiri, kutokana na pengo ambalo lipo lakini ni mchakato. Mchakatu unaendeleaje wa uajiri hivi sasa tuko katika hatua gani ili kuweza kuhakikisha kwamba, pengo hili la mafundi hususan katika upande wa TV linazibwa, ili kuepusha usumbufu pengine hata wakuwataka wale ambao wamemaliza muda wao pengine kuwaanzima mara kwa mara kuja katika vyombo vyetu kutusaidia utaalamu. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri atakapokuja basi atwambie tu, kwamba ni mafundi wangapi wanatarajia kuwaajiri kwa Unguja na Pemba na ni lini mchakato unaendeleaje.

Mhe. Naibu Spika, sasa nende katika ukurasa wa saba kwenye hoja namba 4 na hoja namba 5 nitazichanganya kabisa ambayo ipo kwenye ukurasa wa nane, juu ya suala zima la sehemu hizi za historia kubwa zaidi ambalo limetajwa katika hoja hapa, ilikuwa ni suala zima la ukusanyaji wa mapato. Niseme tu, kwamba katika hoja hii nimpongeze sana Mhe. Simai Mohammed Said kwa kuweza kutoa rai ile ya kwenda katika utaratibu wa kukusanya mapato kwa njia ya *electronic*, kwa sababu hivi sana unapozungumza suala la kusambaza vitabu vya risiti, nchi hii imepigwa sana na suala vitabu vya risiti, hivi sasa tunazungumzia ukusanyaji wa mapato kwa njia ya *electroric*. Kwa hivyo, sisi kama serikali hivi sasa nafikiri tuanze kuachana na utaratibu huo. Hivyo nimuombe sana rafiki yangu kwamba suala la risiti za mkono hizi kwa kweli tutaendelea kupigwa kwa hiyo tuangalie utaratibu ambao wa ki-*electronic* ambao utakusanya mapato katika sehemu hizi za historia.

Lakini nishauri tu kwamba sehemu hizi zenye makumbusho au vivutio vya kihistoria ni sehemu ambazo nyengine kwa kweli majengo yake yamechakaa mno na mengine yamekwisha anguka. Kwa hiyo, tujitahidi sana katika kufanya ukarabati ambao hauwezi kuondosha ile asili ya maeneo haya. Vile vile, nishauri kwamba kwa zile sehemu za kihistoria ambazo zinatembelewa sana na wageni ni vyema kujenga ofisi jambo ndogo pamoja na vyoo viwili cha wanawake na wanaume inaonekana maeneo mengi hayana hata kiofisi ambacho pengine muhudumu wetu anaweza kukaa pale na kuweza kuratibu mambo mengine.

Lakini hapana vyoo baadhi ya sehemu ambayo inawafanya wanaotembelea kuwa na wakati mgumu pale wanapokuwa na haja. Kwa kweli, tumejifunza mengi tulipotembea kwa mfano Arusha tulitembelea Hifadhi ile ya Arusha ile hifadhi kubwa sana karibu nusu na robo ya kisiwa cha Unguja, lakini huruhusiwi kufanya haja yoyote katika msitu ule na lazima ufanye katika sehemu maalum. Sasa seuze katika sehemu zetu hizi za historia tujitahidi sana ziwe na vyoo ziwe na kiofisi kidogo ambacho kitakuwa kinaratibu shughuli zile. Ofisi hii wakati mwengine inasaidia kwa sababu Mhe. Waziri amesema kwamba tutakuwa na daftari la mahudhurio sasa kama huna kiofisi katika hayo maeneo daftari hilo sijui kama litakaa wapi.

Mhe. Naibu Spika, tunapata malalamiko juu ya hivi vyanzo au hizi sehemu za historia kutokuwa na maandiko. Kwa hivyo nashauri sana hizi sehemu zenye vyanzo vya kihistoria kumbukumbu basi ziwe na maandiko, jana nilimsikia *Professor* mmoja ambaye alikuja katika Tamasha na Uzinduzi wa Kamishieni ya Kiswahili alitembelea kwa Bi Khole pale alikuwa anahojiwa moja kati ya kasoro ambayo ametoa kwamba hakuna maandiko yanayomuhusu Bi Khole. Sasa ni vyema katika vile vyanzo muwe na maandiko mule na hata yale maandiko yatakuwa yanasaidia katika kukusanya kipato. Kwa mfano, hata kama ni *brochure* au vitabu ambavyo vinaelezea historia ya pale pahala vile vile itakuwa ni chanzo cha kuweza kukusanya mapato. Hivyo, nihimize sana utaratibu huo utumike, ili kuweza kuona kwamba sekta hii inatukusanyia mapato zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee katika ukurasa wa 9 nizungumzie au nichangie na mimi kwenyue Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar BTMZ.

Mhe. Naibu Spika, hapa ilizungumziwa suala la kuviwezesha vilabu na wenzetu wametoa majibu mazuri, kwamba katika mwaka 2016/2017 walitenga shilingi milioni 76.7 katika kuviwezesha vyama au vilabu mbali mbali vya michezo. Mhe. Naibu Spika, katika eneo hili napatwa na wasiwasi kidogo bajeti kwa kweli ya Baraza la Michezo bado ni ndogo sana. Kutokana na hali hiyo, niombe sana serikali kuweza kuongeza bajeti katika Baraza hili la Michezo la Taifa la Zanzibar. *(Makofi)*

Tukiangalia bajeti ya mwaka ambao ameutaja Mhe. Waziri ilitengwa shilingi 84,000,000/= katika kitabu chake cha bajeti cha mwaka huu ukurasa wa 79 lakini katika kitabu hicho hicho ukurasa wa 97 kwa mwaka huu bajeti ya Baraza la Michezi katika kuendeleza na kukuza michezo ni shilingi 70,000,000/=. Kwa kweli, hizi pesa Mhe. Naibu Spika ni kidogo sana katika suala zima la kuendeleza la kukuza michezo.

Zanzibar ina vyama vyingi vya michezo kama sikosei vinafika vyama 13 vya michezo au kuzidi sasa kuwa na shilingi 70,000,000/= kuitenga kwa ajili ya kuendeleza na kutunza michezo labda iwe inachangiwa na vifungu vyengine vya idara inayohusika, lakini hizi fedha ni kidogo. Hivyo, tuiombe serikali kama tunaka udhati kweli kweli kuendeleza michezo basi bajeti hii kwa Baraza ni ndogo sana. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu lengo sio kuvisaidia vilabu pale vinavyoenda mashindanoni tu, isipokuwa lengo ni kuanza kuwakuza na kuwaendeleza kabla hawajenda mashindanoni, na ndio maana mara nyingi sana tunaenda kushiriki na sio kushindana. Kwa hiyo, matokeo yake tunapatwa na aibu, tuanze kuifikiria kuweza kuendeleza michezo tokea kwenye mazoezi na miundombinu.

Mhe. Naibu Spika, umezungua suala la kuogelea Zanzibar kama nchi haina bwawa lake la kuogolea, sasa hii haileti picha nzuri katika kuendeleza michezo, wakati kwa nchi nyengine ile skuli tu ya *nursery* ya maandalizi basi ndani mule munakuwa na bwawa la kuogolea. Hivyo, naiomba sana serikali kuweza kuhakikisha kunakuwa na miundo mbinu ya kuweza kuhakikisha tunaendeleza michezo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika vyama ambavyo tunavyo hivi sasa vyengine vinasuasua na vyengine vishakufa Zanzibar ilikuwa katika nchi za Afrika ya Mashariki, basi ilikuwa namba moja katika michezo ya *badminton* nakumbuka Zanzibr ilikuwa namba mbili katika michezo ya *table tennis* michezo, hiyo sasa hivi iko wapo watu wanategemea Haile Selassie na Ben-Bella yale ni maholi ya skuli.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri alichukuwe sana hili kuweza kutafuta wafadhili popote kuweza kuona Zanzibar inakuwa na miundombinu mizuri, ili kuifufua ile michezo ambayo ilikuwa inaipa hadhi nchi hii, tusiangalie *football* tu na hata hiyo *football* hatufanyi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mwezi uliopita nilikuwa mgeni rasmi katika kufunga Mashindano ya Ridhaa pale Amani inasikitisha Mhe. Waziri na nilikuwaga kama nakwenda vifaa tunavyotumia kwa michezo vya michezo nafikiri toka uwanja ule uundwe hatuwezi kuwa na viwango vizuri vya michezo kwa vifaa ambavyo ni vya miaka ishirini.

Mhe. Naibu Spika, nimeukuta mkuki tayari ushaungwa kwa fundi, yaani ulikatika ukapelekwa kuungwa huwezi mkuki ule ukatujenga kiwango ambacho tunakitaka, mikuki ina kipimo vyake mikuki kwa mfano ya wanawake ni *grams* 600 lakini ukiuchukua mkuki wa pale Amani tayari ushapungua uzito ukichukuwa wa wanaume nimeangalia jiwe lile la kurusha *shot put* tayari lina viraka.

Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri aniruhusu na tayari Chama kile cha Riadha nimekiahidi kuweze kununulia vifaa vya michezo vya kurushia ikiwa *javelin, shot put* na *dustcut* na tayari nishazungumza na kampuni inayoagiza vifaa hivi kutoka nje. Kwa hivyo, naomba sana tushirikiane ili tuweze kuona kwamba vyama vyetu hivi vya michezo tunavikuza, kwa sababu riadha inawachezaji wazuri sana kutoa KMKM, Magereza, Uhamiaji, lakini vinahitaji msisitizo mkubwa sana. Kwa kweli, ridhaa ilitupa heshima kubwa sana na mchezaji mmoja tu wa riadha analeta sifa katika taifa, juzi juzi tu kuna Simbu huyu ambaye alishiriki mashindano India Mumbai, alishiriki mashindao Uingereza ni mtu huyu mmoja lakini kaweza kuijengea taifa la Tanzania sifa.

Kwa hiyo, tuangalie na hii michezo midogo midogo kama ile mengine hatufanyi vizuri basi tuna uwezo wa kufanya vizuri katika michezo mengine midogo midogo. Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri tushirikiane katika hili kuweza kuona kwamba hivi vyama vya michezo vinatengewa pesa vinatengewa pesa, vinasaidiwa ili kuweza kuona vinafanya vizuri katika mashindano mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, tuna vyama vingi *basketball* juzi nilienda pale wanafanya vizuri tu, lakini sasa hakuna ligi au ikiandaliwa ligi utasikia vilabu vya Pemba haviwezi kuja kwa sababu havina

nauli sasa huwezi ukajenga vya michezo kwa mashindani ya upande mmoja tu katika visiwa hivi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo mimi nikushuruku sana kwa kunipa nafasi hii lakini vile vile niishukuru sana Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa juhudi zao, Mhe. Simai alisema kwamba hoja zao ni kidogo lakini hoja kidogo inaashiria kwamba kuna utendaji mzuri kwa mimi niavyoona kwa sababu najua kamati imefanya vizuri na haikupendea lakini hoja zikiwa kidogo maana yake zile changamoto nyingi katika wizara hazipo.

Kwa hiyo, niwapongeze sana wenzetu na waendelee na juhudi hizo na mimi nasema tu kwamba naiunga mkono hoja kwa asilima mia ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Nadir Abdul-latif na ajitayarishe Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bissimillahi Rahman Rahim* naomba nimshukuru Mwenyei Mungu sana kwa kunijaa uzima na nawapa salamu zangu za dhati wananchi wangu wa Jimbo la Chaani ambao wengi hatujaonana muda mrefu.

Lakini namshukuru kwa kunipatia nafasi Mhe. Naibu Spika kabla sijaanza kuchangia Ripoti hii ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo nitaomba kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa hekima zake, utekelezaji wa ahadi zake kwa kweli kabisa pamoja na imani yake na heshima yake kwa watu wote wadogo na wakubwa ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Nimezungumza haya kwa sababu kwanza nipoingeze kwa utekelezaji wake katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika Jimbo langu kuna vitu takribani vitano ambavyo vinaendelea kuimarika ndani ya mwaka huu au ndani ya awamu yake ambavyo vikubwa sana kwa wananchi wangu wa Jimbo la Chaani. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa Chaani wa Maji, Soko la Kinyasini, Hospitali Kikobweni pamoja na kufungua Msikiti Mtukufu hivi karibuni ndani ya Wadi ya Bandamaji kaja kufungua nampongeza sana kwa kushiriki kwenye vitu vitukufu kama hivi na yeye mwenyewe na wananchi wa Jumbo la Chaani wamerafurahi sana kwa ujio wake. *(Makofi)*

Kwa kweli, nampongeza sana pale ambapo alipoweza kunitaja mimi Mwakilishi wa Jimbo la Chaani kunitambua kuwepo, lakini nasikitika sana kwa wale wote ambao hawajaweza kunitambua na kutonipa taarifa kwamba Mhe. Rais anaenda kufungu Msikiti Bandamaji na Uongozi mzima sijapewa taarifa lakini nilihudhuria heshima ile kwa sababu ya Mhe. Rais wa Zanzibar ukubwa wangu bosi wangu katika chama nimeenda lakini pia kwa niaba ya Mwenyezi Mungu kitu kitukufu ndicho kilichonifanya nihudhurie la sio hivyo nisingeenda. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Rais kwa heshima zake na wale wote ambao walivyunja kanuni na pia kunitoa jina langu kwenue taarifa ya kutoa neno la shukrani la Jimba la Chaani mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, basi nawapa pole sana lakini Mhe. Rais alinitambua na akanipa heshima yangu nampongeza sana. *(Makofi)*

Na ndio maana namsifu mara nyingi sijawahi kumsema kwasababu huyu mzee kakamilika kwa mujibu wa ubinadamu yuko vizuri sana na Mwenyezi Mungu amjaalie afya aendelee na nikiwa Rais miye kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atakuwa mshauri wangu wa mwanzo. *(Makofi)*

Mwenyezi Mungu akija kunijaalia Rais wa nchi hii mshaauri wa mwanzo atakuwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwangu mimi nitamuomba kwa sababu wazee ni washauri wazuri akiwemo baba yangu mzazi na wengineo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi mchangio wangu mdogo tu ndio maana nikaanza na kumsifu Rais wangu kwanza nipongeze wizara hii kwa ujumla lakini Mhe. Waziri niliwahi kukueleza viwanja vyangu wa Jimbo la Chaani nililipia taa za uwanja mpira wa kuchezea usiku, lengo lake kuimarisha mambo ya michezo na hasa siku za sikukuu wataweza kutumia wananchi Jimbo la Chaani na Kaskazini kufanya siku za sikukuu kwa mataa yake kutumia kufanya sherehe za vizuri ningeomba sana. Mhe. Naibu Spika, yale mambo nilokuomba kuleta nguzo za umeme mambo yote nitafanya mimi mwenyewe naomba sana utekeleze kwenye viwanja hivi kwasababu umeme wa shamba ni mdogo mataa yale hayawezi kuwaka na viwanja vitatu nishaweka kila kitu. Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mhe. Waziri tukatembee apate aangalie vipi vya kusaidia kwa upande wa michezo ili kufurahisha vijana.

Lakini ningendelea kwa mengine ambayo maswali ya utalii. Kwa kweli, nimejaribu kulisoma ripoti hii kuisoma vizuri lakini nimeandika mwenyewe ki-*memo* changu ambacho nitazungumza kwa jumla, ili tuimarishe utalii na uwe mzuri Zanzibar na uvutiwe, basi kitu cha mwanzo tuangalie kitu gani kinawakwaza wageni, vitu vingi vinawakwaza wageni.

Mhe. Naibu Spika, kwanza tuondoshe usumbufu kwa wale wote mapapasi au watu ambao katika maeneo ya utalii wanakerwa hasa Forodhani na *beach boys* ambao wako mabaharini kutwa wawauliza wageni madawa ya kulevya watawasumbua wamelala watawaendea. Kwa hivyo, naomba sana uwekwe ulinzi maeneo ya baharini polisi kuzunguka, watakapoona wanawasumbua wageni basi wawezi kuwazuiya na kuwahoji, ikiwezekana wapewe vibali maalum *beach boys* ambao wataweza kuongea na wageni. *(Makofi)*

Hili jambo linasumbua sana utalii na tukumbuke kwamba watalii wanakuja hapa Zanzibar si kwa ajili kwamba wamekuja kwa ajili ya jina wamekuja kupumzika, walokuja kwa ajili ya wameoa wamekuja *honeymoon*, walokuja kupumzika na tafrani zao wamechoka wana makazi yao wamekuja kupumzika. Kutokana na hali hiyo, naomba suala la ulinzi liimarishwe katika mahoteli, baharinina sehemu nyenginezo *especially* Forodhani, kuna mpaka wendawazimu Forodhani wanakuwepo usiku wanakera wageni hawana akili kabisa, wageni wanakula wanawaendea, watu ambao hawana akili wanakuwepo maeneo ya Forodhani ambayo ni kitovu cha utalii ndani ya nchi hii.

Lakini jengine nashauri vile vile hoteli ambazo tunazipa *grade* lablda *five star hotel, four star hotel*. Kwa hiyo, napenda kujua vigezo gani ambavyo wanavitumia kuipa hoteli nyota na hawa ambao wanatoa vigezo vile kama vile hoteli yako nyota tano, wamefata kiwango kipi na wamesomea labda wapi. Kwa mfano, *five star hotel* ya Unguja ambayo ni *five star* kwa nchi nyengine inakuwa *standard* ya *three star*. Sasa napenda kujua vigezo vyetu sisi vinakuwa zaidi vipi mpaka mtu vinampa nyota au mtu kwamba ana pesa yake ya kununua leseni ya *three star*

hotel anakwenda kununua hata kama hoteli yake *guest house*, tungeweka *condition* maalum, ili tukaweza kuziweka hoteli kwa mujibu wa *standard* inayotakikana kimataifa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, napenda kulizungumzia suala la ajira Mhe. Waziri. Kwa kweli, mahotelini Wazanzibari ajira zao ndogo wazalendo Wazanzibari wazaliwa wa Unguja na Pemba. Hivyo, naomba ikasimamia ipasavyo wizara yake na wizara zote husika zinayohusiana na mambo ya kazi asilimia 80% ni lazima kama kufa kwa Wazanzibar wapewe ajira asilimia 20% ndio wapewe watu wengine ndani ya nchi hii, kwasababu tukiangalia matokeo yake ni kinyume. *(Makofi)*

Kwa kweli, ziko hoteli nazipongeza zina wafanyakazi asilimia 90% Wazanzibari, lakini asilimia 90% za mahoteli ya Zanzibar wafanyakazi si Wazanzibari. Mhe. Naibu Spika, naomba vizuri zaidi akae na wizara zote husika Wanzanzibari wapewe kazi asilimia 80% na 20% uzibakishe kwa wengineo, na nitakuja na taarifa maalum ambao naifanyia *research* ya kuja kukwambia wafanyakazi wangapi Wazanzibari hawana kazi na wangapi ambao wana kazi sio Wazanzibar katika nchi yetu.

Lakini ningependa kujua kwenye *database* zenu ambazo zimeangaliwa humu ndani muweze katika masuala ya hoteli. Mhe. Naibu Spika, napenda kujua hadi hivi sasa Zanzibar tuelezwe kwamba kuna hoteli ngapi za *five star, four star* na *three star*, ili tukapata kujua Zanzibar tuko vipi kwenye masuala ya *database* na hoteli ngapi tunazo ndani ya *database* zenu ambao humu ndani hazijaorozeshwa.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumshauri Mhe. Waziri, kuwepo kwa *Information Desk* katika sehemu zote muhimu za nchi hii, ili wageni wanapata tabu sehemu ambazo wanataka kwenda wanapotea hawajui kwa kuuliza wapi, matokeo yake wanavamia watu waliokuwa sio. Hivyo ni vyema tungeweka maeneo ya *Information Desk free of charge* ambayo na yawepo sehemu kama vile Forodhani, *Airport*, Shangani, Malindi, Nungwi pale karibu na Kituo cha Polisi, Paje karibu njia pamba, Makunduchi na sehemu nyenginezo liwepo *Information Desk* ambayo wageni wataweza kusimamisha gari yao pindipo wamekwama hawajuii wanakwenda wapi wakauliza pale wakapata *information*.

Vile vile ushauri mwengine kwamba kwenye suala la utalii vikawekwa vikundi vya utamaduni *Airport* na Bandarini, ambapo vitakuwa umeviajiri *permanent* vipo pale kwa ajili kufurahisha wageni wanapowasili hasa madege makubwa, waocheza, wanaofanya sarakasi, wanaoimba nyimbo za kiasili, waajiriwe vikundi vimekaa havina kazi, wananchi wanapata tabu ajira vikundi kama vitano vitano kila siku vibadilike ndege zinakuja nyingi, wananchi bandarini na *airport* wale Wazungu wageni wapatwe kufurahishwa kidogo hata kama kachoka kidogo atahisi afadhali. *(Makofi)*

Kwa kweli, Mhe. Naibu Spika kuhusu suala la utalii kwenye kujitangaza Mhe. Waziri kweli tuko vizuri Zanzibar, lakini kuna nchi nyingi lakini bado nchi ya Zanzibar haijulikani ikiwemo wageni kutoka *Kuwait*, *Qatar* na wengineo wanakwenda sana *Londan* na sehemu nyenginezo. Mhe,. Naibu Spika, tungeomba kwenye *Middle East* tukaendelea kufanya utangazaji au tukashiriki maonesha ambayo tunashiriki kila siku tukajitangaza vizuri zaidi *Middle East* na *America* nchi kama za *Brazil* huko na nyenginezo bado Zanzibar haijulikani sana. Naamini inawezekana

jidihada zimeshafanyika, lakini tuendeleze *Russia* na nchi nyenginezo ambao zina fedha raia wake wana fedha kuja kutumia, ili tuweze kutangaza nchi zaidi. Mhe. Naibu Spika, katika hili naomba tushirikiane zaidi na serikali husika tukapata bei nafuu kutangaza katika vyombo vyao vya TV zao ambazo wanazotumia nchi hizo.

Kuhusu suala la vitege uchumi vya utalii Zanzibar, tukiangalia makubusho mengi yako katika hali mbaya. Tungeomba ili utalii wako uwe mzuri kwa sababu wewe ni waziri basi hizi sehemu zote ambazo zinahusiana na sehemu za historia na mambo ya utalii ziwe katika *condition* nzuri uzitengeneze ziwe katika hali iliyokuwa inaonekana.

Mhe. Naibu Spika, nimetaka kuzungumzia suala la Idara ya Habari. Mhe. Waziri ningemshauri au ningependa kujua hadi hivi sasa wanahabari ambao sio viongozi wa juu hawa wa chini ambao wanaochukua video nje humu ndani wamewapeleka nje ya nchi kwenda kusoma au kuona wenzao wanafanya kazi vipi, ili na wao waweze kuiga lakini isitoshe ili Zanzibar iwe na habari nzuri basi mitambo yao iwe mizuri, vitendea kazi viwe vizuri, maslahi yao yawe vizuri na vitu vyenginevyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nawaombea zaidi kwamba tuweze kuwafikiria kwasababu waandishi wa habari dunia wote wana mshahara mkubwa posho zao kubwa. Je, kwa upande wa Zanzibar ambao tunasema mambo yao yako mazuri yako vipi, vile vile ningependa kujua na hawa elimu yao wamepatiwa vipi hapa hapa au vipi. Hivyo, naomba wakapelekwa na wao wakasoma nje, wakajionea, wakakaa angalu wiki moja mbili wakaona mazingira ya watu wanatumia vipi na wao wakawa kidogo *more advance* la si hivyo tutawalaumu kila siku wakati vifaa vyetu pengine haviko sawa.

Lakini pia niwapongeze kwa sababu mambo yao naona kidogo yamebadilika sasa hivi kwenye TV yako vizuri, na hasa kuna siku niliona *live* kuna tukio lilitokea Amani likarushwa *live* kabisa lile nilipenda sana naomba utaratibu huo uendelezwe kuwepo na mitambo *standby* inapotokezea kitu *live* tuweze kushiriki kama anavyoshiriki *Azam TV*.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo nilotaka kulizungumza lilikuwa la michezo, Mhe. Waziri suala la michezo nafikiri nimeshakukumbusha. Lakini vile vile wana michezo wa mipira Zanzibar wabeba vyuma, waogeleaji, wanaopigana pamoja na *volleyball* ningependa na hawa mngewatafuta *market* ya nje wakashiriki *league* ambazo za nje mkawapeleka kidogo wakacheza mipira nje wakapata na wao kidogo mabadiliko ya mambo ya mipira, mambo ya *volleyball* na vyenginevyo kuliko kuwapeleka hapa hapa tu Unguja na Tanzania Bar. Nadhani ni vyema wakapelekwa angalau kidogo Msumbiji, Mombasa Kenya na sehemu nyenginezo waweze kushiriki angalau Zanzibar ipate kidogo umaarufu kwa upande wa michezo, kuliko masuala ya utalii peke yake tutafute na michezo vile vile.

Mhe. Naibu Spika, ningepongeza sana kwa kuona kwamba kuna watu wamefungiwa biashara zao sehemu ya Kiwengwa ambao wamesababisha mgogoro na wananchi. Hili ni jambo zuri sana kuwafungia, lakini si kuwafungia tu muwachukulie hatua nyenginezo za kuwapandisha Mahakamani, ili watu kama hawa wakome kuwasumbua wananchi ambao wakimya na wazalendo.

Mhe. Naibu Spika, suala la utalii vile vile kwenye kutatua matatizo ya watalii ambao wanalalamika sana ni njia Mhe. Waziri. Tunaomba akae na Wizara ya Mawasiliano ili njia zote ambazo zinaingia kwenye mahoteli ya Zanzibar ziwe njia zenye lami au kifusi ambacho hakichimbuki mara kwa mara. Kwa mfano, leo ukitaka kwenda Nungwi basi kama huna gari *Four-Wheel Drive*, gari yako ukaiache Kituo cha Polisi kwa sababu haiingii kule ndani utaivua *bumpers* zote uzivunje. Kwa hivyo, tungeomba sana kwamba barabara zote zinazoingia kwenye mahoteli ikiwa *Five Stars*, ikiwa hoteli ndogo basi barabara ziwe nzuri kwa sababu mgeni ameshatoka masafa marefu matokeo yake tunamtia kwenye mashimo kama mgonjwa wa migongo anapanguka huko huko kwenye gari. Tungeomba sana hizi njia Mhe. Waziri azitekeleze na aziendeleze vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, suala la utalii ni kubwa kusema la ukweli na Zanzibar ndio tunaloringia. Hivyo, tungeomba sana Mhe. Waziri awe makini sana kwa yale mambo yote afanye mwenyewe na watendaji wake, mchakato mzima wa kuangalia kitu gani kinasumbua Zanzibar kwenye masuala ya utalii na kitu gani ambacho kiko vizuri, ili aweze kujirekebisha mambo yaende vizuri.

Sambamba na hilo, naomba kushauri kwa wageni wote ambao wanaoingia Zanzibar wangeweka vile vibuku vidogo ambavyo vina *full information about Zanzibar* ambavyo vitaeleza hoteli za Zanzibar ziko ngapi, nzuri labda sehemu ya *restaurant* nzuri Zanzibar atapata wapi ya Chinese, Indian au Italian *Restaurant*, itaeleza makumbusho yako sehemu gani na bei gani na tuweke pia na *interest fee* ambayo wataweza kuona ni shilingi ngapi, mtu atakwambia kuna *dolphins*, kuna *Jozani Forest*, kuna masuala mengineyo ambayo yote ambayo anayajua Mhe. Waziri yanayohusu kwa upande wa utalii. Vitabu hivi naomba vitowe bure kwa sababu ukifanyisha kwa wingi ikiwa nje ya nchi au ikiwa hapa havi-*cost* ghali lakini vitaweza kumsaidia mgeni kwa njia rahisi ikiwemo na *Map of Zanzibar* ambayo itaonesha Mji Mkongwe na Zanzibar nzima itaweza kumuendesha bila ya kupata tabu, kwa sababu kuna wageni wao wanaweza wakatembea nchi kwa ajili ya map tu sio lazima kuuliza kutumia *navigation system*.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo sitaki kuchangia sana kama nilivyosema mwanzo niliinuka zaidi kumpongeza Rais wangu na hasa kwenye maendeleo ambayo ya miaka yake hii kumi inayokwenda, vitu vikubwa ambavyo vimefanyika tunaviona hasa miradi mikubwa ya utalii inayofanyika *Five Stars* hoteli makubwa makubwa yaliyojengwa ndani ya uongozi wake, hii peke yake inaonesha kwamba anafanya kazi kubwa kwenye suala la utalii, kwenye suala la habari na suala la michezo. Mhe. Waziri nitaomba ukija uniahidi lini tutakwenda Jimbo la Chaani kunitilia nguzo zangu ili mambo yaende vizuri.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, ripoti hii naikubali kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Abdalla Ali Kombo.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa ruhusa yako na mimi niwe mmoja katika kuchangia ripoti ya wizara hii. Kwanza namshukuru Mhe. Waziri wa wizara, Naibu Waziri kwa ripoti fupi lakini kwa kufikiria haina mashaka. Na pia namshukuru Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe wake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa na kidogo sana ya kuchangia katika wizara hii. La kwanza kwenye mafunzo mimi ningeomba tu hawa waandishi wa habari, hasa hawa wa Mawio ambao kila siku asubuhi tuko nao waweze ama wabuni hizi taarifa ambazo wanatupa basi kuwe na *feedback,* yaani watupe na nini kimefanyika baada ya mtu kukamatwa au baada ya tukio. Wanatupa mengi hasa kuhusiana na madawa ya kulevya, wabakaji na kadhalika, lakini baadae hatujuulishwi sasa wale watu waliokamatwa nini kimetokea wananchi ndio tunaobakia kwamba ah! Ah! Hakuna chochote. Lakini wangetujuilisha wale waliokamatwa wangapi wamefungwa, wangapi wameachiwa huru, jambo muhimu tupewe *information* baada ya kisa nini kimefanyika kwa serikali. Hilo moja.

Mhe. Naibu Spika, la pili kwenye *page* ya 6 na 7 kuwe na *database* ya wizara. Nawashukuru kwamba wameweza kuanzisha kitu hiki lakini pia msisitizo wangu tena wizara peke yake haitoshi kuwa na *database* yake. Nawashukuru *ZIPA* pamoja na Baraza la Wawakilishi wametusaidia kwenda kutizama Kituo cha wekezaji Dar es Salaam hapa *One Stop Center* ipo, ingawaje idara ama wizara za Zanzibar zinasema hiki kitu ni kigumu, lakini wenzetu Bara wameweza kufanya na wamefanikiwa.

Wenzangu ambao tumekwenda wote ni mashahidi *One Stop Center* ipo kuna watu wa Uhamiaji na watu wa taasisi nyengine zote. Kwa hivyo, naomba tena ili tuwe na utalii ambao unafahamika wenye takwimu, wenye kila kitu ambacho kinatakiwa tuwe na *One Stop Center* kuliko kuwa na *database* za Wizara ya Habari, na Utalii lakiniUhamiaji wana zao na *ZRB* wana zao. Nasisitiza pia serikali ifanye hiki kitu ambacho kinawezekana na kizuri kwa mambo yetu ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, utalii kwa wote ambayo iko kwenye *page* 5. Naiomba sana wizara wakashirikiana na watu binafsi wakahimiza usafi wa maeneo ambayo watalii wetu wanatembelea. Kwa mfano, ukienda Kizimbani kuna vijichuguu vya vibanda na chanja chanja za ajabu ajabu hasa siku za mvua inakuwa kero na mashaka makubwa. Vibanda hivi vichafu havina mpango ni vyetu lakini lazima tuseme ukweli, watalii wanakwenda. Hivyo, naomba wakae na watu binafsi kwa sababu sasa hivi utalii kwa wote wapange na kuzungumza mazingira angalau yawe ya maana na yawe safi.

Kwa mfano, leo utakwenda kwenye chanja kuna embe, kuna mafenesi, sisi tunayajua kama mafenesi yanakatwa wanapewa ni mazingira ambayo kwa kweli hayafai. Mhe. Naibu Spika, naomba tu wizara kupitia kamisheni zenu ama idara zenu, basi na ninaomba Mhe. Waziri asisukume watu aende mwenyewe kama sehemu nyengine alikwenda kuona hali halisi tuka-*improve* yale maeneo.

Lakini pia naiomba wizara hii kukaa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuya-*identify* maeneo ambayo ni ya *spice*. Ukweli wa mambo Zanzibar inaitwa *Spice Island* lakini hatuna maeneo ya hizo *spice*. Tunajinata na kujipiga vifua tu lakini ukimuliza hasa Waziri wa Kilimo au nikikuuliza yeye Waziri wa Biashara haya maeneo yako wapi. Tutasukuma tu Kizimbani, Kizimbani. Sasa ningependa wizara tatu hizi mkakaa pamoja tukatafuta eneo pamoja na watu binafsi ikawa hii ni *special* ya viungo. Ni sawa sawa kwa mfano Forodhani Mzungu yeyote au mtu mweusi yeyote nje ya nchi

yetu anaizungumza Forodhani ni sehemu ya kupumzika na ni sehemu ya utalii. Tungekuwa na eneo kama hili kwa Zanzibar yale maeneo ambayo yanafaa ingekuwa vizuri sana.

Kwa kweli, hivi sasa hivi tunajua wageni wanakuja kuna siku za Mwakakogwa wanajua iko Makunduchi, Pomboo wako Kizimkazi, Paje ukienda sasa hivi sijui eti kuna myavuli wanaruka sijui inaitwaje. Kwa hivyo, tayari kuna maeneo watalii wanakuja wanajua kuna nini. Sasa ningependa kukawa na eneo hili kama la *spice* ingawaje serikali haifanyi biashara lakini tukawaachia watu binafsi wakisaidiwa na serikali. Mhe. Waziri sina zaidi nakusifu hongera sana na ahsante sana. Mhe. Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Ali Kombo sasa basi nimpe nafasi Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. Chum Kombo karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kukushuru wewe binafsi kwa uongozi wako mzuri wa vikao vyetu vya Baraza hili tukufu na ukiwa ni mwanamke tunaamini kwamba wanawake tunaweza. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya shukurani hizo sasa naomba niende moja kwa moja katika michango ambayo au maelekezo ambayo wametupa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili. Kwa kweli lengo na madhumuni ni kujenga na pia kushauri serikali kuona kwamba tunawatendea haki wananchi ambao wametutupa kuja kufanya kazi katika Baraza hili tukufu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa kuendelea kutushauri wizara yetu na mimi nakiri kwamba tunapokea maelekezo yao na tunaendelea na kazi vizuri kama Mhe. Rais alivyotuamini na sisi tunaahidi kwamba tutafanya kazi kwa bidii ili na yeye kupata sifa kwa wananchi.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti wa Kamati amechangia katika sehemu ya utalii na kusema kwamba watalii warudi tena. Lakini naomba na mimi nitoe mchango wangu kwamba watalii wapo na sisi tutafanya jitihada zaidi, ili waendelee kurudi tena na kuja kuona vivutio vya nchi yetu na sifa ya ukarimu ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Mhe. Simai Mohammed Said amechangia kupitia maeneo mbali mbali na kutupa ushauri. Lakini haya yote tunayapokea yakiwemo ya wizara kufanya kazi vizuri na kusema kwamba ripoti yetu ni fupi sana ana wasi wasi kidogo ama kamati imepitia juu juu au wizara inafanya kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimthibitishie Mhe. Simai Mohammed Said kwamba kamati haikupitia juu juu, huu ni uthibitisho kwamba Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo tunafanya kazi vizuri kupitia Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo lakini tukishirikiana na watendaji wetu na ndio maana ukaona ripoti yetu iko sahihi na iko vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Simai Mohammed Said amechangia suala la maeneo ya kihistoria pamoja na Mhe. Rashid Makame Shamsi kwamba tutumie risiti za *electronic*. Ushauri huu tunaupokea na sasa hivi serikali ipo mbioni kutafuta risiti hizi za *electronic* na pale zikiwa tayari tu kwa kuwa tunachukua risiti kupitia Serikali Kuu na sekta hii ya kihistoria nayo risiti hizi zitakuwepo na zitatumika kwa ukusanyaji wa mapato, ili mapato ya serikali yasiingie mifukoni kwa watu binafsi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, vile vile Mhe. Simai Mohammed Said kataka suala la kuogelea tushirikiane na wenzetu wa Tawala za Mikoa kupitia KMKM. Hili pia Mhe. Naibu Spika, nataka niseme kwamba hili ni muhimu na hasa ukizingatia sisi wanawake yanapotokea majanga, sisi ndio yanayotukumba zaidi tukiwa na watoto wetu. Tumeshuhudia matukio mbali mbali hata pale zilipozama meli mbili wanawake ndio ambao tumepoteza maisha na watoto.

Hata hivyo, dini yetu pia imetutaka kwamba tujue kuogelea kwa watu ambao wako maeneo ya pwani tufanye mazoezi ya kuogelea. Lakini hili pia tunalichukua na tutashirikiana na wenzetu tuone kwamba pamoja na mazingira ambayo wanawake yanakuwa yametubana kama ulivyosema Mhe. Naibu Spika, kwamba mazingira yetu sisi tunataka maeneo angalau yana stara ili tuweze kufanya hili zoezi. Lakini naahidi kwamba tunalichukua na tutaendelea kulifanyia kazi kama ambavyo wenzetu wametushauri na pia lina umuhimu kwa sisi wanawake.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Simai Mohammed Said kazungumzia bei za wanafunzi wanapokwenda katika maeneo ya kihistoria lakini na wale wageni. Mara nyingi kama atakuwa anafuatilia tunapojibu maswali, suala hili limewahi kuulizwa na huu utofauti upo kati ya wanafunzi na wageni wetu wanapoingia katika maeneo haya, wanafunzi wanakuwa wanalipia shilingi elfu moja. Kwa hivyo, hili namtoa wasi wasi ajue kwamba tunajali uzalendo na pia tunajenga heshima kwa wanafunzi au kwa wananchi wetu kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf katushauri kwamba tuweke vikundi vya utamaduni katika sehemu za kihistoria na Uwanja wa Ndege na Bandarini. Hili ni zuri tu kwani pia na mimi nakubaliana nae kwamba tunapoweka vikundi hivi katika sehemu hizi pia ni sehemu ya kuutangaza utalii wetu wanapokuja wageni wataona zile tamaduni zetu ambazo tunazo kwa kuvutia ngoma zetu za asili, na hili pia tutaendelea kulifanyia kazi ili tuone kwamba utalii wetu tunautangaza zaidi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katupa ushauri juu ya kuwasomesha wafanyakazi nje. Hili nalo pia tutalifanyia kazi na tutaliangalia kwa kina. Lakini ningeomba zaidi na sisi Waheshimiwa Wajumbe tuangalie zile gharama ambazo mfanyakazi kwa mfano tunamtoa kumpelekea China pengine kenda kuchukua *diploma,* lakini *diploma* hii hii hapa Tanzania ipo kwa hiyo na hili nalo pia tuliangalie kwa kina, ili kupunguza zile gharama ambazo pengine mfanyakazi atachukua kutoka hapa na kwenda nje lakini gharama zile tunaweza kuzi-*solve* hapa hapa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Nadir amechangia kuhusu maeneo yetu ya kihistoria. Maeneo yetu ya kihistoria kuwa katika hali mbaya. Hili ni kweli mara nyingi tunakuwa tukilizungumzia kuhusu maeneo yetu ya kihistoria, lakini hata pia Mhe. Rais wa Zanzibari hili alishatuagiza kwamba tulifanyie kazi na pia kuhusu utalii kwa wote, tuimarishe ili wananchi wetu wote wafaidike na sekta hii ya utalii kwa wote.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache nikushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi hii naunga mkono kwa asilimia mia moja taarifa hii. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Sasa ni muda wa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa mara nyengine nataka nitoe shukurani zangu za dhati kwanza kwa kumshukuru *Allah (S.W)* kwa kutuwepesishia mambo yetu haya hususan asubuhi hii ya leo. Lakini vile vile kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wewe mwenyewe Mhe. Naibu Spika, jinsi ulivyopokea michango ya Waheshimiwa Wajumbe wako mahiri na yakakuingia mpaka ikakufikia na wewe kuweza kuchangia kwenye kiti chako. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niwatambue wachangiaji wetu wote waliotuchangia katika uwasilishaji wa ripoti yetu hii. Kwanza nianze na mchangiaji wa kamati, Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), kwa michango yake mizuri aliyoitoa. Lakini pamoja na michango hiyo, vile vile napenda nitambue michango iliyojumuishwa na wajumbe wake kwa ujumla ambao aliwataja majina, nahisi sio vibaya nikaendelea nao kuwataja majina kwa kuwatambua juu ya michango waliyoitoa katika kutekeleza taarifa hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari,na Utalii ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, napenda sana kutambua wachangiaji jumla yao ni tisa (9), waliochangia katika taarifa yetu ni wachangiaji watano ambao wamechangia njia ya moja kwa moja, lakini wachangiaji wanne wamechangia kwa njia ya maandishi.

Wachangiaji waliochangia moja kwa moja ikiwa pamoja na Kamati ni:

1. Mhe. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Simai Mohammed Said
3. Mhe. Rashid Makame Shamsi
4. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
5. Mhe. Abdalla Ali Kombo

Vile vile, Waheshimiwa waliochangia kwa njia ya maandishi ilikuwa ni pamoja na:

1. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
2. Mhe. Hidaya Ali Makame
3. Mhe. Masoud Abrahman Masoud na
4. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)

Nawapongeza sana kwa michango yao waliyoitoa na kwa ujumla wake Mhe. Naibu Spika kama ilivyozungumzwa taarifa hii haikuwa ndefu, lakini imekuwa na wachangiaji wengi sana nawapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kutizama ujumla wa michango iliyotolewa ilikuwa ni michango ya pongezi na nashukuru kwamba wachangiaji wote waliochangia wameiunga mkono ripoti yetu kwa asilimia mia moja. Hakukuwa na hata Mheshimiwa mmoja ambaye amepunguza angalau asilimia moja katika michango yake. Kwa maana hiyo basi, isingekuwa faraja kuwa na mengi ya kuyajibu, lakini nifarajike zaidi kuona kwamba wizara yangu imepokea maoni, mawazo, ushauri kutoka kwa waheshimiwa hawa.

Pamoja na kuyagusa machache ambayo ninaweza kuyasema, lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba, maoni yao, ushauri na michango yao imetupa hamasa kubwa sana Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kuendelea kushirikiana na kamati yetu na kuhakikisha kwamba, haya yaliyojitokeza tunayafanyia kazi kwa lengo la kutimiza malengo yaliyopangwa katika wizara yetu na kuhakikisha kwamba tunawatumikia wananchi na kuwapa ufanisi wanaoutarajia. Lakini vile vile kuweza kuyatimiza maagizo ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Naibu Spika, Mhe Simai Mohammed alikuwa na ushauri mwingi sana, ushauri mzuri, ushauri ambao umeungwa mkono na wachangiaji wengi. Lakini suala la kuwa na *swimming pool* kwa kuogelea sio wanawake tu na sisi wengine tumekuwa na mazoea ya kuogelea katika bahari kuu. Lakini naona wizara sasa hivi itafanya jitihada maalum kuhakikisha kwamba suala hili lililozungumzwa ushauri wake unachukuliwa na uweze kufanyiwa kazi. Ushauri wao tunaupokea kama ulivyowasilishwa.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na suala la wafanyakazi ambalo pia alilizungumza Mhe. Simai Mohammed Sais juu ya Sekta ya Utalii. Napenda kumueleza wazi kwamba, masuala haya ya Sekta ya Utalii na wafanyakazi yameshaelezwa kwa kina nayo kwa sasa ni sera. Sera ipo ya serikali na sehemu ya kuitekeleza sera hii naamini Wizara yetu ya Habari itashirikiana na wizara zote zile kulifanyia kazi suala hili.

Vile vile Mhe. Rashid Makame Shamsi naye alikuwa na ushauri mzuri sana ambao alijaribu kuueleza *page* hadi *page*. Pamoja na maagizo yetu 10 lakini aliweza kuyachangia maagizo manane kwa ufanisi wake kabisa. Namshukuru sana Mheshimiwa kwa ushauri wake na ushauri wake tumeupokea. *(Makofi)*

Ushauri wa kujenga vyoo katika sehemu za watalii vile vile na sehemu zile ambazo za makumbusho na mambo mengine ni ushauri ambao mote tunamotembelea tunaukuta umefanyiwa kazi vizuri, ushauri huu ninamhakikishia wizara imeupokea na itaufanyia kazi kama ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, pia kulikuwa kuna masuala aliyouliza ya mafundi wanaotegemewa kuajiriwa katika *ZBC*. Nataka nimhakikishie kwamba tunatarajia kuajiri mafundi 20, najua ni kinyang'anyiro, wawakilishi mtakaa *standby* kuona kwamba wapiga kura wetu waliotuajiri wanazing'ang'ania hizi nafasi. Nafasi hizi ni kwa wazalendo, mafundi wa kweli ambao wataidumisha vizuri televisheni yetu na Wizara hii ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kupitia sekta ya habari.

Ushauri wa maandiko kama ya Bi Khole alivyoyaeleza na ushauri wa magofu mengine kufanyiwa kazi, ushauri huu ambao pia umetolewa kwa maandishi kujua namna gani ile historia iliyopotea inaweza kurudi tena nao vile vile tumeupokea na tunaufanyia kazi.

Kuhusu bajeti ya Baraza la Taifa la Michezo kuwa ipo kwa kusaidia vyama hivyo vya michezo. Tunakiri hilo, vyama vyetu ni vingi tuna vyama 33 vya michezo ambavyo vimesajiliwa katika Baraza la Taifa la Michezo la Zanzibar. Bajeti tuliyoizungumza hapa ya mwaka 2016/2017 tunakiri kuwa haikuwa ya kukidhi haja kwa vyama vyote. Lakini napenda kumjuilisha tu kwamba wao ni wenzetu wa kuipitisha bajeti ijayo, natumaini tutakuwa tumeona changamoto hizi ambazo zimejitokeza na bajeti ijayo inaweza ikafanyiwa kazi vizuri zaidi.

Pia alishauri kununua vifaa vya michezo, kutizama uhalisia wa Zanzibar na michezo ile ya kizamani iliyopotea kama vile *table tennis na badminton*. Kweli ni michezo muhimu urushaji wa mikuki namna ya kuruka *jump* zile ndefu na fupi, yote hii ilikuwa ni michezo ambayo Zanzibar inailetea sifa ya hali ya juu ni michezo hiyo katika jitihada zetu za kukitengeneza Kiwanda cha *Mao Tse Tung stadium.* Tunatarajia vifaa vipya vingi vitakuwepo matufe, mikuki na vifaa vyenginevyo, uwanja wa table tennis nao pale utakuwepo, *long tennis, short tennis* zote zitakuwa zinachezwa katika viwanja vyetu vipya. *(Makofi)*

Vile vile katika sera ya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 mpaka 2020 ni wazi kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahakikisha kujenga viwanja ndani ya wilaya zake. Kwa hivyo, viwanja vile navyo tutatarajia kushirikiana na wizara husika, ili kutizama miundombinu nayo inakuwa mizuri na vifaa vinapatikana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf leo kwa upeo mkubwa namshukuru sana kwa michango yake ambayo ameitoa, amezungumza sana suala la makumbusho kwenye bajeti ya mwaka huu tena shilingi bilioni moja kuimarisha maeneo ya kihistoria na ya makumbusho kuwa ilikuwa ni ndogo sana. Kweli tunakubali hivyo na azma kubwa ipo katika kuhakikisha kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inazirudisha historia zile na inaweka umahiri katika makumbusho ambayo yanaonekana kupotea.

Alizungumza sana juu ya suala la utamaduni. Kwa mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya viklundi vya danaa kushiriki kwenye jamii nalo pia tumelifanyia kazi hilo na linaweza likafanyiwa kazi vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile ameeleza juu ya kutaka na kuwa na matamanio juu ya vigezo vilivyowekwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vigezo hivyo vipo na sisi Zanzibar tunavifuatilia.

Vile vile zoezi la uwekaji viwango vya mahoteli kuvijua kwamba hoteli hii ni *five star,* hii ni *four star*. Viwango hivyo vyote vipo na mimi nitampatia kwa maandishi tuna hoteli ngapi ambazo ni *five star* ngapi, *four star* na nyenginezo kwa mujibu wa daraja zilizopangwa. Kwa hivyo, na yeye Mhe. Nadir Abdul-latif ushauri wake uliokuwa ni mkubwa pia vile vile tumeupokea kabisa ushauri huo.

Mhe. Naibu Spika, amezungumza pia kuhusu kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Hili ni jambo zuri sana na ni jambo ambalo serikali ina matumaini nalo kabisa kuona kwamba, watalii wetu wanaofika hapa wanaona miundombinu mizuri, wanaziona hoteli zetu zinafikika kwa urahisi na zinaweza kutusaidia katika kuleta watalii wale ambao wanapenda kurejea maeneo wanayotembelea.

Ni kweli hivi sasa tuna idadi ndogo sana ya watalii ambao wanatembelea nchini na kujirejea rejea, lakini kwa kutengeneza miundombinu, kwa kushirikiana na wizara husika kama lilivyozungumzwa na Mhe. Abdalla Ali Kombo; naye ni wazi tutashirikiana na sekta binafsi kutizama usafi na masuala mengine ambayo yanahusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, napenda sana kumshukuru Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na yeye kutoa ufafanuzi wa kina katika masuala yale ambayo yalikuwa yameulizwa. Kuna suala zima amelifafanua vizuri suala la *database*. Napenda kumhakikishia tu Mhe. Simai aliyeuliza suala la *database*, nataka kumwambia kwamba Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo hivi sasa haipokei pesa ya ana kwa ana, fedha zote zinapokelewa kwa njia ya benki na sisi tunakubali mfumo huo wa *electronic* ambao umezungumzwa na wengi. Kwa hivyo, mfumo aliopendekeza Mhe. Simai Mohammed wa *DFR* kutumika kwa kuwahesabu wageni, kutumika kwa kuhesabu mapato, kuwajua wageni wanavyoingia nao wote umefanyiwa kazi kwa namna yake.

Mhe. Rashid Makame Shamsi pongezi zake na waheshimiwa wote waliochangia pongezi zao tumezipokea, lakini pongezi za dhati alizopewa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein nazo tumepokea na tunaahidi kwamba salamu hizo mbali ya kuwa tutaonekana tutazifikisha kama vile zilivyowasilishwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, napenda sana kuwashukuru waliochangia kwa maandishi hususan Mhe. Masoud Abrahman Masoud wa Jimbo la Bububu ambaye aliweza kutaka kujua zaidi juu ya ujenzi wa uwanja uliojengwa Dole wa *Olympic* ambao mimi mwenyewe kwa ushahidi nimewahi kutembelea. Kweli uwanja ule upo na hivi sasa uwanja ule unatumika, ingawaje kulikuwa na matatizo mawili matati yaliyojitokeza juu ya mazao na miti iliyoharibiwa au iliyokuwa inatumika na wananchi wa pale. Nataka kumhakikishia kwamba Mhe. Mjumbe wananchi wake watamsikia kwamba amewatetea na sisi Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo tutashirikiana na yeye kuhakikisha namna gani suala lile la vitu vilivyoathirika linapatiwa ufumbuzi wake kwa wananchi wetu ambao wana malalamiko hayo.

Vile vile amechangia sana juu ya suala la historia akasikitika sana juu ya Msikiti wa Mkame Ndume ambao anahisi historia yake imepotea kabisa na hivi sasa haipo kabisa. Kwa hivyo, ni jukumu letu Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kupitia Idara yetu ya Makumbusho kuweza kutizama asilia hiyo ya historia iliyokuwepo, ikiwezekana tujue namna gani katika jitihada hii tunayokwenda nayo katika bajeti ya 2017/2018 vipi tutaweza kuyarudisha haya mambo yetu ya kale na historia yake. Na ukusanyaji wa mapato katika maeneo hayo kama alivyoeleza tutaendeleza jitihada tutaweka vitu vya kukusanyia mapato kwa njia za *electronic* vifaa na vile vile tunaweza tukaweka ofisi ndogo kwa kuweza kukusanya mapato hayo ili serikali iongeze mapato yanayotokana na utalii.

Mhe. Hidaya Ali Makame pamoja na kueleza mambo mengi katika mchango wake wa maandishi, namshukuru sana kwa pongezi zake kwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, ushauri wake mwingi aliyotoa tumepokea hususan uliyojaa kwenye habari kutaka kuwa na watu wa habari ambao wanajali uzalendo wa kufanya kazi zao zaidi kuliko kuweka yale maslahi yao mbele. Ushauri wake tumeuchukua.

Vile vile, tumechukua ushauri wa kuwasomesha wale watu nje ya nchi yetu, lakini inaonekana kwamba wanaporejea nchini wanapoteza uzalendo na wanafanya mambo ambayo yanakuwa ni kinyume na maadili katika sekta yetu hii ya habari. Ushauri huu tutauchukua na tutakuwa makini kabisa katika kuangalia yale ambayo wanayafanya wanaporudi masomoni. Kwa hili ikiwezekana katika kipindi hiki nataka nimhakikishie Mhe. Hidaya Ali Makame kwamba, kwa wale ambao watakuwa wanakwenda kinyume na taratibu wizara haitawavumila na hatua kali inaweza kuchukuliwa ikiwemo hata kumuachisha hizo kazi hata kama tumeshamsomesha na pesa zetu amechukua.

Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) alizungumzia sana juu ya masuala mazima ya habari namna gani hivi sasa Wizara ya Habari ilivyosimamia suala zima la habari, hususan katika vyombo vyetu vya televisheni na namna gani ving'amuzi ambavyo vinawezekana sasa hivi kuonekana pamoja na kuomba kuongeza *channel*. Utaratibu upo kama tulivyosema wafanyakazi wetu wa *ZMUX* ni endelevu, wafanyakazi ambao tunawapa motisha ya hali ya juu na ushauri wake tumeuchukua. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimeeleza mengi lakini kwa ujumla wake napenda sana kumshukuru Mhe. Spika kwa kamati yetu aliyotuchagulia, lakini vile vile kukushukuru wewe Naibu Spika kwa siku ya leo namna gani ulivyoendeleza huu mjadala wetu na mjadala wetu ulivyokuwa umekwenda na kukubalika kwa asilimia mia kabisa. *(Makofi)*

Mwisho kabisa nizitoe shukurani zangu kwa kupata pongezi maalum, nimepata pongezi maalum kwa Mhe. Abdalla Maulid Diwani wa Jimbo la Jang'ombe kwa namna anavyoona tumeibadilisha televisheni yetu na vile vile tulivyoweza kujenga Uwanja wa Gombani. Namshukuru sana Mhe. Abda Maulid Diwani kuona kwamba Uwanja wa Gombani ulilalamikiwa sana hususan kwenye upande wa *tartan.* Lakini jitihada zilizochukuliwa na wizara zimeweza kupeleka uwanja unapooneshwa kwenye televisheni unaweza kufanana na viwanja hata vilivyoko Spain, Ujerumani na Uingereza. Namshukuru sana Mhe. Abdalla Diwani. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri kwa ushirikiano wa pamoja tunaoufanya katika kazi zetu na wote kutukubalia kwamba kuona chombo hiki cha habari ni chombo muhimu ambacho kinaweza kikaueleza ulimwengu hali halisi ya Zanzibar au kinaweza kikasaidia kuweza kukuza uchumi, utalii na mambo mengine ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana naomba kutoa hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ameshatoa hoja kwa hiyo wale tunaokubali, tunaopokea hoja wanyooshe mikono. Nawashukuru sana hoja imepokelewa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Sasa tunaendelea na Hoja za Serikali kwa kuwa tuna muda wa kutosha wa Mhe. Waziri wa Afya kuweza na yeye kutoa hotuba yake, hivyo namkaribisha Mhe. Waziri wa Afya. Mhe. Waziri wa Afya karibu. *(Makofi)*

Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2016/2017

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Ustawi wa Jamii iliwasilisha ripoti ya shughuli walizofanya kwa mwaka 2016/2017 mbele ya Mkutano wa Tano wa Baraza la Tisa la Wawakilishi la Zanzibar, maagizo na ushauri mbali mbali ulitolewa kutokana na ripoti hiyo, ambapo sekta yetu ina wajibu wa kuyatekeleza na kuyafatilia yale yote ambayo imetakiwa kuyafanya.

Mhe. Naibu Spika, katika ripoti iliyowasilishwa na kamati Wizara ya Afya imetakiwa kitekeleza maagizo mbali mbali na pia kushauriwa katika masuala ya afya, ili kuweza kuimarisha afya za wananchi. Hivyo, utelelezaji wa maagizo hayo na ushauri umeelezwa katika taarifa hii ambayo nawasilisha.

Mhe. Naibu Spika, taarifa hii inaeleza maagizo na ushauri uliotolewa pamoja na utekelezaji wake ambapo imehusisha jumla ya maagizo 44.

Agizo 1. Kamati imeshauri serikali kuhakikisha kwamba bajeti ya Wizara ya Afya inaongezwa, ili mpango na utekelezaji wa kazi wa wizara ziweze kutekelezwa ufanisi mkubwa zaidi. Katika utekelezaji wake Mhe. Naibu Spika, serikali tayari imeshaongeza Bajeti ya Wizara ya Afya kutoka bilioni 44.2 kwa mwaka 2016/17 na kufikia hivi sasa shilingi bilioni 58.7 kwa mwaka huu tunaokwenda nao wa 2017/18, hasa katika Bajeti ya Dawa na Vitenganishi vya Maabara ambayo imepata ongezeko kubwa sana kutoka bilioni 4.8 hadi kufikia bilioni 7.2.

Matartajio yetu ni kwamba fedha hizi zitasaidia sana katika kutatua baadhi ya changamoto ambazo zinatukabili katika eneo hili.

Agizo 2. Mhe. Naibu Spika, ilikuwa serikali itoe kipaumbele cha ajira ka wataalamu wa Afya na hasa madaktari kwa kuwawekea maslahi mazuri na vivutio vya kazi kwa waliopo. Naomba kuelekeza utekelezaji wake Mhe. Naibu Spika, kwamba lengo la Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kwamba inapata wafanyakazi wa kutosha kwa ajili ya kutoa huduma

mbali mbali katika hospitali na Vituo vya Afya Unguja na Pemba. Kwa kuzingatia hili serikali imeagiza madaktari ya wafamasia wenye ngazi ya shahada ya kwanza kuajiriwa moja kwa moja pale ambapo watajitokeza kutuma maombi yao.

Kwa hiyo, hawa huwa watuwaachi na tunawachukuwa moja kwa moja. Pamoja juhudi hizi serikali pia inaendelea kuajiri wafanyakazi wa kada nyengine kwa mujibu wa mahitaji yanapotokeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka 2016/17 wizara imepatiwa nafasi za kuajiri jumla ya wafanyakazi 286 kupitia ajira za kujaza nafasi tupu ambazo zilikuwa 65 ziliachwa wazi na nafasia mpya 221 kwa fani mbali mbali. Hawa naomba nieleze Mhe. Naibu Spika, hawamo maodali ni wa fani kuagizia uuguzi, ukunga na kuendelea mbele. Katika nafasi hizo nafasi 180 zilitengwa kwa ajili ya hospitali ya Mmazi Mmoja tu na zilizoridhiwa hadi hivi sasa ni 152.

Hadi kufikia Oktoba 2017 mwezi huu wizara tayari imeshaajiri jumla ya wafanyakazi 131 kati ya hao wafanyakazi 74 ni wa Hospitali ya Mnazi Mmoja na napenda kueleza Baraza lako tukufu hawa waliripoti Jumatatu iliyopita na kwa vituo vingine ni 57 kwa Unguja na Pemba. Wafanyakazi wote waliajiriwa kwa mwaka 2016/17 wamo madaktari 45 wauguzi 102, wafamasia 2, fundi samifu 38, fundi sanifu maabara 4, fundi sanifu vifaa tiba 5, afisa tabibu 3, afisa afya mazingira 1 na mtaalamu wa viungo bandia 1. Hawa wote walitokana na vibali vya ajira vilitoka kwenye serikali moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, wizara imepokea pendekezio lililotolewa katika hoja nambari 26 ya kuongeza ajira za maafisa wa afya mazingira katika kila kituo cha afya. Hivi sasa tuko katika hatua za ugatuzi, hivyo, mawasiliano ya karibu sana yanaendelea baina yetu sisi na Halmashauri za Wilaya kupitia Wizara Tawala za Mikoa na mara tu mawasiliano hayo yatakapokamilika basi hatua hizi za kuajiri maafisa wa afya mazingira zitachukuliwa. Kwani vituo hivyo vya afaya hivi sasa tayari chini ya ugatuzi vipo katika Halmashauri za Wilaya ambayo iko chini ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na wao ndio watakaokuwa wanahusika moja kwa moja katika masuala ya ajira katika vituo hivyo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na hoja za maslahi ya wafanyakazi. Serikali imefanya juhudi ya kuongeza mshahara kwa wafanyakazi wake wote kuanzia kipato cha chini hadi wale waandamizi pamoja na kuongeza kiwango cha kipato cha chini katika sekta zote. Hili lilifanyika mnamo mwezi wa Aprili mwaka 2017. Katika suala hili madaktari wameangaliwa na kupewa kipaumbele cha juu kabisa ili kutunza wale waliopo na pia kuwavutia wafanyakazi wengine waliopo nje katika kada ya afya ili waweze kuja nchini kuja kuwatumikia wananchi. Kwa sasa mshahara wa chini wa daktari yaani *MD, Doctor of Medicine* unaanzia milioni 1,004,000 na daktari bingwa analipwa kuanzia milioni 1,283,000/= hadi milioni moja laki saba.

Sambamba na hilo wizara imekuwa ikilipa maposho mbali mbali kwa watendaji hao maposho hayo ni pamoja na posho la lilizo na posho la mazingira hatarishi. Aidha utekelezaji wa suala la ugatuzi litasaidia sana kubakiza wafanyakazi hususan katika maeneo ya vijijini kwani itatoa fursa za kuajiri wafanyakazi kupitia Halmashauri husika za wilaya.

Agizo 3. Wizara imeweke kanuni za maadili ya wafanyakazi kwa hospitali ya vituo vya afya pamoja na kuweka mfumo rahisi wa kutoa taarifa na maalalamiko kwa wananchi ambao wataona mabadiliko ya kazi yakivunjwa na baadhi ya wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji tayari kanuni na maadili ya wafanyakazi ni suala muhimu sana kwa wizara yetu. Wizara tayari imekaa na kujadiliana na bodi husika za wataalamu yaani *Professional Boards and Councils* ili kuona jinsi ya usimamizi wa uchukuwaji hatua kwa wale wote watakaobainika kukosea. Bodi za Madaktari na wauguzi ambazo ndizo mihilimi mikuu ya ya kusimamia maadili ya kiutendaji kwa kada husika tayari zimetengeneza miongozo yao *Code of Conducts and Practice* kwa ajili ya kusimamia masuala ya maadili pamoja na Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake ambayo inasimamia nidhamu kwa ujumla kwa watumishi wote.

Zipo kesi 6 ambazo tayari zimeshachukuliwa hatua baada ya Baraza la Wauguzi na Wakunga kupelekewa malalamiko rasmi. Kutokana na makosa hayo hatua zilizochukuliwa ni kupewa barua za onyo, onyo kali wahusika hao wengine kusimamishiwa leseni zao za kufanya kazi usajili za huduma za uuguzi na ukunga na wengine pia kusimamishwa kazi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, kuundwa kwa Bodi ya Maafisa wa Afya ya Mazingira ni miongoni mwa utekelezaji wa suala hili. Aidha wizara inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni ya Utumishi ya mwaka 2014 zenye kusisitiza maadili kwa wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na hoja ya kuweka mfumo wa kutoa taarifa za malalamiko kwa wafanyakazi. Hospitali ya Mnazimmoja imeanzisha huduma za malalamiko kwa wateja kwa saa 24 ambapo wagonjwa au jamaa wa wagonjwa hutakiwa kupeleka malalamiko yao kwa ajili ya wafanyakazi. Pia watendaji wa kitengo hicho wamejiwekea utaratibu maalum wa kuingia katika wodi za wagonjwa kwa ajili ya kujua matatizo yanayowakabili na upatikanaji wa huduma huduma husika. Aidha kumewekwa nambari ya simu maalum bila ya malipo ambayo kwa sasa inafanyiwa marekebisho pindi tu itakapokamilika basi nambari hiyo itapatikana na ikipigwa malalamiko yataweza kuwasilishwa na kushughulikwa mara moja.

Agizo 4. Serikali ifanye mpango wa kujenga nyumba za wafanyakazi wa hopsitali za Abdalla Mzee, ili kuondoa changamoto ya usafiri inayowakabili wafanyakazi hao.

Mhe. Naibu Spika, suala la ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali za Abdalla Mzee linafanyika kazi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya watu wa China. Serikali imetenga jumla ya shilingi bililioni moja kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizi ambazo zitajengwa ndani ya eneo la Hospitali ya Abdalla Mzee. Mnamo mwezi wa Julai 2017 wataalamu kutoka China walikuja Zanzibar kwa ajili ya kufanya mazungumzo juu ya ujenzi huo na walifika Pemba katika Hospitali ya Abdalla Mzee kwa ajili ya kuchukua vipimo vyote. Hatua zinazoendelea hivi sasa ni kufanya upembuzi yakinifu kuchora michoro husika pamoja na utengenezaji wa *BoQ*, ili mpango huo wa ujenzi uanze mara moja kwa kushirikiana na Serikali ya watu wa China.

Agizo 5. Kamati ilishauri wizara inapopelekewa au inapoletewa changamoto hasa zile ambazo zinauhitaji mkubwa katika utoaji wa huduma kuzifanyia kazi kwa kutafuta ufumbuzi, ili wananchi waweze kupata huduma kikamilifu. Tatizo la ukosefu daktari wa ganzi katika Hospitali ya Kivunge ni changamoto kubwa nayo ambapo kamati ilichukuwa nafasi hii kutushauri Wizara ya Afya na kuomba Wizara ya Afya kutatua kwa haraka.

Mhe. Naibu Spika, napenda kujuilisha Baraza lako tukufu kwamba Hospitali ya Kivunge sasa hivi tayari imeshapatiwa wataalamu wawili wa ganzi na usingi ambapo wapo hapo *full time* saa 24. Aidha katika kupunguza uchache wa wataalamu hawa nchini wizara tayari imeshapeleka masomoni jumla wataalamu 15 kwenda kusomea kada hizo 12 wako nchini Unganda 2 wako Tanzania Bara na 1 yuko nchini Misri hivi sasa wakiendea na masomo hayo. Wizara bado inazidi kuwashajihisha madaktari na wauguzi wajiendeleze zaidi katika fani hii ya ganzi na usinginzi.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia iliishauri wizara pamoja na serikali kwa ujumla kuangalia uwezekano wa kutoa kipaumbele kikubwa katika sekta ya afya kwa kuipangia bajeti ya kutosha ili changamoto kubwa ya ukosefu wa vitendea kazi dawa, ukosefu wa mafuta ya gari kwa baadhi ya taasisi za hopsitali ziweze kupungua kwa kasi kubwa ili taasisi hizo ziweze kufanya kazi na wajibu wao wa kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, serikali tayari imeongeza bajeti ya ununuzi wa dawa, vitenganishi na vifaa tiba kutoka bilioni 4.9 kwa mwaka uliopita hadi kufikia bilioni 7 kwa mwaka huu tunaokwenda nao. Fedha hizo ni pamoja na ongezeko la huduma mpya kama vile kusafisha njia ya mkojo na mafigo, matibabu ya saratani na vipimo vya *MRA*. Wizara ina matumaini makubwa kwamba huduma hizi zitazidi kuimairika ikiwemo upatikanaji wa dawa muhimu kwa wakati.

Agizo 6. Mhe. Naibu Spika, kamati iliishari wizara pia kuzidisha juhudi za kuajiri wafanyakazi watakaoweza kuziba mapengo yaliopo katika hospitali ya vituo vya afya mbali mbali ili dhana ya upatikanaji wa huduma za afya iweze kutumizwa.

Mhe. Naibu Spika, pia kamati iliagiza Wizara ya Afya kufanya uchunguzi wa kina kwa wahusika wote wanaochukuwa jukumu la kuwahamisha wafanyakazi wanaopelekwa Pemba pasi na kuwa na sababu maalum na kupelekea ukosefu mkubwa wa wafanyakazi na kurudisha nyuma juhudi zinazochukuliwa na serikali kuimirisha sekta ya afya. Hivyo, kamati ilichukuwa nafasi kuwasilisha kilio hiki katika ripoti yake hii ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa na serikali.

Katika utekelezaji wetu Mhe. Naibu Spika, wizara imepokea na imeufanyia kazi ushauri kwa kuzidisha juhudi za kuajiri wafanyakazi ili waweze kuziba mapengo yaliyopo katika hospitali na vituo vya afya. Aidha suala la kuwahamisha wafanyakazi wanaopelekwa Pemba kwa kuwarudisha Unguja hivi sasa suala hili limedhibitiwa na wizara na hatukubali tena kuwarudisha wafanyakazi waliopangiwa Pemba mpaka wamalize muda wao na wale watakaokuwa kutoka Pemba kuja Unguja hivyo hivyo hawatorudi Pemba mpaka wamalize muda wao waliopangiwa. *(Makofi)*

Agizo 8. Mhe. Naibu Spika, kamati ilishauri wizara iongeze wataalamu katika Hospitali ya Kivunge, ili kuokoa muda na fedha ambazo zimekuwa zikitumika katika harakati za kufanya rufaa kwa wagonjwa na kuwapeleka katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja, ili fedha

zitakazotumika kwa ajili ya mafuta zitumike kwa ajili ya kununulia dawa na vifaa muhimu vya hospitali.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa tayari Hospitali ya Kivunge ina daktari 5 *Assistant Medical Officer* 5, madaktari wasaidizi 5, wapiga picha wa *X-Ray* 2, daktari mtaalamu wa mifupa *Orthopedic Technologists 1, Sonographer 1* na muuguzi msaidizi wa usingizi na gazi wawili. Hata hivyo, ushauri wa kamati tumeendelea kuupokea na tutaendelea kuufanyia kazi kwa kuongeza idadi ya wafanyakazi wa Kivunge hususan ukizingatia idadi ya wagonjwa wanaofika Kivunge kupata matibabu.

Agizo 9. Kamati ilishauri wizara kufanya juhudi za makusudi za kutafuta wafadhili watakaotusaidia kujenga nyumba za madaktari katika vituo vya afya vilivyo nchini kwa lengo la kuondoa tatizo la makaazi kwa madaktari pamoja na kuwaondoshea usumbufu wanaopata hivi sasa baadhi ya madaktari wetu wa kutoka mjini ama kutoka sehemu za wanazoishi kwenda kwenye vituo vyao husika ambapo baadhi yao hulazimika kusafiri masafa marefu sana kuvifata vituo vyao vya kazi.

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wetu wizara imekuwa ikisaidiana sana na itaendelea kusaidiana na wafadhili mbali mbali katika kujenga nyumba wakiwemo *Milele Foundation, DANIDA, ADB* na pia kushirikiana na wananchi moja kwa moja kupitia Wawakilishi wao. Juhudi inayochukuliwa na wizara hivi sasa ni kwamba wafadhili wanaojitokeza wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi wanaotaka kujenga Vituo vya Afya baada yake huwa tunawaelekeza waende wakajenge nyumba za madaktari wasijenge tena vituo vya afya, kwa sababu tunavyo vituo vya afya vya kutosha na wakijenga nyumba za madaktari ni sawa na kujenga kituo cha afya, kwa sababu yule daktari atapata kukaa saa 24 katika eneo lile ili kuweza kufikisha huduma zile kwa wananchi moja kwa moja kwa wakati huo.

Kwa hiyo, hilo ni ombi letu kwa Waheshimiwa Wawakilishi kuhusiana na suala la nyumba na pia wanapotuchangia *Ambulances* kwenye vituo vyao basi watusaidie pia katika huduma za kuwapatia mafuta. Mara nyingi huwa tuna *Ambulances* nyingi ama Wawakilishi wamechangia *Ambulances* nyingi katika maeneo yao, lakini kunakuwa na uhaba wa mafuta kwa sababu hilo liko nje ya bajeti yetu.

Hata hivyo, uendeshaji wa Vituo vya Afya kwa sasa rasmi uko chini ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kupitia Manispaa na Halmashauri za Wilaya husika toka kuanza rasmi kwa zoezi la ugatuzi Julai mwaka huu. *(Makofi)*

Naomba pia niseme kwamba tunaendelea kushirikiana nao kwa karibu sana na kwa upande wa dawa, upande wa taalauma na fani za wafanyakazi bado tunaendelea kushirikiana nao kwa karibu sana ili kuwapatia *support* yoyote kutoka wizarani kwetu.

Agizo 10. Hospitali ya Kivunge ambayo kwa sasa imezidiwa katika utoaji wa huduma kutokana na kuhudumia karibu Mkoa mzima wa Kaskazini Unguja, wakati ilikusudiwa kuhudumia Shehia 7 tu. Kutokana na hali hiyo kamati inaomba wizara kufanya huduma kuwa bora zaidi za hospitali hiyo kwa kuipatia vitendea kazi vitakavyoweza kukidhi mahitaji.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya hivi sasa tayari kupitia mradi wake wa kupandisha hadhi Hospitali za Vijiji, Wilaya na Mikoa chini la Ilani cha Chama cha Mapinduzi imetenga fedha kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma katika ngazi za Mkoa. Aidha kwa kushirikiana na washirika wa kimaendeleo pamoja na *HIPZ* inasaidia upatikanaji wa vifaa tiba kwa wastani wa shilingi milioni mia nane zimetengwa kwa ajili ya kujenga jengo jipya la kima mama sambamba na kuimairisha huduma nyengine katika Hospitali hiyo ya Kivunge.

Agizo 11. Kamati iliishauri wizara kuimarisha huduma za vipimo vyote katika hospitali zake pamoja na vituo vya afya kwa lengo la kuwaondoshea usumbufu wananchi na hata wafanyakazi wanaotoa huduma hizo.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wake naomba niseme kwamba ushauri huu tumeupokea na tunaendelea kuufanyia kazi kwani wizara imefanya ufatiliaji mkubwa wa kuona hali halisi ya utoaji wa huduma za vipimo katika Vituo vya Afya na Hospitali. Kwa kuanzia wizara inaangalia vipimo ambavyo mama wajawazito wanatakiwa kuvipata pindi wanapohudhuria katika kituo cha afya ama *clinic* hizo.

Mambo yaliyobainika ni kwamba baadhi ya vyumba vinavyotumika kwa huduma za maabara ni vidogo haziendani na viwango huduma huwa zenye kusita sita na changamoto ya vifaa kwa ajili ya huduma hizo zinafanyiwa kazi. Taarifa hizo tayari zimeshaingizwa katika mpango kazi wetu, ili kuweza kuchukuliwa hatua muafaka mara moja.

Agizo 12. Kamati ilizidi kutoa wito kwa watendaji wakuu wa wizara kutambua wajibu wao na wawe na utaratibu maalum angalau kila baada ya miezi mitatu kuvitemebelea vituo vyao vya kazi, kwa ajili ya kutafuta changamoto na kuzichukulia kwa lengo za kuzifanyia kazi changamoto hizo.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wake zipo taratibu za kupatia vituo vya afya takribani kwa kila robo mwaka kuona kwamba hali ya utendaji vituoni hapo inaimarika. Ufatiliaji huu hufanyika kuptia vitengo tafauti pamoja na timu za afya za wilaya ambayo hutembelea vituo vya afya katika wilaya zao kwa kila robo mwaka. Pia wafanyakazi wa miradi mbali mbali kama vile, Maleria, UKIMWI na Kifua kikuu hutembelea vituo vya afya takribani kila mwezi kuona jinsi huduma hizo zinazotolewa.

Aidha kwa upande wa viongozi wakuu wakiwemo Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wamekuwa wakivitembelea vituo vya Afya kwa lengo hilo hilo la kuona kwamba changamoto na kuweza kuzifanyia ufumbuzi ambapo Waheshimiwa wamekuwa wakitembelea vituo vya afya katika ziara hizo huwa wanagundua.

Kamati pia ilishauri wizara ihakikishe upatikanaji wa vitenganishi kwa ajili ya shughuli za maabara kuwa za uhakika ili shughuli zote zinazopaswa kufanyika katika maabara hizo ziweze kutekelezwa kwa wakati. Aidha tatizo linalolalamikiwa na takrbani na wafanyakazi wengi wa wizara ni posho mbali mbali. Hivyo, kamati iliomba wizara ilichukuwe suala hili ilifanyie kazi pamoja na hatua kadhaa zilizokwisha kuchukuliwa katika kulitatua.

Mhe. Naibu Spika, ushauri huu tumeuchukua na tunaendelea kuufanyia kazi. Kwani bajeti ya dawa ambayo inajumuisha na ununuzi wa vitendanishi imeongezeka, kama nilivyosema hapo awali, kutoka bilioni 4.9 hadi kufikia bilioni 7 katika mwaka 2017/2018.

Aidha, suala la maposho mbali mbali linaendelea kutolewa likiwemo posho la likizo na maposho baada ya saa za kazi, ambayo hutolewa kulingana na kima cha mshahara wa mfanyakazi husika.

Kamati pia ilishauri wizara na serikali kwa ujumla kujitahidi kutafuta wafadhili watakaosaidia ujenzi wa maabara, ikiwa ni pamoja na wizara kuanza mchakato wa kutafuta maeneo maalum yatakayokuwa karibu na maeneo ya vituo vya afya kwa ajili ya kujenga maabara za kisasa zitakazosaidia kwa kasi kubwa upatikanaji mzuri wa huduma za afya kwa wananchi moja kwa moja.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa sera ya afya, vituo daraja la pili na hospitali zote zinatakiwa kuwa na maabara zitakazo saidia kutoa huduma kwa wananchi. Hata hivyo, vipimo vinavyotolewa huwa vinatofautiana kulingana na daraja la kituo ama hospitali. Huduma za maabara zinazotolewa katika kituo cha daraja la pili, sio sawa na zile zinazotolewa katika hospitali za vijiji. Hata hivyo, kuwa na maabara za kisasa ni ushauri mzuri na wizara itauzingatia ushauri huo wa kamati.

Hoja 15. Kamati imezidi kusisitiza kwa kuishauri wizara kujitahidi katika upatikanaji wa vitendea kazi, hasa kwa hospitali na vituo vya afya vya vijijini, ambavyo vinakabiliwa na ukosefu wa nyenzo za usafiri na gari za kubebea wagonjwa.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, ushauri huu tumeupokea na tunaendelea kuufanyia kazi, kwa kutambua hilo, hivi karibuni tu wizara imenunua gari nne kwa ajili ya kusafirishia wagonjwa na kugaiwa gari hizo katika hospitali ya Wete, Micheweni, Makunduchi na Kivunge zikiwa hospitali zetu kuu za wilaya. Maana hospitali ya Mkoani imeshakuwa hospitali ya Mkoa. Pamoja na hayo upatikanaji wa dawa na huduma za uchunguzi umeimarishwa ili kuwaondelea usumbufu wananchi hao.

Hoja 16. Kamati pia ilishauri utatuzi wa haraka wa ukosefu wa huduma ya maji safi na salama, ulinzi na hata uzio kwa baadhi ya hospitali na vituo vya afya kama vile hospitali ya Wete, Makunduchi, na vituo vya Kizimkazi Dimbani na Mkunguni, ili kuepusha uharibifu wa mali na hospitali na vituo vya afya.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Wete tayari imeshapatiwa uzio kwa hatua ya awali. Tathmini ya kujenga ukuta kwa hospitali ya Makunduchi tayari imeshafanywa, ambapo Tsh 211,000,000/= zinahitajika kugharamia kazi hiyo. Wizara itaendeleza juhudi hizi kwa vituo vya afya na hospitali nyengine, kama ushauri ulivyotolewa.

Hoja 17. Kamati ilifurahishwa sana na hatua ya ujenzi iliyofikiwa katika Hospitali ya Micheweni, hivyo kamati inaisisitiza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na viongozi wa Jimbo la Micheweni na Wilaya ya Micheweni, kupitia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, kujitahidi kuchangia fedha zinazohitajika ili kumaliza ujenzi huo, ili lengo lililokusudiwa la kuifanya

hospitali hiyo ya wilaya liweze kutimia sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) nayo iweze kutimia.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya imeunda kamati kwa ajili ya kushughulikia suala zima la ujenzi, kupitia mradi wake wa kupandisha hadhi hospitali zote za vijiji, Wilaya na Mkoa. Kwa sasa kamati iko kwenye hatua ya kufanya tathmini ya kumalizia utengenezaji wa chumba hicho cha upasuaji kwa Hospitali ya Micheweni na kuwasilisha ripoti kwa hatua za Zabuni kupitia njia ya kisheria ya zabuni ya serikali.

Hoja 18. Kamati ilizidi kusisitiza ushauri wake kwa Wizara ya Afya, kuhakikisha kuwa inatoa ajira za kutosha kwa lengo la kupunguza tatizo la uhaba wa madaktari, wauguzi pamoja na wataalamu wengine katika ngazi tofauti.

Kutokana na kadhia hiyo, kamati inasisitiza wizara kufanya juhudi za baadhi ya majengo yake na kuyafanyia matengnezo yale yote ambayo ni finyu na yamechakaa. Pia, kamati inaishauri wizara ijitahidi kutafuta vifaa vya huduma, tiba na viungo yaani upande wa *'physiotherapy'*.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kutokana na mahitaji makubwa ya madaktari, wauguzi na kada nyengine za kitaalam, wizara imeweka wazi maombi ya ajira kwa kuanzia na madaktari, pindipo daktari akileta maombi ya kazi basi anaajiriwa mara moja.

Vile vile, wizara imekuwa ikiendelea na juhudu zake za kujenga majengo ya utoaji wa huduma na kufanya matengenezo Vituo vya Afya vipatavyo 15 kupitia Mradi wa '*Orio'* ambavyo hivi sasa viko katika hatua ya kumaliziwa matengenezo hayo. Pia Mhe. Naibu Spika, ujenzi wa jengo la Mapinduzi Mpya umo katika mradi mkubwa wa ukarabati wa hospitali ya Mnazi Mmoja utakaogharamiwa kwa mashirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, *BADEA*, Mfuko wa Kuwait na Mfuko wa Saudi Arabia.

Mhe. Naibu Spika, hivi majuzi tu tulibahatika Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kutiliana saini na Mfuko wa *Quwait Fund* kwa ajili ya matengenezo hayo. Sasa tukisubiri hatua zitakazofuata za kupatikana fedha ili ukarabati huo uanze.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu pia inatambuwa umuhimu wa kitengo cha *Physiotherapy*, yaani viungo, ndio maana kwa makusudi ilifanyia ukarabati jengo la kitengo hicho pamoja na sehemu ya kutengeneza viungo bandia katika kiwanda cha zamani cha dawa, yaani lile jengo jipya. Ushauri wa kutafuta vifaa vya huduma, tiba na viungo '*pysiotherapy'* tumeupokea na wizara inaendelea kadri iwezavyo kutafuta Wafadhili ili kusaidia huduma mbali mbali katika eneo hili.

Hoja 19. Mhe. Naibu Spika, kamati ilisikitishwa na taarifa iliyoipata katika hospitali ya Chake Chake na nyengine kama zilivyotajwa katika changamoto zilizozikumba na tatizo la uambukizaji wa maradhi ya kifua kikuu kwa wafanyakazi wakati wa utoaji huduma kwa wagonjwa wa maradhi hayo.

Aidha, kamati inaiagiza wizara kufanya juhudi za makusudi kwa kuwatambua madaktari waliothirika na kuchukuwa hatua za kuwatibu, pamoja na kuwapa stahiki zao zote ambazo wanastahiki kulipwa. Kutokana na kadhia hiyo, kamati inasisitiza wizara kufanya juhudi za

kutanua baadhi ya majengo yake na kuyafanyia matengenzo yote ambayo ni finyu na yamechakaa. Pia kamati inaishauri wizara ijitahidi kutafuta vifaa vya huduma, tiba na viungo yaaani '*physiotherapy'*

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya, tayari inafuatilia suala la wafanyakazi sita ambao wametajwa kwa karibu sana, ambao wamebainika kuathirika na maradhi ya kifua kikuu pindi wakiwakazini, na taratibu za kufuatilia mafao yao inaendelea kusimamiwa. Aidha, Kitengo cha '*Physiotherapy'* kitafanyiwa ukarabati kwa msaada wa Kampuni ya '*Infant Clubfoot Appeal* ya Uingereza hivi karibuni.

Hoja 20. Mhe. Naibu Spika, kamati inashauri hatua za haraka zichukuliwe kwa ajili ya kukarabati paa la Hospitali ya Chake Chake, ili wagonjwa wapate unafuu wa afya zao na pamoja na sehemu wanazokaa, kwani hali hiyo inawavunja moyo kutokana na ukweli kwamba mgonjwa hutegemea anapokwenda hospitali kupata nafuu, lakini kutokana na hali iliyopo hospitalini hapo inawavunja moyo na kuwazidishia matatizo, ambapo badala mgonjwa kufikiria afya yake wakati wa mvua inabidi afikirie na sehemu ya kukaa kutokana na kuvuja kwa majengo ya hospitali.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia mradi wa kupandisha hadhi hospitali za vijiji, Wilaya na Mkoa wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 400, ambazo zitatumika kwa ukarabati wa Hospitali ya Chake Chake tu. Aidha, katika ukarabati huo suala la choo kwenye Wodi ya Kifua Kikuu pia litapatiwa ufumbuzi pamoja na paa. Kwa sasa mradi unasimamia tathmini ya majengo yote ya Hospitali ya Chake Chake ili kuandaa *BOQ* kwa ajili ya hatua za Zabuni.

Hoja 21. Mhe. Naibu Spika, kamati pia iliagiza wizara kutafuta tangi la maji (*tank*) na kulipeleka katika hospitali ya Chake Chake, kwa ajili ya kuweka maji ya akiba yatakayotumika katika maabara, pamoja na maeneo yote yatakayohitaji huduma hiyo hospitalini hapo.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, naomba nilijulishe Baraza lako tukufu kwamba, tayari Hospitali ya Chake Chake imeshapatiwa maji ya uhakika na hilo *tank,* kwani kipo kisima ambacho kiko hapo pembeni, kinapeleka maji moja kwa moja hospitalini hapo.

Hoja 22. Kamati, pia iliagiza wizara kuangalia upya mfumo wake wa uombaji wa dawa kwa hosptali zake, ili kuondoa tatizo linalojitokeza hivi sasa la kucheleweshwa upatikanaji wa dawa muhimu, ambapo tatizo hili limeikumba hospitali ya Vitongoji na nyengine, hasa ikizingatiwa kuwa mfumo huo wa '*pull'*, ambao unahitaji kituo cha afya husika au hospitali kupeleka mahitaji ya dawa bohari na kupatiwa dawa hizo kwa mujibu wa mahitaji.

Hata hivyo, mfumo huo umekuwa na tatizo la uchelewaji wakupatikana kwa dawa zinazoombwa, licha ya maombi kuwa yanafanyika mapema na dawa zinapopatikana kunakuwa na upungufu wa dawa muhimu. Aidha, kamati pia iliwasilisha taarifa yake kuiomba wizara kusimamia watendaji wake ipasavyo, ili uzembe kama huo usiendelee kuwepo ama kusubiri mpaka kamati ipitie vituo ndipo hatua stahiki kuchukuliwa.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, wizara imeanza kuupitia mfumo uliopo hivi sasa wa usambazaji dawa kwa kila kipindi cha miezi mitatu, utaratibu wa kupitia tena mfumo huo huwa unafanyika,

yaani *quarterly review*, ili kuongeza kasi ya upatikanani wa dawa muhimu,wizara inajiandaa kuanza kusambaza dawa kwa kila mwezi kwenye hospitali na vituo vyote vya afya kutokana na mahitaji yao halisi. Naomba nirudie hapa. Kutokana na mahitaji yao halisi, utaratibu huu utakapoanza utapunguza sana upungufu wa dawa katika vituo mbali mbali. Tunaondokana na ule utaratibu wa kupeleka dawa zote kwa pamoja, badala yake tunapeleka zile dawa ambazo zinahitajika au zimekwisha kwenye kituo husika na sio zile dawa ambazo ziko pale tayari.

Mhe. Naibu Spika, wizara imeshafanya tathmini ya gharama za matengenezo za mfumo wa maji safi na salama katika hospitali ya Vitongoji. Aidha, wizara inajiandaa kutoa mafunzo kwa mafundi mifereji na michirizi ili kutatua changamoto za maji safi na maji machafu katika hospitali zote.

Mhe. Naibu Spika, hoja za ujenzi wa nyumba za wafanyakazi wa hospitali na vituo vya afya ni moja ya mikakati ya wizara. Aidha, ushauri huu tumepokea kutoka kwenye kamati na tutaendelea kulifanyia kazi.

Hoja 23. Mhe. Naibu Spika, jengine ni changamoto iliyokutwa na kamati katika Kituo cha Afya Bogoa. Kamati imeshauri kuwa ni vizuri katika muundo wa utawala kuwepo na mtu wa maabara, ili aweze kufikisha na kushauri kitaalamu shughuli zinazohusu maabara na kutolewa maamuzi stahiki, ambayo yatainufaisha maabara ya kituo hicho cha Bogoa.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kwa sasa Kituo cha Afya Bogoa yupo mfanyakazi mmoja wa maabara, ingawa bado mfanyakazi mwengine anahitajika ili wawe wawili, hivyo pindi akipatikana tu mfanyakazi huyu basi atapangiwa kazi kituo cha Bogoa. Aidha, kituo chenye daraja kama cha Bogoa kiutawala nikimaanisha mkuu wa kituo basi anapaswa kuwa ni '*Clinical Offìcer'*yaani *CO*. Yupo mshauri wa masuala ya maabara kwa ngazi ya wizara ambae anatakiwa kutoa ushauri wa fani hiyo katika hospitali na hata vituo vyetu vya afya.

Hoja 24. Jengine Mhe. Naibu Spika, kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza serikali kwa uamuzi wake wa busara wa kutafuta wafadhili, ambao ni ndugu zetu wa Serikali ya China ambao walijitolewa kwa hali na mali katika kujenga upya hosptaili yetu ya Abdalla Mzee, iliopo Mkoani Pemba, ambayo kwa kiasi kikubwa inasaidia kutatua changamoto nyingi zilizokuwa zinawakabili wananchi moja kwa moja.

Hata hivyo, kamati ilielezwa changamoto ya ukosefu wa wafanyakazi wa kutosha, ambao wataweza kuhudumia hospitali za hapo, hivyo kamati inaiomba serikali kama ilivyofanya jitihada za kutafuta wafadhili wa kujenga Hospitali ya Abdalla Mzee, basi ihakikishe kuwa inajitahidi kupeleka wafanyakazi wa kutosha katika hospitali hiyo. Aidha, kamati baada ya kukagua jengo la hospitali hiyo inashauri mambo manne kama yalivyoainishwa katika ripoti yao.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji.

i. Hospitali ya Abdalla Mzee inatumia jenereta ambalo liko (*automatic*) kwa ajili ya udhibiti vifaa wakati umeme ukizimwa. Pia Wizara imeendaa bajeti kwa ajili ya mashine za kudhibiti umeme (*stabilizer*) kwenye mashine kubwa kama *CT SCAN*, *X-Ray*, vifaa vya maabara na vifaa vyengine.

ii. Kwa sasa wizara imeshampeleka mtaalamu wa vifaa tiba ili kutathmini na kutoa taaluma kwa watumiaji kwa lengo la kuhakikisha wanavitumia vifaa vyote kwa utaratibu kwa kupitia miongozo na vielekezi (*SOPs*). Hii itasaidia vifaa hivyo kudumu kwa kutumika kwa muda mrefu.

iii. Suala la usalama kwa Hospitali ya Abdalla Mzee. Hili Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kwamba, lipo vizuri kwani ipo kampuni ya ulinzi ambayo inalipwa ili kutoa huduma za ulinzi saa 24 hapo Hospitali ya Abdalla Mzee.

iv. Wizara inajiandaa kuchukuwa kampuni ya usafi kwa Hospitali ya Abdalla Mzee, ili kutatua changamoto za usafi na changamoto ya upungufu wa wafanyakazi wasafishaji iliyokuwepo hospitalini hapo.

Hoja 25. Mhe. Naibu Spika, kamati pia imewasilisha taarifa iliyopewa kuhusiana na mgogoro wa ardhi wa muda mrefu uliopo baina ya familia husika na Chuo cha Afya Bweni.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, hati miliki ya eneo tayari imepatikana mwezi. Mvamizi amepewa notisi ya siku kumi ya kuvunja eneo lake, la si hivyo serikali itavunja eneo hilo. Mjenzi wa ukuta ambaye aliyeshinda Magereza ameshakaguzwa eneo lote hilo, ili ajenge ukuta kwa haraka iwezekenavyo. Kwa sasa naomba niseme suala hili limeshaondoka kwetu Wizara ya Afya, kwa sababu kile chuo kimeshahamishwa kutoka Wizara ya Afya, kiko SUZA. Kwa hivyo, kile kituo kiko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. *(Makofi)*

Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, tumekuwa tukiwasiliana naye kwa karibu sana amekuwa akifuatilia kwa karibu sana suala hili la uzio kwa pale Chuo cha Afya, chini ya usimamizi wake mahiri naamini nalo litakamilika.

Hoja 26. Mhe. Naibu Spika, suala la ukosefu wa ajira kwa wataalam wa masomo ya afya ya mazingira, kamati inatoa ushauri kwa wizara ishirikiane na Wizara ya Nchi afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kuzishauri halmashauri ziwaajiri wataalam hao na pia wizara ijitahidi kuwaajiri katika kila kituo cha afya wataalamu hao.

Utekelezaji. Mhe.Naibu Spika, Wizara ya Afya imekuwa ikishirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Nchi afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, hasa pale ilipokuwa kuna maradhi ya kipindupindu, ambapo wafanyakazi wao walishiriki kikamilifu na hasa Maafisa wa Afya ngazi za wilaya, hadi kufanya sote kwa pamoja kufanikiwa kukiondosha kipindupindu katika muda mfupi. Katika masuala mbali mbali ya kuimarisha afya ya mazingira, hata hivyo wizara itaendeleza mashirikiano ya karibu hasa katika ajira za Mabwana Afya ambao watakuwa moja kwa moja wilayani chini ya tawala za mkoa, ambao watakuwa wanafanyakazi katika maeneo haya. Haya tutashirikiana na mara tu itakapopatikana nafasi hiyo basi wafanyakazi husika watapelekwa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Hoja 27. Mhe. Naibu Spika, kamati pia iliiomba Wizara ya Afya izidishe juhudi ya kuweka vifaa vingi vinavyokosekana katika Hospitali ya Mnazimmoja, ili wanafunzi wanapofanya mafunzo kwa vitendo waweze kujifunza kwa uhakika ikiwemo kuviona na kuvifanyia kazi, vifaa vyote walivyojifunza wakiwa chuoni kwao.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Taifa cha *SUZA* inahakikisha wanafunzi wanapata eleimu bora kwa nadharia na vitendo. Kwani katika sheria ya Hospitali ya Mnazimmoja tayari ni hospitali ya kufundishia na ina mashirikiano pamoja na mkataba na *SUZA* moja kwa moja katika kuwapa mafunzo wanafunzi hao ya vitendo.

SUZA iliingia makubaliano hayo ya (*MoU*) na hospitali ya Mnazi Mmoja jinsi ya kuhakikisha kuwa vifaa vyote na wataalamu wote kwa ajili ya masomo ya vitendo vinapatikana kwa wakati wote hospitalini hapo. Aidha, kwa sasa hospitali inavyo vifaa vyote vinavyohitajika kwa kujifundishia na hatuna upungufu wa aina yoyote. Pia, Hospitali ina wataalamu wa kutosha wa fani mbali mbali na kwa ngazi mbali mbali hadi, kutokana na hayo mafunzo ya Shahada ya Uzamivu yanayotolewa hivi sasa.

Hoja 28. Mhe. Naibu Spika, kamati inazidi kusisitiza ushauri wake kwa wizara pamoja na serikali kwa ujumla kuhakikisha kuwa inaajiri wafanyakazi wa kutosha katika sekta ya afya, kwa ajili ya kukidhi mahitaji na kupunguza tatizo la ukosefu wa madaktari, jambo ambalo limekuwa ni changamoto kubwa na kila hospitali na kituo cha afya kilichotembelewa na kamati hii ya ustawi wa jamii

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri bado ana kurasa nyengine kama 7 au 8 katika kitabu chake cha ripoti au taarifa ya utekelezaji na ingekuwa vizuri zaidi akaimaliza mchana huu wa leo kwa hiyo nmuomba sana Mhe. Waziri Haji Omr Kheir atutengulie kanuni ya muda ili tuweze kuendelea,

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika kwa mujibu wa Kanuni ya 23 naomba Baraza lako Tukufu tuweke Kanuni ya muda kando, ili Mhe. Waziri wa Afya aweze kumalizia hotuba yake. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyoshe mikono, wanaokata, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Afya, karibu uendelee.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na idara Maluum za SMZ kwa kutoa hoja hiyo ya kuongeza muda.

Mhe. Naibu Spika, Aidha, kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa upatikanaji wa vifaa vya afya pamoja na chanjo kwa watoto, kwa lengo la kuepusha maradhi ambayo yanaweza kuwaathiri watoto wachanga.

Hata hivyo, Hospitali ya Mwembeladu inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa *AC* katika chumba cha kuhifadhia mashine ya *CD4*, mashine ambayo ni ya gharama kubwa. Kamati inashauri serikali kufanya jitihada za kununua *AC*, kwa ajili ya chumba hicho ili kupunguza gharama ambazo zinaweza kujitokeaza.

Pia, kamati inaishauri Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kufanya mpango wa haraka wa kukihamisha kituo cha daladala kilichopo mbele ya mlango wa Hospitali ya Mwembeladu, ili kuondosha kero kubwa sana ya msongamano na usumbufu mkubwa kwa mama wajawazito wanaowahishwa katika kituo hicho kujifungua na wale wa rufaa.

Suala la sare za wafanyakazi kujikatia wenyewe. Kamati iliishauri wizara ilifuatilie jambo hili kutokana na ukweli kuwa suala hilo ni jukumu la serikali kuhakikisha kuwa wafanyakazi wake wanapata sare za afisi na kada nyengine wanavyofanyiwa na afisi zao wakiwemo askari, ambao wamekuwa wakipatiwa sare hizo na taasisi na sio kujinunulia wenyewe kwa pesa zao.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, chanjo zote hivi sasa zinapatikana katika vituo vya afya na hospitali isipokuwa chanjo ya *BCG* ambayo inakinga maradhi ya kifua kikuu. Chanjo hii ilikosekana kuanzia Julai 2017 na inatarajiwa kupatikana mapema mwezi ujao wa Oktoba. Hata hivyo, watoto wote waliokosa chanjo hiyo katika siku walizopangiwa basi tutahakikisha wanapatiwa chanjo hizo mara tu chajo hizo zitakapowasili. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa kidogo naomba nitoe maelezo ya ziada chanjo hii ilikosekana sio kwa kukosa fedha sisi au kwa upande wetu, isipokuwa ilikuwa huko huku masuala ya kilimwengu zaidi, kwa sababu chanjo hizi zinakuwa *regulated* na haya mashirika ya kimataifa na chanjo hii ilikosekana katika masuala hayo ya kilimwengu zaidi kupita *GAVE*.

Mhe. Naibu naomba nijulishe Baraza lako tukufu pamoja na Kamati kuwa, *'AC'* tayari imeshanunuliwa katika chumbo hicho na hivi sasa inafanya kazi kwa ubaridi wa hali ya juu kabisa hapo Mwembeladu Hospital na mimi nilibahatika kwenda kuonja ubaridi wake.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kituo cha daladala cha Mwembeladu kimekuwa kikileta usumbufu mkubwa kwa wazazi wanaokuja kujifungua na wafanyakazi wa Hospitali ya Mwembeladu. Usumbufu pia unajitokeza wakati wa kuingia au kutoka kwa Ambulance pale Mwembeladu kwa sababu zile dala dala zinapaki pale getini kabisa, Wizara tayari imeshaandikia barua rasmi kwa afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ juu ya ombi la kuondolewa kituo hicho na wizara husika inalifanyia kazi tatizo hilo.

.

Mhe. Naibu Spika, kadri hali ya fedha itakapoimarika basi wizara itanunua sare za wafanyakazi. Aidha tayari ununuzi wa sare umeingizwa katika mpango kazi wa Idara ya Huduma za hospitali na tayari hospitali ya Abdalla Mzee wafanyakazi wake wamepatiwa sare mbili mbili za sare kila

mmoja, kwa hivyo tutatoka kwenye hospitali moja kwenda nyengine kadri ya bajeti itakavyopatikana ya idara hii.

Agizo 29. Kamati, inaishauri wizara ichukue tatizo liliopo hivi sasa katika Kituo cha Afya cha Shakani, kituo cha Bimwanaasha na katika ripoti ya mwakani, kamati itahitaji maelezo ya maendeleo ya kituo hicho juu ya suala la ukarabati wake ulipofikia.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, wizara imo katika harakati za kutafuta ufadhili nnjeya bajeti yake iliyokuwa imejipangia ili kukijenga upya Kituo cha Shakani hivyo,kituo hiki kimo katika mipango ya kutafutiwa ufadhili kama baadhi ya vituo vyetu vyenginevinavyohitaji kutengenezwa tunavyoendelea kuzungumza na wafadhili, tunaendelea na jitihada ya kutafuta mfadhili kama itawezekana basi katika mwaka huu wa fedha.

Agizo 30. Kamati, imefurahishwa na taarifa kuwa Kituo cha afya Bwefum kimo katika mpango wa kujengwa upya kupitia ufadhili wa washirika wa maendeleo katika sekta ya afya. Kamati, inashauri ujenzi huo uende sambamba na kuzuia uvamizi wa meneo ya kituo pamoja na kukipatia kituo hicho hatimiliki ya eneo lake.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Wizara ya Afya imelichukua agizo hili na tayari imeshaanza upimaji katika baadhi ya vituo, ili vituo vyote viwe na hati miliki. Kwa muda huu taratibu zinaendelea kwa vituo vya afya 15 kupatiwa hati miliki, na kila tukimaliza awamu moja tutaelekea awamu nyengine yavituo 15 vyengine. *(Makofi)*

Agizo 31. Kamati, inaishauri serikali kukipa kipaumbele Kituo cha Damu Salama kwa kukiongezea bajeti, ili kiweze kujiendesha na kuondoa changamoto zilizoelezwa hasa ikizingatiwa umuhimu wa shughuli zinazofanywa kituoni hapo pamoja na umuhimu wa upatikanaji wa damu salama katika hospitali zetu zote za Unguja na Pemba. Pia, kamati inashauri basi lililopata ajali la kituo litengenezwe haraka iwezekanavyo, kwa ajili ya kuweza kufanya kazi kama lilivyokuwa mwazo na kuepusha kuchakaa zaidi endapo litakaa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo na kuongeza gharama zisizo za lazima.

Kamati, inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kutoa umuhimu wa haraka wa kupatikana fedha za ukarabati wa basi hilo, ambalo linasaidia sana kuzunguka maeneo tofauti kwa ajili ya kukusanya damu. Kwa kweli, kuharibika kwa basi hilo kunapelekea zoezi la ukusanyaji wa damu kuwa na changamoto na kama tunavyojuwa kuwa akiba ya damu ni muhimu katika hospitali zetu zote.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2017/2018, wizara imetenga jumla ya shilingi milioni 300 kutoka fedha za maendeleo kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa Damu Salama kwa hapa Zanzibar, bajeti hiyo itakwenda moja kwa moja kwa benki kuu hiyo ya damu salama. Aidha, tokea mwezi April 2016, wizara ilifanya malipo ya shilingi 23,900,000 moja kwa moja kwenda Kampuni ya '*Budda Autopart'* kwa ajili ya matengenezo ya basi, matengenezo ya basi hilo yanaendelea kupitia kampuni hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri jana nilibahatika kulitembelea basi hilo kutokana na ripoti hii, wanachosubiri sasa hivi ni vioo vile vilivyovunjika, kidogo kumetokezea tatizo la kupatikana

vioo hivyo kutoka China, kwa sababu lile basi ni la zamani kidogo na vioo hivyo walishaacha kutengeneza. Kwa hivyo, tunaomba inafanyiwa *modification* maalum ya vioo hivyo na vitakuwa viko njiani hivi karibuni kufika hapa Zanzibar.

Agizo 32. Kamati, inapenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Bodi ya Chakula Dawa na Vipodozi kwa mafanikio mengi iliyofikia katika utendaji wake wa kazi. Hata hivyo, kamati inaiagiza bodi kuwachukulia hatua kali wafanyabiashara wote wanaojihusha na kughushi bidhaa na nyaraka mbali mbali kutokana na kukosa uaminifu kwa wafanyabiashara.

Vile vile, kamati inaigiza Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi kwa kushirikiana na taasisi zote husika kuzidisha juhudi za ukaguzi, ili iweze kuzibaini sehemu zinazotumika kuficha vyakula ambavyo havijakaguliwa na kuingizwa sokoni bila kukaguliwa.

Kamati inaishauri wizara kwa kushirikiana na taasisi za ulinzi serikalini, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika bandari na njia zote zisizo rasmi, ambazo hutumika kupitisha vyakula, dawa na vipodozi. Hivyo, kamati ianagiza wahusika wote wanoshiriki katika kufanya vitendo hivyo wachukuliwe hatua kali kama sheria inyoelekeza.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi *(ZFDA)* itaendelea kushirikiana na taasisi nyengine za Kiserikali na zisizokuwa za Serikali katika kuimarisha udhibiti wa Ubora na Usalama wa bidhaa za Chakula, Dawa na Vipodozi kwa hapa Zanzibar ili kulinda Afya ya Jamii na wananchi wote.

Aidha, *ZFDA* itaendelea kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama katika kuwadhibiti wale wote watakaokwenda kinyume na matakwa ya sheria, kupitia vyombo vya kusimamia sheria.

Naomba nitoe taarifa kwamba jana bodi hii imekamata mzigo mkubwa sana wa vyakula ikiwemo, kuku, mchele na vifaa vyengine na vyakula hivyo vilikuwa havina tarehe ya *manufacture* wala *expire* inawezekana ikawa havijaharibika, lakini sheria yetu inatakiwa chakula kile kiwe na tarehe ya *manufacture na expire* kabla hakijaingia nchini. Kwa hivyo, vyakula vyote hivyo tulivikatalia kuingia nchini mpaka viwe na tarehe hiyo husika kwa hivyo bodi hii inaendelea kufanya kazi zake vizuri sana. Kutokana na hali hiyo, tutakataa maombi yoyote yatakayokuja ya kusaidia katika suala hili, kwa sababu kwetu sisi kulinda ya afya za wananchi ni jukumu letu la kwanza, lazima kwa nchi yetu na dhima kwa Mwenyezi Mungu pia. *(Makofi)*

Agizo 33. Kamati inaishauri wizara kuipatia vifaa Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi, ili iweze kufanya kazi zake vizuri nakuondokana na tatizo liliopo hivi sasa la uchakavu wa vifaa, kutokana na hali hiyo. Kamati inaagiza kuchukuliwa hatua kali pamoja na kupewa adhabu kali kama seira inavyoelekeza kwa wafanyabiashara wanaokwepa kulipa ushuru wanapoingiza bidhaa nchini na wale wote wanaotoa ushirikiano finyu, wakati wa kukaguliwa ama kuchunguzwa bidhaa zao, ili iwe fundisho kwa wengine wote.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi kupitia mpango mkakati wake, inakusudia kuimarisha huduma za uchunguzi wa kimaabara ikiwemo mafunzo kwa wachunguzi na ununuzi wa vifaa vya maabara na kupata ithibati ya kimataifa ya maabara chini

ya mpango wa uwiyano wa usajili wa dawa kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC).*

Kwa hivyo, katika Jumuia ya Afrika ya Mashariki tunaingia moja kwa moja kama Zanzibar na cheti hicho tutapata na chakula kitakachokuwa kinaingia kutoka sehemu yoyote kikiingia katika mipaka ya Zanzibar, basi cheti chake kitatambulikana katima mipaka ya Afrika ya Mashariki.

Agizo 34. Kamati inaiagiza kuchukuliwa hatua kwa wawekezaji wote wasiofuata utaratibu uliowekwa hapa nchini hasa wawekezaji wa mahoteli wenye tabia ya kuja na dawa kutoka katika nchi wanazotoka na wakiondoka kuziacha dawa hizo na kuanza kuuzwa katika vituo vya vijijini.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kupitia Wakala wa Bodi ya Chakula Dawa na Vipodozi, jambo hili la kuingiza dawa bila kufuata utaratibu na kuziingiza kwenye mifumo yetu ya utoaji wa dawa limeshabainika na hatua zitachukuliwa kwa wale wote watakaokwenda kinyume na sheria iliyowekwa juu ya usambazaji dawa.

Agizo 35. Kamati, inaigiza Bodi ya Ushauri katika Hospitali Binafsi kuwachukulia hatua wamiliki wote wa hospitali za binafsi wanaokiuka taratibu zilizowekwa na kuwapa adhabu kali kwa mujibu wa sheria, ili wasirudie tena tabia hiyo wanazozifanya.

Aidha, kamati inaishauri wizara kuifanyia marekebisho Sheria ya Hospitali Binafsi ambayo ni Sheria Nam. 4 ya mwaka 1994, ambapo imeweka masharti yaliyopitwa na wakati kusababisha baadhi ya wamiliki kutokuwa na woga wa kuvunja masharti kutokana na adhabu hiyo kuwa ndogo na kutoendana na wakati wa sasa. Kamati inasisitiza kuwa suala la uwiano wa malipo ya leseni kwa Hospitali Binafsi liangaliwe upya na Bodi pamoja na wizara.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi inachukua hatua kuzisimamisha hospitali binafsi ambazo zinaenda kinyume na taratibu, hatua zinazochukuliwa ni pamoja na:-

1. Kuzifunga hospitali hizo hadi zitakapotekeleza maagizo waliopewa,
2. Kuzitolesha fidia hospitali hizo.

Aidha, upitiaji wa Sheria Nam. 4 mwaka 1994 ya Hospitali Binafsi upo katika hatua ya awali ya kufanyiwa marekebisho ili kuendana na mabadiliko ya wakati na mahitaji ya huduma za afya kwa wananchi. Pia uwiano wa malipo ya leseni, Bodi ya Ushauri wa Hospitali binafsi imeweka pendekezo la bei ya viwango vya leseni kulingana na hospitali husika na huduma inayotoa, hili halihitaji sheria ni muongozo ambao waziri anasaini na tayari juzi nimeshasaini muongozo wa kutoa bei mpya kwa hospitali zote binafsi pamoja na zile hospitali mnazokwenda Waheshimiwa Wawakilishi kwenda kuchuliwa viungo. Kwa hivyo, kutakuwa na bei mpya za usajili wake na hilo ni jambo la muongozo sio la sheria kwa sababu limo kwenye sheria tayari.

Agizo 36. Kamati, inaishauri Wizara ya Afya kuwasiliana na kukaa na Wizara ya Fedha na Mipango kutatuwa changamoto ya wamiliki wa Hospitali Binafsi ya kukatwa kodi kama ya wafanyabiashara, ili kutoivunja moyo sekta binafsi hususan wanaoingia kuwekeza katika sekta ya afya. Ambayo inasaidia sana serikali kufikia lengo la kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, masuala ya kodi yanaratibiwa na Wizara ya Fedha na *ZRB* chini ya sheria zao zilizowekwa. Wizara ya Afya haihusiki hata kidogo na mapato kupitia kodi hizi. Wizara itawasilisha maombi ya kamati ambayo Wizara ya Fedha pia tuko pamoja nao humu wameyasikia, ili kuhakikisha kwamba wanapata angalau unafuu kidogo hawa wanaojitolea kuwekeza katika sekta ya afya katika sekta binafsi.

Agizo 37. Mabaraza yapatiwe bajeti za fedha zinazokasimiwa katika matumizi wa afisi, ili kusaidia ufanisi wa kazi zao, ambazo ni muhimu katika maendeleo ya sekta ya afya kwa ujumla wake.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kiutaratibu Mabaraza yote yanatakiwa kujiendesha wenyewe hata hivyo, wizara imepokea ushauri ili kuona jambo hili litapatiwa ufumbuzi na fedha hizo kupatikana kwa wakati.

Agizo 38. Kamati, imesikitishwa sana na taarifa iliyopatiwa katika Baraza la Wauguzi na Wakunga kuwa taaluma hiyo hivi sasa inakosa wataalamu waliobobea watakaoweza kuwafundisha wanafunzi wa fani hii maadili ambayo yatasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza kesi za mara kwa mara zinazotokea katika hospitali zetu kutokana na ukosefu wa maadili ya kazi kwa wauguzi na wakunga wengi. Hivyo, kamati inachukua fursa hii kuishauri wizara kufanya juhudi za makusudi kusomesha wataalam wazalendo na kuwapangia maslahi mazuri, kwa lengo la watakapomaliza kusoma waje waendeleze gurudumu la fani hiyo, ambayo ni muhimu katika jamii yetu. Aidha, kamati inasisitiza upatikanaji wa vitendea kazi, wizara kulipatia Baraza la Wauguzi na Wakunga usafiri utakaorahisisha kazi zao.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Wizara kupitia wataalam wake wa fani ya Uuguzi na Ukunga na Baraza lake inatambulika ndani ya Wizara ya Afya hata hivyo kwa kushirikiana na *UNFPA* tayari tumepeleka walimu katika vyuo mbali mbali ikiwemo Tanzania Bara ili kuja kuziba pengo na kuendeleza maadili kwa wataalam wetu kwa fani hii.

Jengine ninalotaka kusema hapa Mhe. Naibu Spika, ni kwamba maadili ni mojawapo ya *subject* ama masomo yanayosomeshwa kupitia Chuo cha Afya Mbweni ambacho kipo chini ya Chuo Kikuu cha *SUZA.* Lakini hivi sasa ni muhimu zaidi kuimarisha usimamiaji wa maadili katika vituo vyetu kwa sababu wale wote wanaokuja wanakuwa wameshasoma *subject* hii ya maadili na wanakuwa wamepasi vizuri mitihani yao, lakini wanapofika hospitali wanakuwa tofauti, kwa hivyo hatua husika nazo zitachukuliwa katika eneo hili.

Agizo 39. Kamati, imelipokea suala la kutowekwa kwa stahiki za Mrajis wa Baraza la Tiba Asilia na Tiba Mbadala, kwa masikitiko makubwa na inaiomba wizara isichoke kulifuatilia suala hilo hadi litakapokamilika, ili stahiki ziweze kupatikana kwa mujibu wa sheria.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, suala la ofisi kwa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala linaendelea kufanyiwa kazi na wizara kwa Unguja na Pemba, na mara tu litakapokamilika basi taarifa husika itawasilishwa

.

Agizo 40. Kamati, inaliagiza Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala wakati wa kufanya ukaguzi katika maeneo yote kwa kushirikiana na vikosi vya ulinzi na usalama vya taifa, ili kujihakikishia usalama wao. Kutokana na hali hiyo, kamati inaiomba wizara kulisaidia Baraza kuliombea ulinzi wanapokwenda kukagua kutoka wizara inayohusika na vikosi vya SMZ kwa lengo la kukubaliana na hilo kwa ajili ya kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wa zoezi hilo.

Naomba Mhe. Naibu Spika, niseme baadhi ya hivi vituo hivi vya Tiba Mbadala na Tiba Asili nadhani nyie wenyewe Waheshimiwa mnajua vipo maeneo hatarishi, kwa hivyo wakienda wale wakaguzi wetu lazima waambatane na askari vyengine viko huko ndani huko kabisa.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala linashirikiana kwa karibu sana na Vikosi vya Ulinzi na hasa Jeshi la Polisi pamoja na Vikosi vya SMZ kwa kufanya ukaguzi wa maeneo hasa pale inapobidi. Aidha, Wizara imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kufanya vikao mbali mbali kwa ajili kujadili masuala yanayohusiana na Tiba Asili na Tiba Mbadala, na wao tunawashukuru Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ wamekuwa wakitupa mashirikiano ya karibu mno. Suala la kushirikisha Baraza la Manispaa pamoja na Halmashauri, wizara imelipokea kwani ni suala muhimu katika kulifanikisha suala hili la Tiba Asilia na Tiba Mbadala.

Mhe. Naibu Spika, **k**amati pia ilishauri wizara kukaa na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, ili wakubaliane kuhusiana na suala la baadhi wa wakunga wa jadi kusajiliwa ama kutosajiliwa. Kwa vile hawaruhusiwi kuzalisha hasa ikizingatiwa kuwa kuna baadhi ya vijiji pamoja na vituo vya afya havitoi huduma kwa muda wote wa masaa 24 na huduma hizo hotolewa na hao wakunga wa jadi.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, mamlaka yao ni kusajili waganga wa kienyeji pamoja na wakunga wa jadi. Sera ya Afya inasisitiza mama wajawazito kujifungulia katika vituo vya afya na kuwataka wakunga wa jadi kuwashauri mama hao kujifungulia katika vituo vya afya, ambako ni salama na ndiko hatari ya aina yoyote ikitokezea basi panakuwa na vifaa vya kuokoa maisha ya mama na mtoto. Hatushauri kina mama kujifungulia katika nyumba hizo za kienyeji na wataalam waliosomea masuala haya ya ukunga wapo na wanapatikana. Kwa upande wetu wa wizara tutaendelea kushirikiana kwa karibu sana na wakunga wote wa jadi ama wakunga wa kienyeji katika kufanikisha lengo hili na kuokoa maisha ya mama na mtoto.

Agizo jengine Mhe. Naibu Spika, kamati pia ilishauri wizara na serikali kwa ujumla kwa ujenzi wa jengo jipya la maabara, uzingatie na upatikanaji wa vifaa vya kazi vya kisasa pamoja na kuongeza vitengo vyengine vya maabara vyote vinavyohitajika kwa ajili ya kuepuka hasara mara mbili. Vile vile, kamati ilishauri kuongeza maslahi ya wafanyakazi kutokana na ukweli kuwa kwamba wataalam wa sekta mbali mbali ikiwemo ya sekta ya afya kuwasomesha kunahitaji gharama kubwa sana, ambapo serikali yetu huingia gharama hizo na baada ya kumaliza masomo kwa wataalam hao hukimbia kutokana na maslahi kuwa madogo. Hivyo, ili kuondoa tatizo hilo ni vyema maslahi ya wataalam hao yakazingatiwa kuyafanya yawe mazuri ili kuwabakisha hapa Zanzibar na wasende kwengineko.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Sera ya Afya kuanzia vituo daraja la pili hadi hospitali vinatakiwa kuwa na huduma za maabara. Ujenzi wa maabara moja kama kamati ilivyoshauri inaweza kuleta shida kwani wagonjwa kutoka sehemu tofauti na inabidi watafute huduma hizo katika maabara hiyo. Tunakiri kwamba kuna haja ya kuziimarisha maabara zetu zote kwani katika baadhi ya vituo vya afya na hata hospitali bado hadhi ya vipimo havipatikani kutokana na sababu tofauti. Hata hivyo, upatikanaji wa vipimo unategemea na daraja la kituo hicho au hospitali hiyo. Kwa upande wa maslahi ya wafanyakazi tayari haya yameshaimarishwa lakini kila fursa itakapopatikana, basi naamini serikali hii ina moyo mkunjufu sana na wafanyakazi sekta zote, pamoja na wafanyakazi wa afya maslahi haya yataendelea kuimarishwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati pia ilisikitishwa na taarifa kuwa kuna wafanyakazi wawili waliopelekwa kusomea utaalam wa matumizi ya mashine ya *DNA* ambao hadi hivi sasa mmoja hajarudi nchini na mwengine hajulikani alipo. Kutokana na kadhia hiyo, kamati inashauri kuwa wizara ifuatilie walipo wafanyakazi hao na ikibainika basi hatua stahiki zichukuliwe kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, wataalam wawili (2) kutoka katika kila Idara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kati yao mmoja alikwenda masomoni ni kweli *MUHAS* sio kama hajulikani alipo jina lake liko kwenye mabano (Sabra Seif Masoud) kwa mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya fani ya *Molecular Biology* na mwengine jina lake ambalo lipo pia kwenye mabano (Saide Abdalla Mbarak) yeye huyu alirudi alikwenda kufanya kozi ya *Molecular Medicine* Nje ya nchi na baada ya hapo kurudi. Wafanyakazi hao kimsingi ndio wanaopaswa kufanya uchunguzi wa *DNA Tests* kwa hapa Zanzibar. Hata hivyo, mfanyakazi mmoja aliyefanya kozi ya *Molecular Biology* huko *MUHAS* hakumaliza masomo yake na aliyakatisha njiani na aliandika barua rasmi kwa mujibu wa sheria ya utumishi kuacha kazi, mambo yalikuwa magumu kidogo.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia iliomba serikali kusawazisha stahiki za Mkemia Mkuu kwa kurejesha hadhi yake kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake.

Utekelezaji. Mhe. Naibu Spika, kuhusu stahiki za Mkemia Mkuu wa Serikali ni madai ya malipo yanayotokana na marekebisho ya muda mrefu sana ya mshahara wake na posho kutoka wakati huo alipokuwa mhadhiri wa Chuo Kikuu hadi kufikia hadhi ama Cheo cha Mkemia Mkuu wa Serikali. Madai hayo ni kuanzia huko alikotokea Wizara ya Elimu ambayo yalianzia mnamo mwezi wa Februari 2011 hadi tarehe ya marekebisho ya mishahara ya watumishi wa serikali yaliyotangazwa katika mwaka wa Oktoba 2013.

Madai hayo yameombwa na Wizara ya Afya kwa wizara inayohusika na Utumishi Umma Serikalini. Hadi sasa ni shilingi milioni tano ndizo zilizolipwa kati ya shilingi milioni kumi na nne zinazodaiwa, hizi tulitakiwa sisi Wizara ya Afya, tulipe moja kwa moja kwa mujibu wa sheria hiyo juu ya stahiki zake. Hizo nyengine zinalipwa na Utumishi wa Umma moja kwa moja.

Kuhusu stahiki nyengine kama vile nyumba, Wizara ya Afya ilitoa ufafanuzi kuwa kwa hivi sasa haina nyumba za kumpatia Mkemia Mkuu wa Serikali, lakini posho la nyumba analipwa kama vile ambavyo watumishi wengine wanahusika katika ngazi zao husika wanavyolipwa katika Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na Kamati nzima Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, ambaye naye katika historia ya Zanzibar kishawahi kuwa na yeye siku moja katika nafasi hii, niliyosimama mimi hapa, kwa kutupatia miongozo busara, hehima zake pamoja na wajumbe wake wote wa Kamati, pamoja ndugu zetu watendaji wa Baraza la Wawakilishi, kupitia meza ya Katibu wetu wa Kamati ambaye yupo hapa leo amekaa kwa kutupa mashirikiano. *(Makofi)*

Kwa kweli, mambo haya si rahisi mambo haya ni mazito, magumu yana dhima pia kubwa kwa Mwenyezi Mungu, lakini tumekwenda nayo vizuri tumefanya ziara vizuri, tumeona mambo mengi na mengine mazito, mengine makubwa mengine yanahitaji muda zaidi, mengine yanahitaji fedha nyingi zaidi. *(Makofi)*

Kwa hayo, Mhe. Naibu Spika naomba niendelee kuwashukuru wao pamoja na wewe kwa kutupatia nafasi hii, ya kutoa leo ufafanuzi wa hoja zote zilizowasilishwa kwetu. Vile vile, naomba niahidi mbele yako Mhe. Naiu Spika kwamba Wizara ya Afya itaendelea kupokea na kutekeleza maagizo na ushauri mbali mbali, utakaotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wako wote wa Baraza hili Tukufu. Sambamba na hilo tunatoa ahadi kwamba tutazidisha juhudi zetu na kasi ya utekelezaji katika majukumu katika sekta hii, kwani ni sekta ambayo inahitaji nguvu kubwa sana ya kupatiwa, ili tuweze kukidhi haja za mahitaji ya wananchi wetu wote.

Kwa hayo, machache naomba niendelee kukushukuru wewe Mhe. Naibu Spika. Kwa heshima na taadhima naomba sasa kutoa hoja ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Afya, nakushukuru na tunatarajia kwamba Waheshimiwa Wajumbe, mtakuja mapema leo jioni saa 11.00. Kwa hiyo, mpaka sasa ninao wachagiaji wawili kwa wizara hii, ni matarajio yangu kwamba tutapata wachagiaji zaidi ya hawa, na Waheshimiwa wenyewe ni Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Shehe Hamad Mattar. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe niliowataja waje mapema, ili waanze kuchangia kwa wizara hii, itakuwa Mwenyekiti kwanza halafu baadaye atachangia wao.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kusitisha kikao naomba nitoe tangazo moja ambalo lilitoka kwa Mhe. Ali Salum Haji (Mnadhim wa Chama cha Mapinduzi) anaomba kwamba baada ya kikao hichi kuakhirishwa Wajumbe wa Chama cha Mapinduzi tukutane kwenye ukumbi wa juu.

Baada ya kusema hayo nasitisha kikao hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.17 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi (Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii): Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii naomba kusoma Hotuba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Kuhusu Utekelezaji wa Kamati wa Wizara ya Afya.

Utangulizi

Mhe. Mwenyekiti**,** nachukuwa fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujalia afya njema na uzima na kuweza kutukutanisha tena katika ukumbi huu kutekeleza makujukumu ya kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, nachukuwa fursa hii kukushukuru kwa dhati Mhe. Mwenyekiti kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwasilisha kwa muhtasari maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati yangu inaipongeza sana Wizara kwa juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuimarisha sekta ya Afya na hatua kadhaa za maendeleo zimefikiwa chini ya Uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein.

Naomba kuchukuwa fursa hii kwa niaba ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kumpongeza kwa dhati kwa kazi kubwa anayofanya husasani katika sekta hii ya afya kwa kuimarisha miundombinu ya Afya, Kuimarisha maslahi ya Watendaji wa Wizara ya Afya na upatikanaji wa huduma za afya hasa dawa katika Hospitali na vituo vya afya nchini kote Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati yangu inafanyakazi kwa mashirikiano na wasaidizi wakuu wa Mhe. Rais katika sekta ya Afya na naomba hapa niwapongeze Waziri wa Afya Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Harous Suleiman Said.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati yangu inatambua juhudi kubwa zinazochukuliwa na watendaji wa Wizara ya Afya katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya kiafya, na kwa upekee naomba niwapongeze watendaji wote wa Sekta ya Afya na kwa dhati kabisa nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Asha Abdalla na Naibu Katibu Mkuu wake Ndugu Halima Maulid pamoja na Wakurugenzi wote, Wakuu wa Taasisi na Vitengo, Afisa Mdhamini Pemba pamoja na Mabaraza na Bodi zote zilizo chini ya Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti**,** watendaji wote niliowataja pamoja na viongozi wao wamefanyakazi kwa mashirikiano makubwa na Kamati kuhakikisha maagizo ya Kamati yaliyotolewa yanatekelezwa na ripoti ya utekelezaji wake kuwasilishwa mbele ya Kamati ya Baraza hii leo.

Mhe. Mwenyekiti**,** naomba kuwashukuru Waheshimiwa wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, kwa stamina na uadilifu wao mkubwa katika kazi za Kamati. Hakika michango yao madhubuti imesaidia sana masuala yaliyotajwa katika ripoti hii. Naomba niwataje majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame	Mwenyekiti
2. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Mjumbe
4. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	Mjumbe
5. Mhe. Hidaya Ali Makame	Mjumbe
6. Mhe. Makame Said Juma	Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Mjumbe
8. Ndg. Aziza Wazir Kheir	Katibu
9. Ndg. Khamis Hamad Haji	Katibu

Mhe. Mwenyekiti**,** Mwezi Februari mwaka 2017 Kamati ya Ustawi wa Jamii imetoa ripoti yake kwa Wizara inazosimamia ikiwemo Wizara ya Afya yakiwemo maagizo ambayo yametokana na kazi kubwa iliyofanywa na Kamati. Kamati inapongeza sana Serikali kwa kufanikisha ujenzi na ufunguzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee pamoja na jengo jipya la Wazazi na watoto katika Hospitali ya Mnazimmoja.

Mhe. Mwenyekiti Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati

Kamati ya Ustawi wa Jamii imekaa na Wizara ya Afya na kupitia kwa pamoja utekelezaji wa Maagizo yote ya Kamati, na kwa ujumla Kamati imeridhika na majibu ya Maagizo hayo. Hata hivyo, lazima nikiri kuwa yapo baadhi yametekelezwa kwa ufanisi mkubwa kama ambavyo Mhe. Waziri alivyowasilisha katika hotuba yake muda mfupi uliopita.

Mhe. Mwenyekiti**,** Vile vile yapo maagizo ambayo yanahitaji fedha zaidi katika bajeti ya mwaka, zipo changamoto ambazo Wizara yenyewe lazima ijipange vizuri kuzikabili ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu watendaji wachache ambao wanakwenda kinyume na maadili ya kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti**,** Watendaji hawa ndio wamekuwa wakiipa jina baya sekta ya afya hasa Hospitali ya Mnazimmoja. Hivi Daktari Mkuu anaona uzito gani kumchukulia hatua Daktari asiyelala zamu usiku au Muuguzi Mkuu kwa nini anachelewa kumkata siku za mapumziko Muuguzi, Mkunga au Odali ambaye hafiki kazini kwa wakati au wengine kutumia lugha chafu kwa wangonjwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati ya Ustawi wa Jamii ina maoni kadhaa ya ziada katika maeneo mbali mbali yanayohusu utekelezaji wa maagizo yake kwa Wizara ya Afya kama ifuatavyo:-

Upungufu wa Watendaji Katika Sekta ya Afya

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati ya Ustawi wa Jamii imetoa agizo la kupatiwa ufumbuzi tatizo la upungufu wa watendaji katika Sekta ya Afya hasa madaktari, Wauguzi, Wakunga na Maodali pamoja na wataalamu mbali mbali wa maabara, mionzi n.k ambao Kamati imebaini upungufu mkubwa katika Hospitali na vituo vya Afya.

Mhe. Mwenyekiti**,** Wizara imefafanuwa vizuri namna ilivyotekeleza utatuzi wa changamoto hiyo na Kamati ya Ustawi wa Jamii inapongeza hatua hizo, hata hivyo, Kamati yangu inaiomba sana Serikali kupitia Wizara inayosimamia masuala ya utumishi wa Umma kuona uzito wa mapungufu hayo ya wafanyakazi hasa Madaktari, Wauguzi, Wakunga na Maodali katika Hospitali na vituo vya afya.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kada za afya ni mbali mbali na kila kada ina umuhimu wake katika kuiendesha vizuri Hospitali. Huwezi kuwaajiri wauguzi ukawaacha Maodali au huwezi kuajiri Madaktari ukawaacha Wafamasia. Suala la kupata uwiano wakati wa uajiri katika sekta ya Afya ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati ya Ustawi wa Jamii katika ziara zake mbali mbali za Unguja na Pemba imeona juhudi kubwa za Serikali katika kuimarisha majengo ya Hospitali na vituo vya Afya hasa vile vya maeneo ya vijijini ambavyo vipo katika hali nzuri na vingi vikiwa na vifaa vya kisasa kabisa. Tatizo kubwa ni upungufu wa wataalamu wa kufanyakazi ingawa baadhi ya vifaa vipo katika vituo hivyo. Kamati inashauri Serikali kuzingatia kwa makini uhaba huu wa wataalamu na kuchukuwa hatua za dharura za kuwajiri wafanyakazi wapya.

Mhe. Mwenyekiti**,** bado Kamati ya Ustawi wa Jamii imekuwa ikihoji mara nyingi namna ya ujazwaji wa nafasi za watumshi wa sekta ya afya ambao wamestaafu na wengine kufariki. Baraza lako litakumbuka kuwa wakati Mhe.Waziri wa Afya akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara yake ya mwaka 2016/2017 alisema katika ukurasa wa 58-59 kuwa jumla ya wafanyakazi 107 wamestaafu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma (Unguja 48 na Pemba 59) na alieleza kuwa wafanyakazi 15 (Unguja 7 na Pemba 8) wemefariki dunia.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa maelezo hayo ya Mhe. Waziri ni wazi kuwa nafasi hizo zipo wazi na zinahitaji kujazwa kwa kuwa mishahara yake inakuwa ipo, hivyo Kamati inashauri kuwa inapotokea upungufu wa watendaji katika sekta ya afya unaotokana na aidha kustaafu au kufariki wafanyakazi basi nafasi hizo zijazwe mara moja kwa vile hakuhitaji gharama nyengine za ziada kujaza na nafasi hizo. Uzuri ni kwamba mitaani watu wenye sifa kujaza nafasi hizo wapo wengi na na baada ya kusubiri ajira kwa muda mrefu mwishowe wanakimbia Tanzania bara kutafuta ajira.

Wafanyakazi wa Afya Kutokuwa Tayari Kufanyakazi Pemba

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa upekee kabisa naomba kulielezea suala la kuhama wafanyakazi wataalamu wanaopelekwa Pemba. Ni moja ya sababu zinazopelekea uhaba wa wafanyakazi Pemba, watendaji wanaopelekwa kufanyakazi Pemba wakifika tu wanafanya mipango ya kurudi Unguja. Vile vile, wapo baadhi ya watendaji wanaomba nafasi za kufanyakazi Pemba na baada ya kupata ajira, muda mfupi tu wanafanya mipango ya kuomba uhamisho na kuja Unguja kwasababu mbali mbali ikiwemo suala la kuwafuata waume zao.

Mhe. Mwenyekiti**,** Pamoja na juhudi za Wizara kukabiliana na changamoto hii, Kamati inashauri sana kuwa utaratibu wa uhamisho wa wafanyakazi kwenda Pemba ahusike Katibu Mkuu tu badala ya maafisa wengine wa Wizara kusaini barua za uhamisho kwa niaba ya Katibu Mkuu.

Vile vile Wizara iweke utaratibu mzuri wa kuzunguka *(rotation)* ili nao wafanyakazi waliokubali kufanya kazi Pemba kutoka Unguja waweze kurejea baada ya miaka miwili au mitatu.

Kuongezwa Bajeti ya Wizara ya Afya

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati yangu imebaini kuwa utekelezaji wa baadhi ya maagizo umeathiriwa kiasi na changamoto ya ufinyu wa bajeti, licha ya nia ya dhati ya Wizara kutaka kutekeleza kama ilivyoagizwa. Hata hivyo, tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuongeza bajeti hiyo ambapo kama alivyoeleza Mhe. Waziri kuwa bajeti ya Wizara ya Afya imeongezwa kutoka Shilingi Bilioni 44.2 kutoka mwaka 2016/2017 na kufikia shilingi bilioni 58.7 kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, Huduma Za Hospitali Na Vituo Vya Afya

Utekelezaji wa maagizo mbali mbali yanayohusu huduma za matibabu ya wananchi katika Hospitali zetu na vituo vya afya unaridhisha kwa kiasi ya wananchi kupata huduma na dawa.

Hata hivyo, bado kuna kazi kubwa inatakiwa kufanyika katika kuimarisha zaidi utoaji huo wa huduma ili uwe endelevu hasa katika suala la vipimo na upatikanaji wa dawa. Bado yapo malalamiko kutoka kwa wananchi hasa katika Hospitali ya Mnazimmoja ambayo kwa mujibu wa sheria namba 3 ya mwaka 2016 hivi sasa ndiyo Hospitali ya Rufaa na ndiyo kimbilio la wananchi wetu wengi katika kupata huduma za afya.

Mhe. Mwenyekiti**,** pamoja na mafaniko makubwa yaliyopatikana uimarishaji wa majengo mapya, uanzishwaji wa huduma mpya za saratani na usafishaji figo, kuimarisha muundo wa Hospitali baada ya sheria mpya, lakini Hospitali ya Mnazimmoja inazidiwa na wingi wa wagonjwa ambao hauendani na ongezeko la wataalamu na vifaa tiba vilivyopo, Kamati inashauri katika kuimarisha huduma za Hospitali hiyo kuzingatia changamoto hii.

Mhe. Mwenyekiti**,** Wananchi wameipokea kwa furaha hatua ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutiliana saini hivi karibuni na Mfuko wa Kuwait *(Kuwait Fund)* kuipatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mkopo wa Dola za Kimarekani Milioni 13.6 kuimarisha Hospitali ya Mnazimmoja pamoja na vituo vyengine vya afya.

Mhe. Mwenyekiti**,** njia nyengine ambayo kamati tunapendekeza na kushauri ifanyike ni kuziimarisha Hospitali za Wilaya kama vile Kivunge, Makunduchi, Wete, Chake Chake na Micheweni kwa kuimarisha miundombinu, kuongeza wataalamu na vifaa tiba ili kuzipunguzia mzigo Hospitali zetu kuu za Mnazimmoja na ile ya Abdalla Mzee Pemba.

Mhe. Mwenyekiti**,** sambamba na hilo, Kamati ya Ustawi wa Jamii inashauri sana kuimarishwa vituo vya Afya vya msingi ambavyo hivi sasa vimegatuliwa na vipo chini ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ. Endapo vituo hivi vitaweza kumudu kutoa huduma za msingi kwa wananchi vitasaidia sana kuzipunguzia mzigo Hospitali za Wilaya na Hospitali zetu Kuu. Kamati ya Ustawi imetembelea vituo hivi vingi kote Unguja na Pemba na kuona kuwa vimejengwa vizuri na imewekewa vifaa vya kufanyiakazi,

changamoto kubwa inavyovikabili ni upatikanaji wa wataalamu wa kufanyakazi kama nilivyoeleza hapo juu.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa ujumla taasisi ya Hospitali ya Mnazi mmoja ambayo inajumuisha Hospitali ya Wazazi ya Mwembeladu na Kidongo chekundu zinahitaji kupatiwa utaratibu maalumu na endelevu wa kupatiwa fedha za matumizi mengineyo *(O.C)* kwa vile Hospitali hizi zinatoa huduma kwa saa ishirini na nne. Yapo mambo yanaonekana madogo madogo lakini yanarudisha nyuma ufanisi wa utendaji kazi kwa mfano suala la usafi, kuharibika kwa vifaa tiba mara kwa mara na kuchakaa kwa baadhi ya sehemu za majengo.

Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba

Mhe. Mwenyekiti**,** Hospitali nyingi na vituo vyetu vya afya vinakabiliwa na uhaba wa dawa muhimu na vifaa vya kisasa vya kuchunguza na kutibu maradhi. Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kuchukuwa hatua za kuhakikisha upatikanaji wa dawa unakuwa endelevu na hivi sasa tatizo hilo limepungua kwa kiasi kikubwa, hata hivyo Kamati inashauri juhudi hizo ziongezwe ili dawa zinapomalizika vituoni isichukuwe muda mrefu ziwe zimeongezwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kwa upande wa vifaa tiba bado kuna changamoto kwa baadhi ya vituo kutumia vifaa vya zamani. Kamati yangu ilibaini kuwa Hospitali ya Kivunge na Chake Chake hazina mashine ya kisasa ya kusafisha picha za *X-Ray (automatic processor)* ambayo inarahisisha kufanyika uchunguzi kwa muda mfupi. Vipo baadhi ya vituo ambavyo havina hata mashine za kupimia presha na uchunguzi wa kawaida. Kamati yetu imeagiza Wizara kuchukuwa hatua za dharura kupitia vituo hivyo na kubaini changamoto hizo kwa lengo la kuzitatuwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** Hospitali ya Rufaa ya Mnazimmoja mara kwa mara inakumbwa na tatizo la kuharibika vifaa muhimu vya uchunguzi wa maradhi kama vile *CT Scan* na *MRI*. Kamati ya Ustawi wa Jamii inashauri Wizara katika kuendelea utekelezaji wa maagizo yanayosubiri upatikanaji wa fedha, basi izingatie kuwa na mpango wa kuzuwia maharibiko ya vifaa hivyo kama vile kuvikaguwa na kuvifanyia *"service"* mara kwa mara kama inavyopendekezwa na mafundi pamoja na kuweka utaratibu mzuri wa kuvitumia ili visizidiwe na kazi.

Mhe. Mwenyekiti**,** suala la upatikanaji wa mashine ya uchunguzi wa vinasaba (*DNA*) lina umuhimu wa kipekee katika upatikanaji wa ushahidi katika masuala ya jinai na kwa umuhimu huo utekelezaji wa sera ya afya hautatimia kama kifaa hiki hakijapatikana. Umuhimu huo umetajwa kwenye Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2015, katika ukurasa wa 174-175 na naomba ninukuu.

"katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2015-2020), Chama cha Mapinduzi kitailekeza SMZ kuiendeleza zaidi sekta ya afya kwa kutekeleza yafuatayo…(b) kuendelea kuifanya Hospitali ya Mnazimmoja kuwa ya Rufaa kwa kuongeza huduma za matibabu ya saratani na kuimarisha huduma za uchunguzi na ununuzi wa vifaa kama *MRI, DNA*…" mwisho wa kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wa Baraza lako wameshawahi kujadili kwa kirefu kuhusu umuhimu wa upatikanaji wa *DNA* ili kusaidia katika uchunguzi wa kesi za udhalilishaji ambazo zinaonekana kuongezeka kila kukicha.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo pamoja na Kamati ya Ustawi wa Jamii kuelekeza wizara kutekeleza upatikanaji wa kifaa hicho, utekelezaji wake bado haujafanyika kwa vile kifaa hicho kina gharama kubwa sana. Pamoja na hayo, kamati yangu bado inashauri wizara kuzingatia umuhimu wa kuwepo kifaa hicho kama ilivyotajwa katika ilani ya CCM na kama Wajumbe wa Baraza hili walivyoshauri katika vikao vilivyopita, hasa wajumbe wanawake ambao wameguswa sana na kesi za udhalilishaji wa watoto na wanawake.

HUDUMA ZA KINGA

Mhe. Mwenyekiti, huduma za kinga ni muhimu katika kudhibiti kuibuka kwa maradhi, kinga ni bora kuliko tiba. Nchi yetu kwa muda mrefu imekuwa inakabiliwa na janga la maradhi ya kipindupindu kila wakati wa vipindi vya mvua. Hali hii mbali na kuisababishia hasara serikali ya kukabiliana nayo, lakini pia inaleta athari mbaya kwenye maisha ya watu kwa vifo, karantini ambayo husitisha shughuli za kiuchumi za wananchi wengi. Kamati ya Ustawi wa Jamii imeona juhudi za wizara katika kudhibiti mripuko na juhudi hizo zinaanza kuzaa matunda kwa baadhi ya maeneo kama vile Kojani ambako kwa misimu miwili ya mvua hakukuwa na mripuko wa maradhi ya kipindupindu.

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio hayo yamekuja kwa vile wizara imesimama kidete kuchukua hatua za kukinga kwa kuelimisha wananchi kuchimba na kutumia vyoo, kunawa mikono kila unapotoka chooni, kuacha kujenga kwenye vyanzo vya maji na kunawa mikono kwa sabuni kabla ya kula. Pamoja na mafanikio hayo ya kupongezwa bado kuna kazi kubwa inahitajika kufanyika hasa katika Manispaa ya Magharibi “A” na Magharibi “B” ambako hivi sasa idadi kubwa ya wagonjwa wa kipindupindu inapatikana huko.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaendelea kusisitiza wizara kuongeza kasi ya utoaji wa elimu ya kinga pamoja na kuchukuwa hatua za kudhibiti mapema visababishi vyote vya mripuko wa maradhi ya kipindupindu kama vile wauzaji wa vyakula wasiozingatia usafi, nyumba zisizokuwa na vyoo na umwagaji wa maji machafu ya chooni katika mitaro ya maji machafu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha usalama wa afya zetu na kukinga athari ya vyakula na dawa tunazotumia, kamati inapongeza Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (*ZFDA*) kwa kazi wanayofanya ya kukaguwa na kubaini vyakula na dawa ambazo zimepitwa na wakati na hazifai kwa matumizi ya binaadamu. Kamati yangu inatoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na *ZFDA* kwa kutoa taarifa za baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu ambao wanaingiza na kusambaza vyakula na dawa ambazo zimeshapita muda wa matumizi.

Kwa kufanya hivyo sio tu tutakuwa tumenusuru afya zetu lakini pia tutaepusha nchi yetu kutumika kuwa jaa la vitu vilivyokwisha muda wake.

Mhe. Mwenyekiti, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wake. Katika hatua hiyo, Kamati ya Ustawi wa Jamii inapongeza juhudi za serikali kuimarisha maabara hii muhimu.

Kamati inaendelea kukumbusha tu kuhusu hadhi ya Mkemia Mkuu ambayo imetajwa kwenye sheria, bado suala la maslahi ya Mkemia Mkuu halijapatiwa ufumbuzi na kamati yangu inachukuwa fursa hii kuitaka Wizara inayosimamia Utumishi wa Umma kuchukuwa hatua kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ili maslahi ya Mkemia Mkuu na madai yake yarekebishwe kwa vile suala hilo lishakuwa la muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo Mkurugenzi wa Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala tumeona kuwa hadhi yake ya Ukurugenzi kimaslahi haipo sawa sawa na tumeagiza Wizara ya Afya wakae na wizara inayosimamia Utumishi wa Umma kulitatuwa tatizo hilo. Kamati inashauri tena hatua zichukuliwe kwa kuwa hii ni haki ya mtu. Kamati pia imeshauri Baraza hili litafutiwe Ofisi za Kudumu Unguja na Pemba kwa vile huduma za tiba asili zimeongezeka kwa kasi nchini kwetu na Baraza hili lina kazi kubwa ya kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma hizo za tiba asili na mbadala.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuhitimisha hotuba yangu naomba niseme kuwa kwa ujumla Wizara ya Afya imetekeleza maagizo ya kamati, yapo maeneo ambayo yapo kwenye uwezo wao wamechukuwa hatua kwa kiwango fulani. Lakini kamati inaagiza tena suala la usimamizi katika utendaji kazi lazima litazamwe kwa undani zaidi. Yapo mengine ambayo watahitaji msaada kutoka Serikali Kuu hasa saula la kuongeza bajeti ya *OC* ya wizara. Tunashauri na kuikumbusha serikali kuyachukuwa ili kuhakikisha kuwa changamoto za msingi zinazoikabili sekta ya afya zinatatuliwa ili wananchi wapate huduma bora na endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, nasisitiza tena kuwa maagizo ambayo wizara inaendelea kuyatekeleza kwa awamu mbali mbali kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha na vifaa, kamati yangu itaendelea kuyafuatilia na kushirikiana na Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa mafanikio yanapatikana.

Mwisho kabisa naomba kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza na nawaomba waendelee kuchangia kwa kushauri maeneo mbali mbali ambayo pengine kamati hatukufika kutokana na uchache wa muda tuliopangiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza haya nakushukuru tena kwa kunipa wasaa huu, naomba kuwasilisha na naungamkono hoja asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Tatu Mohammed Ussi kwa niaba ya Mwenyekiti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii. Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea sasa mchangiaji wetu wa mwanzo naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid atafuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajitayarishe.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwanza napenda kuchukua fursa hii adhimu kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya upendeleo ya kwanza, lakini pia sina budi kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa uwezo wake mkubwa katika utendaji na pia jinsi alivyoonesha upenzi wake mkubwa kwa Wazanzibari, na namna gani Rais wetu huyu alivyokuwa anathamini afya za wananchi wake. Ni ukweli usiopingika kwamba Rais anafanya kazi kwa nguvu zake na bidii yake na maarifa makubwa na anaweza kuwashauri watendaji wa wizara. Mimi naamini kwamba Rais anafanya hivi kwa sababu yeye mwenyewe alitokea huko na anayaona haya na ndio kila wakati akaweza kuishauri na kuisimamia vizuri wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya kwa uwezo wake na bidii yake ya kazi anayoionesha. Ni ukweli usiopingika kama waziri anajitahidi kadiri ya uwezo wake yaliyobakia ni mapungufu ya kibinadamu haya yaende ndio mambo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini timu aliyonayo ni timu nzuri iliyokuwa imemzunguka, lakini kwenye mazuri mengi na mabaya huwa yapo. Kwa hiyo, tunasifu kidogo, tunakosoa kidogo na tunaelekeza ili mambo yaende mbele lengo letu ni kuona kwamba wananchi wa Zanzibar wanapata huduma, wanapata manufaa, wanafarijika kwa kutumia matunda ya Mapinduzi ya 1964.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya mimi leo nina machache tu ambayo nitayazungumza zungumza kidogo, nitapiga piga juu juu kwa sababu naona mengi yameelezwa. Lakini na mimi kwa sababu ninayo kidogo niliyoyaona naomba niyaeleze, twende moja kwa moja ukurasa wa 4. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 4 kwenye kesi pale tutazungumza suala zilipo hizo kesi. Mimi nilitaka kujua ni makosa gani ambayo watumishi hao wamehusishwa nayo, maana yake kuna anasema kanuni za maadili ya wafanyakazi ni suala muhimu na wizara tayari imekaa tayari na kujadiliana na bodi ya wataalamu na kuona jinsi gani wasimamizi wa uchukuaji hatua kwa wale wote waliokosea.

Mimi Mhe. Waziri nilitaka nijue kwa sababu hapa kamati walizungumza kwamba suala la nidhamu katika uwajibikaji ni kitu cha muhimu sana, uwajibikaji ndio unaoleta upendo. Kwanza tunaanza upendo ikisha tunakuja uwajibikaji, bila ya kuwa na upendo huwezi kuwa na uwajibikaji. Sasa je, nilitaka nijue hilo na nilitaka nijue kwa sababu wizara imeweka kanuni, tukirudi ukurasa wa 3 inasema wizara imeweka kanuni za wafanyakazi wa hospitali na vituo vya afya na kutoa taarifa za malalamiko ya wananchi, haya ni mambo muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona tukienda katika vituo vyetu vya afya baadhi, mimi nasema baadhi sisemi wote. Nasema baadhi ya watumishi wetu wamekuwa si wenye kauli nzuri kwa wagonjwa kwa watu wanaowahudumia. Mtu anapokwenda hospitali hata iwe ni mwizi basi kenda pale kwa kutafuta shufaa ya mambo yaliyomkuta, wajibu pale apate kauli nzuri. Akute mtu anamuhudumia anampa kauli nzuri, ile kauli nzuri kwanza inatosha kuwa ni huduma ya mwanzo na mtu kujihisi kwamba yeye anastahiki kupata ile huduma. Sasa inapotokea kwamba mtumishi au mhudumu wa ile hospitali au kituo cha afya mgonjwa kafika pale anampa kauli zisizoridhisha kwa kweli ni jambo la kusonesha sana.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia hayo maneno yake ya kutengeneza hizo kanuni aniulize je wako angalau baadhi ya wafanyakazi wetu walioguswa na mambo haya na kanuni zikafanya kazi na ni wangapi ambao sasa hivi tushawafanyia haya. Maana yake hatusemi tuwafukuze kazi, lakini angalau wajue kwamba aah! huyu mzee kidogo kawa mkali kwa hiyo tukikosea hapa tunapata kidogo namna hii, tunapata kuwajibika kidogo. Hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, la pili katika ukurasa wa 5 nilikuwa napenda kwenye agizo Nam.4 anasema suala la ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Abdalla Mzee. Mhe. Mwenyekiti, suala hili la ujenzi wa nyumba za madaktari mimi naomba na naishauri wizara pamoja na maelezo mazuri mliyoyazungumza humu, lakini ni jambo la muhimu na uzito wa aina yake. Nazungumza hivi kwa sababu gani? Madaktari wetu wanaofanya kazi kwenye Hospitali ya Abdalla Mzee wengi hawakai Mkoani sijui kama wameanza sina hakika ya hili maana sitaki niseme jambo ikisha uje unisute, lakini ninavyojua huko nyuma walikuwa wanatoka Mkoani wengine wanakaa Wete, wengine wanakaa Chake-Chake.

Sasa Mhe. Waziri wewe huoni kama ni kujibebesha mzigo kwa sababu unatumia pesa nyingi, unakodi nyumba, unawakodia gari za usafiri wakifika pale wamechoka uwezo wa kufanya kazi unapungua. Sasa nilitaka nijue lini suala hili tunalianzia na lini kukamilika kwake, ingawa mmeshanieleza lakini ningependa nipate maelezo zaidi ili roho yangu na mimi itulie nipate kujua. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa tukimbilie ukurasa wa 7, agizo Nam.9. Nasema kamati imeshauri kufanya juhudi za makusudi kutafuta wafadhili watakaosaidia kujenga nyumba za madaktari katika vituo vya afya vilivyopo nchini kwa lengo la kuondoa tatizo la makaazi kwa madaktari pamoja kuwaondoshea usumbufu wanaopata hivi sasa ambapo baadhi yao hulazimika kusafiri masafa marefu kufuata huduma kwenye vituo hivyo. Ni kweli kamati imeliona hili, hili ni jambo la kutiliwa maanani, kamati imefanya kazi ukienda kwenye Jimbo langu la Konde tatizo hilo lipo, Msuka hakuna nyumba ya daktari, Mkia wa Ng'ombe Mhe. Mwenyekiti, ukiachia tatizo la nyumba lakini pale kuna tatizo la usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, Mkia wa Ng'ombe ukiachia mbali tatizo la makaazi lakini kuna tatizo la usafiri inapotokea kesi ya dharura pale maji ya bahari makubwa yamejaa na yamekata jangwa, imetokea dharura mtu hawezi kuvuka kutoka Mkia wa Ng'ombe akafika Konde au akapelekwa Hospitali ya Rufaa ya Micheweni au hospitali ya Wete. Ningetaka nijue tutafanyaje kuwasaidia watu wanaoishi Mkia wa Ng'ombe ili kuwaondolea tatizo hilo. Naiomba wizara inisaidie mimi, iwasaidie watu wetu ili na wao kama nilivyosema wafaidi matunda ya Mapinduzi ya 1964 ambayo Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein anayapigia mbio na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inaelekeza hivyo kwamba kupata huduma za elimu na afya ni haki ya msingi kwa kila Mzanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia tulizungumzia suala la ujenzi wa nyumba. Mimi Mheshimiwa leo nakupongeza kwa ripoti hii lakini ingekuja vibaya kidogo ningegeuza macho leo. Sisi pamoja na jumuiya yangu wewe unafahamu namna gani ambavyo mimi na jumuiya yangu tulipigania mpaka kupata ule mradi wa *theatre.* Leo ni jambo la kusikitisha wizara umejitahidi sikati umejitahidi, lakini *theatre* ile ya Micheweni haijaweza kufanya kazi tunasema tuichangie. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, ombi langu na jambo hili nalijua kwamba vijana wetu wa Wete Afisa Mdhamini na timu yake wanajitahidi kufanya ile kazi, lakini wanajibana kwenye *OC* unapompa mtu jukumu la kufanya kazi kwa kutumia *OC* ina maana akate upande mwengine atengeneze mwengine. Naiomba sana wizara umesema kama bajeti umeongezewa wape fedha wale wamalize, wapeni fedha wamalize ili na wao kama hawakutekeleza tuje tuwaulize kwa nini mlipewa pesa ya serikali mmeshindwa kuyafanya yale. Lakini kwa leo mimi naiona bidii wanayoifanya wale vijana, mimi nilikuwa msemaji mkubwa wewe unafahamu, lakini leo siwezi kusema kwa sababu naona bidii yao na nguvu yao inakwenda, wamefunga umeme upande mmoja tuwawezeshe. Nakuomba tuwawezeshe kufanya yale ili maslahi yapatikane.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na tatizo la vitendea kazi limezungumzwa, mimi nashauri sana kama kamati kwa upande wa Unguja na Pemba tumeona hili ni tatizo. Naiomba sana wizara ifanye kila hali inavyowezekana, Waswahili wanasema “kata pua uunge wajihi”. Tunapotaka kuongeza mchele au tunapotaka kupika wali wanasema ukiongeza maji uongeze na mchele ndio tupate wali, kama hatukuongeza mchele tukiongeza maji matupu hauwi wali tena unakuwa uji sasa.

Mheshimiwa mimi namuomba sana tuwaongezee tuwapelekee vitendeakazi watu wetu, tujitahidi kusogeza mbele huduma kwa kuongeza vitendea kazi. Tutafute vitendea kazi tuwape ili kama nilivyosema wanaposhindwa sasa tuwalaumu kwamba mmeshindwa.

Pia nilikuwa nina tatizo linanipa shida kidogo pale Chake Chake kuhusiana na ukarabati mkubwa na tatizo la vyoo pale, ingawa limetajwa kwenye Hospitali ya Chake Chake. Hospitali ile sisi ndio kimbilio letu, kwa sababu watu wengi wanakwenda Mkoani baada ya kushindikana Wete na Chake Chake. Naomba sana Mhe. Waziri suala hili la kuiweka kwenye hali nzuri Hospitali ya Chake Chake kwa upande wa Pemba ni jambo la kuliangalia sana, tujitahidini na Mwenyezi Mungu atusaidie, tuwekeni nia moja tumuweke Mwenyezi Mungu mbele tufanikishe mambo haya.

Hospitali ya Chake Chake Mhe. Waziri namuomba uiangalie kwa jicho la huruma, pamoja na mambo mengine lakini aiangalie kwa jicho la huruma, tusisubiri mpaka tukaja tukaharibikiwa. Wazee wa kwetu mimi nilikuwa nina babu yangu mmoja alikuwa na methali yake akisema "Kimbia ugwe kabla hujaona ng'ombe". Wapemba wanaijua hiyo methali, wanasema "kimbia ugwe kabla hujaona ng'ombe", ng'ombe asije akatufika. Kwa hiyo, mimi naomba tena naomba sana kwamba hospitali ya Chake Chake iangaliwe sana, iwekewe vitendea kazi, iwekewe *instruments* zote ili kila kitu kinachohitajika pale kiwepo sambamba na wafanyakazi.

Mheshimiwa jambo hili litatuweka katika pahala pazuri tukilikosea tutaharibikiwa. Nimefurahi kuona kwa sababu nilikwenda Vitongoji nilipofika lile tatizo nililiona na mara hii sikwenda lakini nimefuatilia, nimeona amejitahidi lakini kutengeneza tu kidogo kwa Vitongoji hakuna maana kama tutasahau pale Chake Chake kwa sababu ndio msingi pale.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Omar Seif Abeid naomba umalizie.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mheshimiwa. La mwisho kabisa Mhe. Waziri namwambia sasa, kwamba kituo changu cha afya cha daraja la pili kilichopo Konde, Konde kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Rais ni kituo cha daraja la pili kinachotakiwa kifanye kazi kwa masaa 24 na tunae *MB* wetu pale aliyekuwa amemaliza kusoma sijui kwa nini hatujarejeshewa mpaka leo munampelekea *nurse* anakiongoza kituo kile. Namuomba sana Mhe. Waziri yule kijana aliyekwenda kusoma turejeshewe pale ili aweze kutoa huduma kituo kile kitoe huduma kwa masaa 24 kama kilivyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar akifuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Ali Suleiman Ali ajiandae.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti ahsante, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uhai na uzima na leo hii nami nichangie machache katika Wizara ya Afya. Kwanza nianze kukushukuru wewe vile vile kwa kunipa fursa hii nami nitoe maoni yangu kuhusu maagizo yaliyotolewa na kamati zetu hizi juu ya Wizara hii ya Afya.

Nianze kwa kuwapongeza kwanza kumpongeza Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa jitihada yake ya dhati ya kuona kwamba raia wake wanakuwa na afya, kwani afya ni tunu na ikiwa wakati huo huo anatekeleza azma ya Mapinduzi kwamba wananchi wa Zanzibar wawe na afya bora lakini pia wapate matibabu yakiwa bure. Sambamba na hayo niipongeze Wizara ya Afya pamoja na watendaji wake wote nao kwa kuchukua juhudi ya kuona kwamba maagizo yote yaliyotolewa na kamati yetu ya Baraza kwamba yamefanyiwa kazi. Hii ni dhahiri kwamba hili ni jembe na linahitaji kutunzwa sana ili liweze kufanya kazi iliyokusudiwa katika Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika mchango wangu kwenye ukurasa nambari mbili Agizo Nam. 2. Agizo hili nashukuru sana kuliona katika kitabu hiki pamoja na kuwa tayari nilikuwa nimeshakuwanayo kichwani kwangu kuona kwamba agizo hili nalo sijui kama litakuwemo, lakini bahati nzuri limekuwemo, suala zima la kuwa na Madaktari na Wafamasia katika vituo vyetu vyote vya afya vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli madaktari na wafamasia nao ni watu muhimu sana, kwani hawa ndio watu wa mwanzo wanaoweza kujua kwamba mgonjwa afanywe nini lakini na dawa gani apewe. Sasa kutokuwanao watu hawa itakuwa kwa kweli tiba itakuwa ina kasoro na leo serikali imefanya juhudi sana kuwatafuta watu hawa na kuona kwamba vituo vyetu wanakuwepo wanafanya kazi kama inavyopaswa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nipongeze kwamba Mhe. Waziri amefanya jitihada kubwa kuvitangaza hivi vipaumbele au motisha vya mishahara ya madaktari ambayo ni kivutio. Kwa sababu tulikuwa tukipiga kelele kwamba madaktari au wataalamu wetu wanakimbia kutokana na mishahara, leo wameitangaza bayana kwamba sasa "aliyemchange naje na ngoma hazingwa". Kwa hivyo, sasa waje wenyewe kama waliko hima waje kuona kwamba wanatoa huduma nchini pao badala ya kukimbia kwenda nchi za nje na kufaidisha wengine, watu hawa ambao

wamesoma kwa Serikali hii ya Mapinduzi na kuwa wananchi hawa ndio wanaotakiwa watoe huduma kwao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina lalamiko langu kwa upande wa Pemba. Kwa upande wa Pemba hawa wafamasia ni wachache, ama hakuna hasa katika vituo vyetu vya serikali au waliomo ni wa daraja la chini, kama wako ni wa ngazi ya *diploma.* Nashauri sana hawa wafamasia wapelekwe angalau japo kidogo wa ngazi ya *degree* nao waweze kutoa utaalamu zaidi na kuwasaidia hawa wenzao walioko chini.

Hivi sasa kuwapata watu kama hao ni shida lakini ni imani yangu katika mpango huu wataweza kupatikana naomba sasa nao wapelekwe Pemba wasibakie hapa Unguja tu. Nako kule hospitali zinaendelea kukua mahitaji yanaongezeka.

Mhe, Mwenyekiti, mchango wangu mwengine niende katika Agizo Nam. 3. Agizo hili niliposema wizara iweke kanuni za maadili ya mfanyakazi kwa hospitali na vituo vya afya pamoja na kuweka mfumo rahisi wa kutoa taarifa na malalamiko. Hapa nipongeze sana kwamba mtindo huu utakuwa ni vyema utaweza kuboresha shughuli zetu katika masuala ya afya, kwani kila siku tumekuwa tukilalamikia hospitali zetu kama vile Mnazi Mmoja pamoja na matatizo yaliyopo kweli kuna mambo ambayo yanafanywa hata ni kinyume cha binadamu. Lakini ni changamoto wanazozipata wenzetu kutokana na uhaba wa wafanyakazi, kwa kweli wafanyakazi wengine wako wanafanya kazi kwa moyo mmoja wanajitahidi lakini sasa mzigo ni mkubwa nao kulingana na wanaotaka kuhudumiwa, ndipo pale tunapowalaumu kwamba wenzetu ni wajeuri, hawatuthamini kwa kweli mimi nawaonea huruma sana. Nimejaribu kuziangalia hospitali za Mnazi Mmoja na hata kule Wete nikaona mzigo uliopo ni mkubwa wa wagonjwa kuliko madaktari waliopo. Lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naona kila siku inatoa vipaumbele kuona kwamba inatoa ajira kwa wafanyakazi hao wanapatikana.

Kwa hivyo, suala zima la kuweka kanuni ya maadili kwa wafanyakazi ni vizuri, kwa sababu kama daktari atavunja maadili yake ya kazi ataweza kuchukuliwa hatua inayofaa. Lakini pia vile vile liwekwe suala zima la kuweka sanduku la maoni katika kila vituo pale, kuna wengine wanaweza kumwendea daktari pale mmoja mmoja akamwambia kuna matatizo haya na yale, lakini wengine wanaoweza kuandika wataandika, wataweka maoni yao ndani ya sanduku lile, lakini sanduku lile lisibaki kuwepo tu kama sanduku la taka maoni yale yachukuliwe na kufanyiwa kazi hapo ndio italeta faida. Vile vile pia kwa wafanyakazi kabla hawajapelekwa kwenye hiyo kamati ya maadili na wao ni vyema tuwasomeshe kanuni za watumishi.

Mhe. Mwenyekiti, kanuni za utumishi hazieleweki kwa wafanyakazi, watu wanafanya tu wakishaajiriwa tu ndio wanafanya kazi kumbe kuna mambo yanamlinda lakini mambo nayo yanaweza kumuadhibu. Kwa hivyo, akishasomewa yale vyama vya wafanyakazi vile au viongozi wengine wachukue juhudi kuwasomea zile kanuni na waone kwamba mimi nikielekea huko nina makosa, itawasaidia sana kuweza kutiwa makosani bila ya kukusudia.

Vile vile kanuni ya maadili itakapokuwepo itaweza kusaidia kuona kwamba kila mmoja anajilinda asivuke mipaka aliyopangiwa, kama ni kutoa huduma atoe huduma inavyopaswa lakini mfumo wa malalamiko nao utasaidia kuondoa zile kero. Sisi wengine tunaweza kumfika

waziri moja kwa moja tukamwambia matatizo yaliyoko hospitali na kwa kweli akafuatilia. Mimi namshukuru sana kwa juhudi yake anaweza kufuatilia malalamiko ya wagonjwa wake.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa tano Agizo Nam. 4. Agizo hili linazungumzia suala zima la mpango wa kujenga nyumba za daktari katika Hospitali ya Abdalla Mzee. Kwa kweli ripoti inasema mnamo mwezi wa Julai wataalamu kutoka China walikuja Zanzibar kwa ajili ya kufanya mazungumzo. Mimi ningependa kujua kwamba, huu ni mwezi karibu wa nne je, hadi sasa hatua gani wamefikia katika ujenzi huu. Michoro wataalamu wameshafika ni hatua gani sasa iliyofikia kuona kwamba sasa kazi inaweza kuanza ili kuondosha usumbufu huu. Suala la madaktari kuwa karibu ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa nambari tano na Agizo Nam. 5. Hospitali ya Kivunge imeshapatiwa wataalamu. Kamati inashauri wizara inapopeleka changamoto hasa zile ambazo zina uhitaji mkubwa katika utoaji wa huduma kuzifanyia kazi. Kwa kweli niwapongeze, waziri alipopata agizo hili kuweza kulifanyia kazi na kuona kwamba sasa Hospitali ya Kivunge, hospitali ambayo inatoa huduma kwa sehemu kubwa sana Mkoa wa Kaskazini Unguja hii inaona kwamba amepata yale mahitaji yanayotakiwa. Lakini sasa, hapa ripoti inaeleza kwamba, wataalamu wameshakuwepo na wengine niwapongeze kuona umuhimu wa kusomesha wataalamu ili na wao wakirudi watoe huduma katika hospitali zetu, wataalamu 15 hawa wametolewa kwenda kusoma nje, na pia ripoti inasema kwamba wanawashajihisha madaktari na wauguzi wajiendeleze zaidi, lakini nimuulize Mhe. Waziri leo anashajihisha madaktari wajiendeleze, lakini ni motisha gani ambayo anawapa watu kama hao.

Kwa sababu ninavyojua sasa hivi wako watu ambao wanajiendeleza lakini mtu anahitajika katika *course* yake kama ni *degree* anahitaji shilingi milioni nne au tano anapewa shilingi milioni moja na nusu analipiwa masomo tu, halipi chakula, malazi, *field* wala chochote. Hapa hii motisha yao ni nini, watu kama wanajitokeza ili watu hawa wapate moyo wasijekuona kwamba wamesomeshwa na serikali yao na kuja kuitumikia ipasavyo. Hili ni jambo ambalo mimi naona tuliangalie sana, tunawahimiza wajitokeze kwenda kuchukua fani hizi ili waje wazitoe huduma hapa lakini na wao tuwaone kwamba tunawasaidia vipi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa sita Agizo la Sekta ya Afya kupanga bajeti ya kutosha. Wizara ilipoagizwa kufanya bajeti ya kutosha kutokana na mahitaji yanavyoongezeka siku hadi siku. Niipongeze serikali kwamba kwa kweli ni jambo kubwa sana kuweza kuongeza bajeti shilingi 4.9 bilioni hadi kufikia shilingi bilioni saba kwa mwaka 2017/2018. Ni pesa nyingi sana na sisi hapa pesa hizi tunaziidhinisha, lakini sasa kuwa na pesa ni jambo moja na kuzitumia ipasavyo ni jambo jengine.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana waziri asimamie suala zima la vitengo vinavyohusiana na manunuzi. Vitengo hivi ni muhimu sana vinahitaji kupewa kipaumbele, kwani manunuzi yale ambayo yanahitajika ni muhimu na kama kule sehemu za maabara, kama hakuna maabara watu wanaofahamu nini mahitaji tunaweza tukaagiza vitu ambavyo havihitajiki, lakini kwa sasa naona kuna marekebisho fulani tayari yameshafanywa ni tafauti na yuma ninavyoelewa hilo, huku nyuma ilikuwa kunakwenda ovyo. Nataka nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba usimamizi katika kitengo cha manunuzi ni muhimu na kupewa kipaumbele, kwani hata wakandarasi wakati mwengine nao wanashindwa kutoa huduma kutokana na kucheleweshwa malipo yao. Wizara ya

Fedha na Mipango na Wizara ya Afya nao waliangalie umuhimu wake afya kwanza, afya ni tunu.

Sambamba na kuongezwa bajeti hii naipongeza kwa kuona kwamba kuna vifaa muhimu kama *MRI, Dialysis* na tiba za saratani zinapatikana. Je, nimuulize Mhe. Waziri hapo nyuma aliwahi kutwambia baadhi ya hivyo vifaa vipo kama *MRI*, lakini unakwenda unaambiwa haifanyi kazi unaambiwa imefanyiwa kazi siku moja. Je, sasa inafanya kazi? Hii mashine ya *MRI* inafanya kazi hapa, maana leo watu wengine wanakwenda Dar es Salaam kufanyiwa vipimo hivi sijui hapa kweli inafanyiwa kazi au imo ndani ya ripoti tu.

Mhe. Mwenyekiti, huku maabara kuna mashine ambazo ni za zamani sana zinahitaji kufanyiwa mabadiliko na matengenezo. Kwa mfano, *Electro-Light* ni mbovu katika maabara zetu, hiyo mashine inahitaji kufanyiwa matengenezo lakini pia itafutwe nyengine ya kisasa na mashine zilizoko zitafutwe za kisasa, lakini wawekwe watu ambao wanaweza kuzitumia ili waweze kuona kwamba uchunguzi wetu unafanyika katika hospitali zetu badala ya kwenda hospitali binafsi. Zile mashine ambazo zinaonekana zinamalizka haraka haraka basi zitafutwe ya pili singojee mpaka ile ikamalizika kabisa ndio tukatafuta nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, mashine za *CT Scan* na *X-ray* na *Ultrasound* zilizopo nasema kwamba hivi sasa zinafanya kazi afadhali, lakini bado wakati mwengine kuna matatizo unaweza ukaambiwa hakuna karatasi. Huu unakuwa ni mtindo, kwa sababu watu wanaitumia fursa ile ya kuona kwamba watu wanalipishwa baadhi ya wengine, wakati mwengine hata ikiwa karatasi za *X-ray* zipo unaambiwa mgonjwa hakuna kanunue. Hii inavunja moyo sana, serikali inataka wafanyiwe vipimo hivi bure kabisa lakini bado kuna wagonjwa wanakwenda pale kwenye *CT Scan* mtu anaambiwa atoe shilingi 50,000 yeye atazipata wapi na tangazo Rais ameshasema kwamba matibabu ni bure. Naomba kile kitengo cha malipo kule Mnazi Mmoja kiondolewe hasa ndio itakapoonekana kwamba matibabu ni bure, lakini leo kuendelea kuweko kule wako wengine baadhi yao wasioitakia mema serikali hii ionekane ni dhaifu bado unakwenda wanadai malipo, wanadai huduma ambazo ni za bure. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba sana atakapoona kwamba kitendo hiki kinafanyika basi na yeye akikemee sana na hiki kitu kinafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, niende ukurasa wa saba...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante, ukurasa wa saba suala zima la nyumba za madaktari, ukurasa nambari tisa nyumba za madaktari majimboni. Kwa kweli sasa hivi tumeacha juhudi hii ya kuona kwamba na sisi wawakilishi tunafanya jitihada ya kuona nyumba za madaktari zipo. Je, Mhe. Waziri kwa zile sehemu ambazo tayari zimeshaanzwa ni msukumo gani atakaoutoa kuona kwamba nyumba hizi zinamalizika, pengine Mfuko wa Jimbo unaweza ukautumia kwa kuona kwamba hospitali zile zinataka ziendelee lakini sasa je, wizara itakuwa ina mpango gani kwa nyumba za daktari zinazoanzishwa na kuunga mkono juhudi za wananchi.

Hayo ni machache nashukuru sana na mengi yapo lakini muda hautoshi, nawapongeza sana naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na nawapongeza sana wafanyakazi wa Wizara ya Afya pamoja na watendaji wote ambao wamefanya kazi hii.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango. Sasa naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub atafuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali na Mhe. Nadir Abdul-latif ajiandae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii jioni hii kukushukuru wewe kuniruhusu hapa kuchangia wizara ambayo mimi, wewe, sisimizi, ng'ombe, punda, kila mtu anahitaji afya bila ya afya huwezi kuishi. Ni wizara muhimu sana, wizara nyeti sana tunayoijadili muda huu, wizara ya kuifikiria sana tena, wizara ngumu kuiongoza tukiri hilo suala maana yake sio mchezo, ni wizara moja muhimu sana bila ya afya huwezi kupata chochote kama sasa na vile maji.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe fursa hii kumpongeza kwa dhati kutoka ndani ya nafsi yangu huwa nikiendelea kusema haya Mheshimiwa jirani yangu Mhe. Suleiman hapa husema hata saa 9 usiku usingizi ukiwa mkali unanguruma aah!Mhe. Dr Ali Mohd Shein kafanya nini hasa katika sekta ya afya sirudi nyuma. Usingizi mzito ule saa tisa saa nane nakoroma nasema kila Rais kafanya mambo lakini kila mmoja kafanya mambo kwa uwezo wake, kama kuna Rais ninayemkumbuka mimi kama Mhe. Dr Ali Mohd Shein katika Sekta ya Afya nitakuwa sijamtendea haki, amefanya kazi na sisi sote shahidi humu. Imani yangu Mhe. Dr. Ali Mohd Shein ataendelea na juhudi zake na mipango ya kuwatumikia Wazanzibari na namuomba Mwenyezi Mungu amtie nguvu ampe afya njema na ari za kuendelea kutekeleza ahadi zake za Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo, amefanya kazi kubwa.

Nitakuwa mwingi wa fadhila na nitakuwa mtovu wa adamu wa mwisho kama sikuwapongeza ndugu zetu wa China. Hawa ndio marafiki wa kweli katika watu waliotusaidia kama watu wa China hakuna, kwa kila aina ya msaada wametusaidia sana Jamhuri ya watu wa China, imefanyakazi kubwa sana Zanzibar niwapongeze kwa dhati sana angekuwa kuwa yupo Mhe. Balozi Seif Ali Idd ningemtuma salamu akatupelekea kwa Balozi ndogo aliekuwepo China, wametusaidia vya kutosha mno ikiwemo kampuni ya *Jiang Su* iliyojenga hospitali ya kule Abdalla Mzee, *professional* imefanyakazi kubwa ambao mradi ule karibu milioni kumi na sita dola sio mchezo *Jiang Su.*

Mhe. Mwenyekiti, niendelee tena kuwapongeza baadhi ya watendaji wa Wizara ya Afya sio wote, akiwemo Waziri, Naibu Waziri rafiki yangu Dr Jamala Katibu Mkuu bado sijapata kuonana nae kidogo ni mpya. Lakini Dr Jamala niko nae karibu sana lakini sijui kama yupo leo juu hapo, ni mtendaji kazi nzuri. Lakini kama sikumshukuru Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame nae nitakuwa sijamtendea haki mwenyekiti wa kamati hii pamoja na watendaji wake. (*Makofi*)

Nimpongeze Mhe. Rais kwa bajeti ya dawa pesa alizotoa karibu 7 bilioni kwenye dawa. Ni jambo la kupongeza sana kwa kujali afya za Wazanzibari. Lakini Mhe. Waziri elimu kama wapo watendaji wako itakuwa vizuri, elimu ya ugawaji dawa hafifu, haitoshi, haikidhi sijui kama kutokana na ajira mliowapa au uwezo wao ni mdogo. Lakini dawa ile ile moja inaweza kutibu maradhi mengine, wataalamu sijui wanatumia lugha inatwa *brander name na genaric name*. Dawa ile ile moja inaweza kutibu lakini utaambiwa dawa ile dirashani haipo wakati ipo. Hiyo kidogo Waziri na Naibu Waziri kaeni kama watendaji wananisikia huko wanisilize uzuri kabisa wasiseme dawa haipo wakati dawa ipo, elimu ni ndogo mnayatoa, watendaji hilo mjipange sana.

Lakini sasa Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo nianze na huu mchango wangu katika kitabu hichi ukurasa wa mwazo kabisa agizo namba 1. Kamati imeshauri serikali kuhakikisha bajeti ya Wizara ya Afya inaongezwa ili mipango ya utekelezaji wa kazi wizara itekeleze kwa ufanisi. Serikali imeengeza Bajeti ya Wizara ya Afya kutoka shilingi bilioni 44.2 kwa mwaka 2016/17 na kufika shilingi bilioni 58.7 kwa mwaka 2017/18 jambo la kupongezwa. Kamati imeliona na imelipongeza na dawa kidogo sasa hivi mimi nashakuru hata jimbo kwangu kiasi sasa hivi sijapata kupigiwa simu. Mara nyingi hupigiwa simu kwenda kununua dawa muda mrefu sijasikia malalamiko hayo kutoka Jambiani. Kwa hiyo, niipongeze wizara nimpongeze Dr. Ali Mohd Shein kwa kitu muhimu maana bila ya dawa huwezi kupata matibabu.

Agizo 2: Serikali itoe kipaombele kwa ajira na wataalamu wa afya hasa madaktari kwa kuweka maslahi mazuri na vivutio vya kazi kwa waliopo. Mheshimiwa hapa Waziri wa Fedha hayupo hivi sasa sijui kama yupo. Hawa madaktari mabingwa angalau mungewawekea msamaha wa magari angalau ikawa kivutio, mkagawa viwanja vidogo vidogo mkawapa viwanja vya kujengea nao vivutio. Lakini madaktari wote mabingwa watakimbia tu wataondoka. Hivi vitu mvifikirie kidogo serikali kuwapa moyo watu hawa. Gari kama daktari mmoja uwezo wake mnampa msamaha wa gari, kivutio vile vile kama pana kiwanja pa kujenga mnamtafutia kiwanja ndio vivutio wanafanya kazi ngumu hawa madaktari tusiwe tunawalaumu tu muda wote.

Lakini na jengine niliombe siasa hapa isiwepo nitaendelea kusema, siasa katika hospitali isiwepo. Anapokwenda pale hata mwizi daktari atamtibu tu hajali anatoka chama gani hajali anatoka upande gani. Kwani hizi hospitali zimejengwa kwa siasa hazikujengwa siasa waliokuwemo wasiokuwemo wote wanatibiwa. Kwa hapa kidogo madaktari wengi wanatukimbia kwa sababu wa siasa wakati mwengine na hili tuliangalie tunatumia pesa chungunzima kusomesha wataalamu baada ya muda wanatukimbia na hili Mhe. Waziri nalo uliangalie sana.

Nije hapo hapo agizo namba 2, Hospitali ya Mnazi Mmoja zimetengwa ajira karibu 180 Mhe. Waziri hivi ninavyokwambia sasa hivi kama kuna mgonjwa katibiwa leo, leo ya nane yuko Mnazi Mmoja mtoto kafa tumboni, naam sizungumzi kwa kubahatisha leo ya nane mtoto kafa tena anatoka jimboni kwangu kafa tumboni kama kusafishwa kasafishwa leo baada ya kuingia mimi mwakilishi. Tunafanya nini siwezi kumtaka jina lake tu hapa lakini kitu cha kusikitisha, nimempigia simu mhusika wa *maternity* anaitwa Mbare sijui akanambia mimi niko likizo mimi. Leo ya nane mtoto kafa tumboni hajasafishwa, ni kitu cha aibu sitaki kumtaka jina mimi na hii si kesi ya kwanza, hapo nyuma ilitokea tena Jimboni kwangu Muungoni kachukuwa siku nne. Uwajibikaji uko wapi, sitaki kumtaja jina hiyo kesi ipo. (*Makofi*)

Lakini uzembe mwengine tusitumie neno uzembe tuseme sijui kupitikiwa naweza kusema uzembe au kupitikiwa mtu anaonesha jino jengine anangolewa jino jengine ni kitu gani hicho imeshatoka kesi Mnazi Mmoja hiyo. Anaonesha jino la kutolewa anangolewa jino jengine tena anasema silo atakatolewa lile tunafanya nini? Kitu cha kusikitisha sana waziri atakuwa anayajua hayo.

Nije hapo hapo namba 2 Mtaalamu mmoja tu wa viungo bandia kwa kweli hatoshi, serikali ifikirie. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis hapa alikuwa anapiga kelele suala hili hili daktari huyu mmoja hatoshi. Kwa hiyo, lichukuliwe na mkalifanyie kazi.

Vituo vya Afya tayari vipo chini ya Halmashauri chini ya Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa Idara Maalum za SMZ na ndio watakaohusika moja kwa moja katika masuala ya ajira ya vituo, huu ni mtego na tutaumiza watu. Ukienda huku Halmashauri watakwambia mimi si kazi yangu, ukienda huku watakwambia Wizara ya Afya tusiige watu, mtu huvaa kiatu au mbuzi hula majani kutokana na urefu wa kamba yake tusijaribu kuiga watu huu ni mtego tutaumiza wananchi hapa, ukenda Wizara ya Afya utaambiwa nenda Halmashauri. Hapa tumekwenda tutumie lugha gani nisije nikateleza mdomo na maneno mengine naweka akiba nisije nikamaliza yote.

Halmashauri watakambiwa mimi si kazi yangu pesa hapana huku Wizara ya Afya watakwambia nenda Halmashauri tutaumiza wananchi wetu. Tusijaribu kuiga tu kila kitu huu ni mtego na sijui tumefikiria nini hapa ugatuzi, ugatuzi upi, tutaumiza wananchi utakwenda pale utaambiwa nenda Halmashauri, italeta dawa hapana dawa atakwambiwa si kazi yangu Halmashauri, utakwenda Wizara ya Afya atakwambia Halmashauri hata akija kutoka mtu keshakufa mtihani mkubwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nije katika malalamiko mengine ukurasa wa 4. Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hoja ya kuweka mfumo wa kutoa taarifa ya malalamiko kwa wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja imeanzisha huduma za malalamiko kwa wateja masaa 24 ambapo wagonjwa au jamaa wa wagonjwa hutakiwa kupeleka malalamiko. Hili nililipigia kelele mimi na nikamshukuru Waziri wazo hili akalipokea na kulikubali lakini kilichokuwepo pale ni boya, mlango upo umefungwa hujui ukalalamike wapi juzi nimekwenda nikayakuta hayo.

Sizungumzi kwa kubahatisha Mhe. Mwenyekiti, nazungumza Mwenyezi Mungu ananisikia hapo pa kulalamikia hapo chini kitengo cha sukari mlango umefungwa mimi nilikuwa siujui utakwenda kulalamika wapi na mwenye nyumba hayupo ukaseme na ukuta? Watendaji hawa Mhe. Waziri utapata shida ng'ombe wa mbele hataki kwenda anapigwa ng'ombe wa nyuma watendaji wako kaa nao siku zote utapata lawama za Wawakilishi humu ndio tunazungumza kwenye kamati tutakulaumu, tutaendelea kukulaumu watendaji wako wala si kosa lako. Lakini mkamatwa na ngozi ndie mwizi.

Mhe. Waziri mimi nakuonea huruma sana tena mpaka Naibu Waziri mimi humkimbia kumuuliza swala la nyongeza nashindwa hawezi kunijibu watendaji wapeni elimu si makosa yenu, tutakuoneeni bure nyie lakini watu wenu hawataki kufanya kazi, Waziri utaitwa hapa Naibu Waziri tutakulaumu bure unakuja kutijibu mambo mengine humu hata hayaeleweki tunatumia Kanuni lakini mwisho tena imani inatujia, si kosa lako kosa la watendaji wako jaribu kuwagomba huruma hailei mwana, hatuwezi kufika. (*Makofi*)

Mhe. Waziri unga utakuja kuingia maji Mwenyezi Mungu akuepushe utaonekana wewe ni mzembe na sote tunakujua mimi nakujua utendaji wako, Naibu Waziri kidogo siwezi kumjua nimemkuta juzi lakini mimi nakujua Mhe. Waziri, watendaji hawa kaa nao kuna siku za Jumamosi, Jumapili weka semina waambie moja, mbili, tatu. Haiwezekani uje ulaumiwe siku

zote Waziri na Naibu Waziri tunakuoeneni huruma wakati mwengine kwa makosa ya watendaji wenu haielekei utafutwe waziri uitwe wewe utajibu mangapi Hospitali zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri mie naenda kwenye changamoto nyengine suala la ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Abdalla Mzee lilifanyiwa kazi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya China. Mhe. Mwenyekiti, hili ni agizo la Mhe. Rais la muda mrefu mimi nilikuwa niko shahidi pale Pemba, nilikuwa Pemba pale hili suala akalipigia kelele sana Mhe. Rais na nilimpongeza sana Mhe. Rais akatuonesha hata picha aliyoileta pale alifanya kazi kubwa ya Hospitali ya Abdalla Mzee ile picha ilinivutia sana mimi katika ufunguzi wa Hospitali ile akasema ndio aliitafuta mpaka akaipata si jambo dogo.

Hapa Mhe. Waziri hebu nisaidie kidogo kulikuwa na changamoto naikumbuka nilii- *note* siku ile mbali na mafanikio tuliyonayo hadi leo hii tulifungua hospitali yetu hii si vibaya nikaunganisha kwamba bado tunazo baadhi ya changamoto hususan ile uhaba wa wafanyakazi katika kada ya uuguzi, udaktari, wafamasia, maabara kwa pande za Unguja na Pemba. Changamoto hizi kupitia miongoni mwa maelekezo yako tumeanza kuzifanyika kazi kwa kushirikiana na Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hebu nieleze mwaka mmoja naa kweli kitu hichi kimefanyika au ndio maneno tu vitendo havipo.

Hii ni changamoto ya muda mrefu na ma-*blocks* manne yaliyokuwa yanataka kujengwa pale nayakumbuka uzari alisema mwenyewe Mhe. Dr. Ali Mohd Shein saa 5: 45 siku ili ilikuwa Mkoani pale, aliagiza kujengwa ma- *blocks* manne aliagiza Mhe. Rais Hospital ya Abdalla Mzee yamefikia wapi kwa ajili ya wafanyakazi nakumbuka hata aliposema ile hadithi ya Mhe. Mao Tse Tung. "hata wewe", hadithi refu ilikuwa ile kama Mhe. Waziri unaikumbuka na Wajumbe walikuwepo siku ile Mkoani Pale "hata wewe" ya kuuza maneno hiyo.

Serikali imeongeza bajeti ya ununuzi wa dawa na vitenganishi vya vifaa kutoka 4 bilioni. Hapa niipongeze wizara hasa katika kitengo cha *dialysis* hichi kitengo kina kazi kubwa na pesa nyingi zinahitajika. Hapa hichi kidogo ni muhimu sana na watu wengi sana wanapoteza maisha kutoka kitengo hichi, kitengo hichi ni muhimu kama kuna msimamizi kiangaliwe pesa nyingi hapa zitahitajika na zitapokea.

Mhe. Mwenyekiti, nije na agizo 11. Kamati inaishauri wizara kuimairisha huduma za vipimo vyote katika hospitali zake pamoja na vituo vya afya kwa lengo la kuwaondoshea usumbufu wananchi na hata wafanyakazi wanaotoa huduma hizo. Mhe. Mwenyekiti, kama pana tatizo Hospitali ya Mwembeladu pana tatizo kubwa sana, kipimo pale kinafanyika wiki mara moja tena kipimo muhimu cha *ultrasound* tena ikishafika watu kumi nafikiri kimekwisha watu wanakwenda saa kumi za usiku *ultrasound* Mnazi Mmoja watendaji nisikilizeni uzuri huko kama mpo na kafatiliaeni, Ijumaa hata Ijumaa na wamo humu wafanyakazi wetu humu katika Baraza wake zao imewakuta mitihani hiyo. Kipimo hicho muhimu utamjuaje mtoto kakaa vipi atahitaji operesheni au vipi. Lakini umeshapima watu 10 *ultrasound* hiyo haifanyi kazi tena na Ijumaa hata Ijumaa aah! huu ni mtihani. Kama kuna pahali kuongezwa *ultrasound* iongezwe pale katika kitengo kile na ukenda hapo Mnazi Mmoja chumba kimoja wamejazana hivi watu. Bado kipimo hichi serikali ifanye kazi kuliko hicho cha *DNA*, hichi kina umuhimu wake kimekuwa tabu sana kupatikana leo wiki nzima Mwembeladu unakwenda kufanya kipimo hicho haielekei.

Baada ya hapo nije katika.....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub muda wako umemalizika lakini naomba umalizie nakuongeza na dakika moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

La mwisho, niombe sana Wizara ya Afya maneno mazuri ukiyatoa mdomoni ni sadaka hata kwa Mwenyezi Mungu, maneno mazuri humtoa nyoka pangoni, kulainisha ulimi si vibaya kwa kuwahudumikia hawa watu, lugha kidogo madaktari tumieni lugha za kibinadamu, maneno mazuri ni sadaka ya bure. Kwani Dini ya Kiislamu haina mitahani kwa kutafuta thawabu. Utaratibu wote Mwenyezi Mungu katupangia maneno tu unapata thawabu, waelimisheni watu wenu na maneno haya. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub na mimi nakushukuru kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali, atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul- latif na Mhe. Simai Mohamed Said ajitayarishe.

Kabla ya kumpisha Mhe. Ali Suleiman Ali naomba niwakumbushe Wajumbe muda wetu wa kuchangia ni dakika 15. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Waheshimiwa Wajumbe muende kwenye dakika hizo na wachangiaji wako wengi ambao wanataka kuchangia.

Kwa hiyo, nawaomba sana muende na hizo dakika. Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia Ripoti au Taarifa ya Utekelezaji ya maagizo ya Kamati, Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, madaktari wetu, wakurugenzi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya hasa tukizingatia kwamba bila ya wao maisha yetu yako hatarini.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wale wanaofanyakazi kwa moyo safi kabisa kwa sababu anaefanya vizuri mpongeze sana na aliekuwa hafanyi kazi vizuri muelekeze.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nampongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hasa tukizingatia kwamba yeye *field* yake ndio hii. Mheshimiwa anaumwa sana na mambo ya hospitali au na mambo ya afya na ana uchungu sana na mazingira yanayokwenda kutokana na anakotoka yeye na tunakolekea wakati mwengine. Lakini nampongeza kwa uwezo wake na mbio zake na akahakikisha kwamba mabadiliko ya vituo vyetu yako makubwa katika nchi yetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiri kwamba madaktari na wauguzi wanakula kiapo wanapokuwa wanafunzi sawa sawa na mimi nilipokuwa mwanajeshi nakula kiapo nitaitumikia nchi yangu na popote nitapotumwa na taifa langu na kiapo kile kinakudhuru kinakwenda

kinyume na kauli hiyo. Kwa hivyo, niseme kiapo kile kina mtihani wakati mwengine kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwanzo unapotakiwa kuwa daktari au muuguzi unatakiwa uwe mtu wa huruma sana na uwe na imani ya kutosha hapo utakuwa mtiifu na utamjua Mwenyezi Mungu kama yupo.

Lakini niseme tu kwamba Mhe. Mwenyekiti, mimi nawapongeza madaktari wetu kama nilivyotangulia kusema na nawapongeza wauguzi na wahudumu wote wa afya zetu. Lakini natoa mambo mawili au matatu.

Kwanza niseme Mhe. Mwenyekiti, jambo kubwa tunalolitegemea kwao ni msaada kwa wagonjwa wetu wanapofika mahospitalini kwetu au katika vituo vya afya. Mapokezi nzuri, heshima nzuri na lugha nzuri basi mgonjwa anapata nafuu akatabasamu na yeye. Lakini unafika pale unaanza kuambiwa umechelewa, umefanya nini au umetoka wapi basi itakuwa kidogo unampa maumivu zaidi yule mgonjwa na wakati huo yuko katika hali ya mahututi hajiwezi.

Kwa hivyo, natoa ushauri wa bure, nawaomba sana watabibu wetu wote wa fani zote tunawategemea wao na Inshaa Allah Mwenyezi Mungu awaongoze katika imani hiyo nzuri ili wafanye kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza kamati chini ya Mwenyekiti wake Dk. Mwinyihaji Makame na wajumbe wake wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya kutuletea taarifa hii muhimu na leo tumesimama hapa kutoa mawili au matatu juu ya kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri. Mimi nitakuwa na mambo mawili au matatu tu mheshimiwa pengine dakika zangu sitozimaliza.

Agizo namba 3 kwenye ukurasa wa 3. Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti,

"Wizara iweke kanuni za maadili ya wafanyakazi kwa hospitali na vituo vya afya pamoja na kuweka mfumo rahisi wa kutoa taarifa na malalamiko kwa wananchi ambao wataona mabadiliko ya kazi yakivunjwa na baadhi ya wafanyakazi"

Mhe. Mwenyekiti, ndio nikasema kwamba yanapotokea hayo, tuone kama yanatokea wakati mwengine kibinadamu, lakini na binadamu anatakiwa apate ushauri ili ajielewe mambo yake yanavyopotea wakati mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, katika hayo tumeambiwa kwamba kuna wafanyakazi kama sita. Zipo kesi sita ambazo tayari zimechukuliwa hatua, katika ukurasa wa 4. Kesi hizo zimechukuliwa hatua baada ya Baraza la Wauguzi na Wakunga kupelekewa malalamiko, kutokana na makosa hayo hatua zilizochukuliwa ni kupewa barua za onyo kali, wahusika hao kusimamishwa leseni na usajili wa huduma za uuguzi na ukunga.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri hili linafaa. Lakini narudia tena binadamu anaweza kuteleza bila ya kujitambua. Mimi naomba ushauri nasaha utumike kwa wale ambao wanakosea na wakielekezwa wanakubali, siwatetei. Lakini nasema tu kwamba tutumie busara za ushauri zaidi ili kumjua kila muuguzi na daktari ajuwe wajibu na lugha yake ifahamike vizuri kwa wagonjwa wanaofika pale.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakalozungumzia jengine, kwanza niwapongeze wananchi wetu wameamka sana kwenye maeneo mbali mbali vijijini na hata mjini, ingawa sasa hivi tuko katika ugatuzi. Ugatuzi huu unamsongamano kidogo, wananchi wengine wanauelewa na wengine hawauelewi. Kwa hivyo, nataka somo hili la Wizara ya Afya na Tawala za Mkoa bado wakae pamoja kuwaelimisha wananchi ili wajuwe tofauti hii iliyojitokeza ambayo tunakwenda nayo sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawapongeza sana wafanyakazi wa Kituo cha Afya Fuoni. Wafanyakazi hawa wanafanyakazi nzuri, ukenda pale lugha nzuri na wanafanyakazi kwa kuhami maeneo mengi katika majimbo yetu katika Wilaya yetu ya Magharibi B.

Mhe. Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Fuoni kuna Jimbo la Kijitoupele, Jimbo la Fuoni, Jimbo la Pangawe na mpaka Jimbo la Tunguu wanafika pale kupata msaada kwa wenzetu wale wa Kituo cha Afya ambao wanafanyakazi nzito na nzuri, watu wanatoka Tunguu wanakuja hapo. Kwa hivyo, mimi nawapongeza kwa dhati kabisa. Hivyo, naiomba wizara iwasaidie wenzetu hawa kutokana na *Ambulance* yao ambayo iko pale mara nyingi huwa haina mafuta na inakuwa adha kidogo. Anapotokezea mama ameshindikana pale apelekwe Mnazi Mmoja basi inakuwa ni tatizo kidogo. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri suala hili aliangalie.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika kituo hicho Mwenyezi Mungu awazidishie imani na lugha zao nzuri ndio maana kinavamiwa sana kupindukia. Kwa hivyo, mimi ombi langu liko hapa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kituo hiki kimekusanya maeneo mengi na wafanyakazi wanafanyakazi wakati mwengine mpaka wanakuwa taabani, lakini wanafanyakazi kwa sababu ndio kiapo chao. Namuomba sana Mhe. Waziri Kituo kipya cha Afya cha Jimbo la Kijitoupele ambacho kipo Magirisi Taveta. Namuomba sana Mhe. Waziri tukimaliza Baraza hili afanye ziara maalum na wananchi angalau wamuone na wawe na uhakika kinachofanywa. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kituo hiki kilijengwa na Mhe. Bunge mstaafu alipokuwa Jimbo la Mwanakwerekwe Mhe. Sereweji, pamoja na Mhe. Shamsi wakati ule alikuwa yeye ni mwakilishi. Walikijenga kwa asilimia nzuri tu, lakini na mimi nikasema kwamba huku ni kuwekeza leo na kesho tunapokwenda. Unapojenga Kituo cha Afya, unapofanya jambo zuri lolote basi utalikuta kesho unapokwenda, nikasema na mimi katika juhudi zangu kwa njia zozote nitakazojaaliwa kituo hiki kimalizwe.

Sasa na mimi kwa bahati nzuri, wenzangu walitumia karibu milioni 64 na mimi nikasema nitapiga kazi kidogo ili nihakikishe kwamba naipa changamoto wizara itusaidie kwa umalizaji uliobakia ambao nitaueleza hapa. Mimi mfuko wangu wa jimbo wa milioni 20 nimezitumbukiza hapa. Nasema sasa hivi madirisha tayari, *fitting* ya umeme yote tayari, *plaster* nje na ndani tayari, mlango wa mbele na nyuma ndani haijawekwa maana niwe muwazi kabisa haijawekwa, lakini mbele na nyuma tayari. Kilichobakia Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kikubwa bado *tiles* chini na bado *gypsum* juu basi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa kupitia wafadhili mbali mbali tuliokuwa nao katika nchi yetu na hata nje ya nchi, twende sambamba ili tuhakikishe kituo hiki kinamalizwa haraka na wananchi wetu wanapata huduma hapa, hasa tukizingatia kinamama wajawazito watajifungua katika kituo hicho, watapata mapumziko mazuri na watoto na wazee watapata mambo ya ya afya hapo hapo karibu.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kuna wafadhili wetu wa ndani wazuri. Nitatoa mfano mmoja, Mhe. Ahmada Shaa ni mbunifu kama Waziri wa Afya. Maana Waziri wa Afya na yeye ni mbunifu wa kutafuta wafadhili mbali mbali katika fani mbali mbali, nampongeza sana kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kazi iliyobakia ni tiles, *gypsum*. Tumepewa na wizara tuseme angalau tupige kuta mimi na mbunge, tuko tayari kuta lote tutalizungusha sisi, ili kuhakikisha kwamba inatupa imani kuwa na wananchi na wao wafaidike na wawe katika hali ya usalama, hasa katika mazingira ya kinamama wanapojifungua. Kwa hivyo, niseme tu kuwa namuomba sana Mhe. Waziri suala hili alipokee.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Shaa aliwahi kuwajengea nyumba ya madaktari katika hospitali ya Tunguu. Nyumba ile tulipiga kelele na imemalizwa, nafikiri daktari yule sijui kama yupo au vipi. Lakini wananchi wale wanaimani wanapata huduma kwa saa 24. Ombi langu kwa Mhe. Waziri, kwa kuwa tuna wafanyakazi wa afya katika hospitali mbali mbali, lakini wapo katika Jimbo letu la Kijitoupele, hivyo limalizwe lile jengo ili wafanyakazi waliokuwa karibu waishi pale basi tutakuwa na uhakika kwamba linapotokea tatizo saa 24 basi watu watakuwa wako karibu wa kupata kutoa huduma kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, jengine la mwisho, naamini baada ya kumuomba sana Mhe. Waziri basi mimi niko tayari kufuatana na yeye kwa kila pahala ili maombi yetu haya tunayoomba twende sambamba. Lakini na mimi najua nimesema Mhe. Ahmada Shaa kwa sababu yeye ni mwenyeji, ni mbunifu na ana njia nyingi za kupata. Kwa hivyo, ombi letu la *tiles* na *gypsum* juu tushirikiane na yeye ili tuhakikishe kwamba tunaisaidia serikali yetu kuhakikisha hili tunalipata. Mimi na mbunge narudia tena ukuta tutaumaliza sisi kwa muda mfupi ujao Mwenyezi Mungu akitujaali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache, niseme tu kwamba naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Pia nawaomba wale madaktari niliowaomba imani zao wazioneshe kwa wagonjwa wetu, ili na wao wapate fungu lao la duniani na kesho akhera. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata. Waheshimiwa Wajumbe kama nilivyosema mwanzo kuwa nina wachangiaji wengi, kwa hivyo kutokana na muda wetu naweza nikawataja wachangiaji wanne na wao nitawapa dakika 10, ili tumpe nafasi Mhe. Naibu Waziri achangie na mwisho kufanya majumuisho Mhe. Waziri wa Afya. Kwa hivyo, wale ambao nitakuwa sikuwataja naomba wachangie kwa maandishi. Sasa naomba nimwite Mhe. Nadiri Abdul-latif, atafuatiwa na Mhe. Simai Mohamed, Mhe. Ahmada Yahya na Mhe. Hamad Abdalla Rashid Gerei ajiandae.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona nianze kwa kukushukuru wewe, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii leo na kuweza kuchangia hii ripoti ambayo ni muhimu sana ya utekelezaji juu ya taarifa yao na maagizo ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa kamati juu ya maagizo mbali mbali, na nitapenda nimnukuu mjumbe mmoja wa Baraza la Wawakilishi hili

ambaye ni *senior* wetu humu ndani kwa sababu tumemkuta kwa sisi ambao ni wapya. Alisema kwamba siasa yote na hasa umuhimu wa ahadi ambazo Chama cha Mapinduzi imeahidi kwa wananchi, basi Wizara ya Afya ni katika sehemu moja ambayo inawagusa sana wananchi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein kwa kazi kubwa ambayo anaisimamia serikali yake, lakini pia kuhakikisha kwamba jicho lake haliwi mbali na hospitali zetu ya Mnazi Mmoja na nyengine zote.

Pia Mhe. Mwenyekiti, uthibitisho huu unakwenda kwamba hata sehemu yake ya kufanyia kazi ipo jirani na hospitali yetu hii ya rufaa. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika ripoti hii kwa mwaka 2016/2017 bajeti ilikuwa bilioni 44.2, na ukiangalia kwamba mwaka huu wa 2017/2018 bajeti imeongezeka kwenda bilioni 58.7. Kwa kweli lipo ongezeko la hizi fedha kwa ajili ya kuwahudumia wananchi, lakini bado mahitaji ambayo wanahitaji pale ni makubwa na kama tunavyofahamu Bara la Afrika na duniani ni Chama cha Mapinduzi pamoja na serikali hii iliyokuwepo madarakani ndio wameweza kuwa na nafasi kubwa sana kutoa huduma nzuri za afya hasa kwa wananchi wetu lakini kwa bure kabisa.

Mimi hivi karibuni jimboni kwangu vijana wangu wanakaribia 15 walipinduka na ajali, na nichukue nafasi kumshukuru Mhe. Waziri wa Afya pamoja na Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira walikuja pia usiku kuungana na sisi na Naibu Waziri wa Afya hakuwa mbali na mimi. Lakini nilipokwenda pale kwenye *emergency* walipokelewa vizuri na wakapata huduma. Masikitiko yalikuwa ni kidogo yule mtu wa *x-ray* aliambiwa abakie, lakini tukajikuta kwamba hayupo. Kwa hivyo, vitu kama vile ni muhimu sana kuhakikisha Mhe. Mwenyekiti nidhamu ya wafanyakazi inazidi kuboreshwa na hawa watu kuwe na utaratibu rasmi wawekewe ili mtu anapoingia na kutoka atambulikane yupo wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu wakati mwengine mtu anaondoka kama anakwenda kupiga urojo au anakwenda kwenye maziko au pia anakwenda kufanya mambo yake ya binafsi, lakini lazima ijuulikane kwamba anapotoka wapi amekwenda na muda gani atachukua. Sio anapoingia kazini anatoka toka tu moja kwa moja, kwa sababu pale ni pahala ambapo wakati wowote mtu anaweza akafika kuhitaji huduma.

Mhe. Mwenyekiti, na hili suala la nidhamu linazungumziwa sana na wajumbe wengi, sasa ni vizuri ukafanyika utafiti hii nidhamu inayozungumzwa, inazungumzwa kwa watendaji wakubwa ambao ni madaktari bingwa, inazungumzwa kwa watu wa kati ambao pengine ni wasaidizi au na hao ma-*orderly* na wengine, kwa sababu ina wafanyakazi wengi sana Mnazi Mmoja. Ukiangalia sasa hivi baada ya jengo lile jipya mahitaji yataongezeka. Moja ya changamoto iliyokuwanayo hospitali yetu ya rufaa ya Mnazi Mmoja, ni kwamba wananchi wengi bado wanafuata huduma katika hospitali ya Mnazi Mmoja, wakati huduma hizi zinapatikana katika hizi hospitali zetu ambazo ziko katika wilaya na maeneo mengine na hivi vituo vya afya. Sasa hizi huduma ambazo zinaboreshwa katika maeneo ya wilaya na vituo vya afya, vifuatiliwe kwa undani sana ili kuhakikisha kwamba wingi wa watu wanaokuja Mnazi Mmoja isiwe kwamba hizi mashine zinazidiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nitakwenda kuligusia suala moja dogo tu ili niweze kuishauri na kuisaidia serikali. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimejaribu sana kuangalia hiki kitengo cha Dayaspora ambacho Mhe. Rais anakianzisha na kipo katika ofisi yake. Lakini hii Idara ya Dayaspora bado haijahusishwa kwa ukamilifu na Sekta ya Afya ya Zanzibar. Hadi hivi sasa ukiangalia ni sehemu moja tu suala la kwenye *dental* na hawa watu wa *HIP* ambao wanasimamia katika suala la Kivunge pamoja na Makunduchi, kina Dk. Firoz nafikiria na wengine ambao ni marafiki na ni watu wa karibu sana wanashirikiana na aliyekuwa Katibu Mkuu, rafiki yangu, kaka yangu Dk. Jidawi. Kwa hivyo, hawa naamini tutumie kitengo cha Dayaspora kwa kuangalia ubunifu gani tunaweza kuwaunganisha na Wazanzibari wanaoishi nje katika Sekta ya Afya.

Pia Mhe. Mwenyekiti, katika haya mazowezi wanaotaka kuja kwa madaktari bingwa au wanataka kusaidia katika vifaa, basi kuwe kuna utaratibu rasmi, sio ma-*document* yawe mengi, lakini kama wanaingia kwenye mtandao nini wanatakiwa wafanye iwe kwa wepesi, kwa haraka na iweze kuleta mafanikio mazuri kwa Wizara ya Afya pamoja na hospitali. Lakini ukiangalia wengine wanalalamika kwamba wanataka kufanya mambo mazuri kuisaidia hospitali, lakini kuna hii *ret* ya *pabirocus* ni kitu gani ambacho kinakuwa katikati hapa. Sasa lazima wepesi uwepo wa kuwaunganisha Wazanzibari na hospitali zetu zote na katika maeneo tofauti. Mhe. Mwenyekiti, naomba nisisitize wakati wanapofanya haya, mengi tusisahau pia kwa upande wa Pemba ili kuhakikisha kwamba pande zote mbili za Unguja na Pemba watu wanafaidika.

Sasa nataka niguse suala la maabara. Mhe. Mwenyekiti, maabara ni sehemu moja muhimu sana ya Mnazi Mmoja. Pale ukienda juu kuna mambo mazuri sana yanafanywa kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Mimi nimekuwa nawasikia humu ndani watu wanalalamika wengi, nakiri kuna changamoto, kwa sababu hii afya ni sehemu moja muhimu, lakini mbona haya mazuri yanayozungumzwa ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja huyasikii nje. Ukienda kule maabara wanasimamia masuala haya ya *matology*, *histopathology* na haya mambo ya *clinical chemistry* wanasomea masuala ya *homons* kuna mambo haya ya *macro biology*. Lakini ukiangalia katika maeneo yote haya wanafanya *test* ya mambo ya saratani, damu na mambo ya *halmons* kuangalia, hayazungumzwi na serikali jinsi gani wananchi wakafahamu mpaka pale wasikie hizi huduma zipo. Kwa hivyo, lazima wananchi waelewe huduma wanazizipata.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapa pana changamoto pia katika hizi maabara zetu. Moja ambayo ni kubwa ni kwamba hatuna *bayomedical engineer* hapa Zanzibar. Mashine inapoharibika kidogo inabidi umuite mtu kutoka Dar es Salaam, na mtu mpaka aje kutoka Dar es Salaam kuja hapa muda umeshakwenda, pengine mashine imeshakaa zaidi ya mwezi. Kwa hivyo, tutafute utaratibu wa kupata *bayomedical engineer* wa kuzisimamia hizi mashine zetu zote. Lakini suala pia la *rays* hizi *chemical* wanazohitaji ili kufanya *test* zao, wakati mwengine zinachelewa sana kutoka bohari mpaka kufika katika maabara. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, ni lazima liangaliwe kwa ukubwa sana.

Kwa mfano, ukiangalia *test* za hizi *clinical chemistry* za *halmons*, karibia mwaka mzima zimelala mashine. Lakini mashine zipo, hizi *reagent* hakuna. Kwa hivyo, mimi nishauri maabara zetu tuhakikishe kwamba tunapata yote haya na zinasimamiwa vizuri na wananchi watambuwe pia huduma ambayo serikali yao iliopo madarakani inawafanyia. Mimi naamini kwamba changamoto zitaendelea kuwepo kwa sababu tunaongezeka na tunahitaji huduma ambayo inaboreshwa, ili wananchi wapate faida na tija kwa ajili ya hospitali wanazokwenda zote.

Jengine ni suala la fedha. Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria tuliyoipitisha hapa Barazani juu ya rufaa ya Mnazi Mmoja, tulisema tulisema kwamba katika ile eneo la fast track watakuw wana *retains* zile fedha, lakini leo ukienda hii mitambo ya *oxygen* ikiharibika tu kidogo wasubiri kutafuta fedha katika sehemu za OC ili waziunganishe huku kupeleka hii mitambo, au katika maeneo mengine madogo madogo. Sasa hivi fedha ambazo walitakiwa wao wa- *retains* Wizara ya Fedha iwaachie, namshukuru sana Waziri wa Fedha yupo hapa ananisikia ninayoyasema juu ya changamoto ya Mnazi Mmoja na naamini atalifanyia kazi kwa haraka ili ile *retain* ambayo inatakiwa isimamie katika utawala wa Mnazi Mmoja asimamie mara baada ya mujibu wa sheria ambao tumeipitisha na naamini katika haya ninayoyasema kabla ya hili baraza halijesha tutapata kujua zaidi ili wananchi wetu na uongozi wa Mnazi Mmoja wasipate hizi kero ndogo ndogo juu ya masuala ya fedha.

Mimi naamini hizi fedha ndogo ndogo wakiwa nazo mambo madogo madogo mengi yatazidi kupungua, ukienda leo pale unakuta wanatumia fedha nyingi sana Serikali katika mambo tofauti mabendeji, mashine ya kuwaka ni pesa nyingi lazima tukiri lakini haitoshi, na kama haitoshi ile ambayo una- *retain* waachiwe waweze kutumia.

Lakini jengine nataka nimalizie Mhe. Mwenyekiti, ni juu ya suala zima la usafi wa hospitali hapa tumezungumza wakati wa bajeti umuhimu wa usafi hospitali nzima ya Mnazi Mmoja, hospitali bado maeneo mengi kwenye vyumba wodi ni kuchagu kwa sababu wananchi wengi wanapoingia na kutoka kuona watu waowanakuwa na michanga, utaratibu uliokuwepo wa kuingia vyumbani kwenda kwenye wodi kuangalia wananchi hakuna nidhamu yausafi wa watu wenyewe binafsi kuhakikisha kwamba wanapoingia katika vyumba na wodi tofauti ili kusimamia usafi mzima wao wenyewe na wale wagonjwa waliokuwepo.

Sijui kama mimi ninachokishauri kitakuwa ni sahihi, mimi nashauri Mhe. Mwenyekiti, Waziri wa Afya pamoja na wasaidizi wake na uongozi wa Mnazi Mmoja waangalie uwezekano kwa mwananchi yoyote anapoingia Mnazi Mmoja ni vizuri kweli kusalimiana lakini watu wasipeyane mikono wanapoingia ndani hasa katika maeneo ya wodi, kwa sababu mtu anaingia anampa mkono huyu lakini hujui ule mkono ametoka nao wapi, huyu mwengine anampa mkono huyu akitoka lakini akishika kwenye ngazi anakamata yale machuma ya ngazi kote, sasa haya machuma kwenye ngazi anapita mgonjwa mwenye damu pengine ana ugonjwa kwenye ngozi anampa mkono mtu mwengine.

Sasa kama kuna ulazima wa kutoa basi tutumie Salam Aleykum lakini iwe kupeyana mikono ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja isifanyike mle ndani na kama tunataka tuendelee na utaratibu huo tuweke zile sababuni na zile dawa ambazo unakuwa unanawa mikononi kama

ulaya unazo, unapangusa kabla hujaingia katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili mwili wako uwe msafi kabisa. Kwa hivyo zile zitasaidia sana ili kulind usari wa wagonjwa kwenye wodi, unaingia katika wodi ambazo watu wameungua, lakini mule ndani hawatakiwi watu wengi kuingia, sasa mimi niliwahi kusema katika kikao cha mwaka jana marehemu babaangu alikuwa mwalimu alivunjika bega walikuja zaidi ya watu 300 kuja kumuona, sasa hiyo nafasi iko wapi mule ndani.

Sasa lazima kuwe kuna utaratibu maalum wa kuingia ndani katika Wodi haiwezekani pahala penye wagonjwa kila mmoja anaingia na kila kitu chake mkononi hatujui wametoka wapi, usafi wao kwa hivyo tuwalinde wagonjwa tuwasimamie wale watu wanaotaka pajengwe eneo maalum pa kusubiri ili rufaa iende.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine kwa kumalizia juzi ijumaa nilifanya ziara kwenye ukuta kwa upande wa baharini nilitoka pale katika eneo lililojengwa kutoa maji ya Mnazi Mmoja, nikatembea mpaka mwisho ya Mnazi Mmoja kuangalia mazingira ya usafi, nimpongeze Waziri kwamba kweli mataka hayatupwi sasa lakini kuna taka ndogo ndogo zinazotupwa za chupa, maboksi lakini kuna vigae vingi ambavyo vina ac*cumulate* katika miaka ya nyuma na vitachukua muda mrefu kuviondoa.Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Mwenyekiti, Waziri mwenye dhamana pamoja na watendaji wake watafute siku maalum ya kuwashirikisha watu wananchi katika jamii mimi mwenyewe pia na wananchi wangu tutajitolea kuja kuokota, naamini pia na kaka yangu Mhe. Ahmada pamoja na Mhe. Suleimani na wengi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakwenda kuokota vigae kule nyuma tusafishe nyuma ya Hospitali ya Mnazi Mmoja na maeneo yote ya mandhari yetu ya hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kuniona na kunipa muda huu kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Tunguu naunga mkono hoja mia juu ya mia ahsante sana kwa kunisikiliza (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Simai kwa mchango wako sasa atafuata Mhe. Ahmada Yahya atafuatiwa na Mhe. Nadir na mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo atakuwa Mhe. Hamad Abdalla Gerei.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie na nitoe mawazo yangu katika ripoti hii ya utekelezaji, mimi si mtu wa dakika

nyingi tano au nne zinanitosha napenda kwanza kumpongeza sana Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapindui kwa kuisimamia kikamilifu Wizara hii. Nakwenda katika nukta ya Mhe. Waziri aliyoizungumza na nimeifurahia sana na hii naomba sana anisikilize kwa utulivu, nimefurahi kusikia madaktari sita au watano ambao kwa bahati mbaya wamepata *infection* ya maradhi ya TB wametibiwa na wako fit, ripoti imeeleza kwamba hawa watu mafao yao yanashughulikiwa.

Ningependa sana Mhe. Waziri tena kwa unyenyekevu mkubwa watu hawa asimamie kwa kipindi kifupi walipwe fedha zao ili waone yale yalikuwa ni ajali kazini, kuna kitu tusingependa kutokezea kitu kinaitwa panda shuka Mhe. Waziri hii mimi mwenyewe nitakuja kuhakikisha hasa kama watu wale wanalipwa ili kidonda kile cha kwanza kimepona cha pili kisiwe cha maumivu kwa kuwa hakulipwa, walipwe pesa zao wajihisi kama na wao wamo ndani ya utaratibu wa kawaida wamelipwa ili watu wengine wawe na imani ikitokea ajali kazini walipwe hiyo nukta ya kwanza.

Nukta ya pili Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 25 wa ripoti hii agizo Na.38 lina mistari 13 lione Mhe. Waziri, lakini jibu lina misitari mitano tu (5) halitoshelezi jibu naomba zaidi ufafanuzi utolewe, hasa ukurasa wa mwisho unaozungumzia kwamba Wizara kulipatia baraza la uuguzi na wakunga usafiri utakaorahisisha kazi yao, *not mention from the original question* kwa hivyo liangalie hilo kidogo litolewe ufafanuzi, kidogo liingie nyama haya masuala ya sentensi zinafika 13 lakini limejibiwa kwa mistari mitano, kwa Hivyo Mhe. Waziri jibu kidogo wakati utakapokuja kujumuisha liwe linaelezea hasa kipengele cha mwisho hicho ambacho ndio kilio sana cha Baraza.

Basi mimi kama desturi yangu dakika zangu ni saba au sita nimemaliza na nakushukuru sana kuwa nimeingia katika orodha ya wachangiaji, tena wala usininyime mimi nikitaka dakika zangu tatu tu hazizidi nakushukuru sana. Naunga mkono ripoti mia chini ya mia ripoti imejibiwa vizuri lakini inataka ufafanuzi mdogo mdogo ili tuweke mambo sawa na kila kitu kimetimia ahsante sana Mheshimia. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Bismillahi rahmani rahim Mhe. Mwenyekiti namshukuru Mhe. Ahmada kwa kuongeza dakika zake chache zilizobakia naomba unipatie mie ili tuendeleze majukumu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir sikuongezi dakika zake nakupa zile dakika kumi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-wardy: Mhe. Mwenyekiti, umesema dakika 15 sasa hivi unanipunguzia naomba kwa hisani yako daika zetu 15.

Mhe. Mwenyekiti, mimi jambo la mwanzo nitaomba kuchangia ripoti ya Afya kama ilivyoletwa na Kamati pamoja na majibu yake, nitakuwa na mchango, nitakuwa na masuali yangu nitaomba Mhe. Waziri aje anijibu atakapokuja kujumuisha.

Lakini jambo la mwanzo Mhe. Mwenyekiti, nitaomba kuzungumzia suala la *Health Insurance* ambayo sasa hivi watu wangi wanatumia Unguja na Pemba kile kikadi ambacho cha afya, ningeomba kumueleza Mhe. Waziri kwamba kadi zile za *Health Insurance* kwamba zinatumika vibaya sasa hivi. Kwa sababu wagonjwa wengi wanapokwenda hospitali sasa hospitali sasa hivi wamekuwa wanachukulia zile kadi kibiashara zaidi kuliko kiafya kweli ni bure, kwamba hospiteli inapotoa service inakwenda kulipwa na *Insurance* baada ya muda ambao waliokubaliana. Mfano mdogo nitatoa Mhe. Waziri apate afahamu mtu anakwenda anaumwa labda na tumbo basi akifika kwa daktari atamuandikia vipimo 20 akapime, wakati mtu anaelezea tumbo atamwambie akapime ishirini ili hospitali ile ipate faida ya vile vipimo ambavyo atakwenda kufanyishwa viwe vingiipate fedha zidi wakati wa kuja kulipwa na *insurance*.

Isitoshe kwenye utowaji wa dawa unaweza kukuta jambo la kumpa mtu dawa mbili anapewa dawa tano na hususan hospitali za *private* ndio zenye tabia hizi nimeshafanya uchunguzi sana, sasa tungelimuomba Mhe. Waziri suala la kadi za Insurance kuweza kuwaita kufanya semina na madaktari wote pamoja na hospitali zote za Zanzibar ambazo ukimaanisha Unguja na Pemba waweze kuelimishwa madaktari hizi kadi za *Insurance* za afya hazijaletwa kwenda kutekeleza kuletea watu madawa kwa wingi au kufanyisha vipimo kwa wingi, mtu atakapohitajika kufanya vipimo vingi basi afanyiwe lakini isiwe biashara aonekane daktari yule amepokea wagonjwa wengi, lakini ametoa madawa mengi na vipimo vingi aonekane kwenye awamu yake aliyokuwepo kwamba kaingiza fedha katika hospitali ile hilo litakuwa ni jambo ambalo sio zuri na kutoa madawa mengi vile vile kwa mtua ambae anaumwa ni hatari kwa afya yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeendelea kwenye suala la mambo haya ya afya kwa kweli ninachotaka kuzungumza kwamba afya ni sadaka kwa sababu hili ni la kujitolea fisabilillahi, kuweko Wizara ya Afya kuanzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi imefika wakati si wa kuwalaumu sana kama watendaji wa chini, mimi ninachomba watendaji wa chini hasa wale ma- nurses madaktari wawe wazalendo kwenye kutoa huduma, wawe wazalendo wawe waaminifu wawe na imani katika kutoa huduma la sio hivyo tutakuja

kuingiza nchi yetu katika janga baya wananchi wanataka kutibiwa wanatukanwa wanatolewa ujeuri.

Lakini ninachotaka kueleza kwamba vitu vile huwezi kumlaumu Naibu Waziri au Katibu Mkuu kila mtu ana majukumu yake, majukumu ya chini yapo kwa watendaji na watendaji kusema la ukweli wanasemwa vibaya na wagonjwa wakienda hospitali ya Mnazi Mmoja, imekuwa sehemu kama vile Chuo cha Mafunzo cha ujeuri na kufukuzwa na kutolewa maneno ni kitu ambacho hakipendezi. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Waziri wachukue hatua ipasavyo kwa watu ambao wananyanyasa wagonjwa kama hivi na nyinyi kama Mawaziri mnakosea Naibu Waziri na Katibu Mkuu tukija tukipata information zetu tutakwambieni humu humu ndani, lakini kwa sasa hivi siwezi kuongeza kwa upande wao kawa sababu sina *information* na uzuri wa mambo haya uzungumze kwa mambo ambayo una uhakika nayo. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimetoa indhari hiyo Mhe. Waziri akae na watendaji wake wa Wizara ili waweze kuangalia wageni wa wateja wanawahudumikia vipi.

Lakini vile vile tumpongeze sana Mhe. Rais tena Dkt. Ali Mohammed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ninachotaka kuwaambia Wizara ya Afya na nchi nzima kwamba wamepata Rais safari hii ambaye anayejali zaidi afya kuliko Wizara zote, tunaona kwamba kila Wizara anaipa fedha inavyotaka na wanafanya lakini Wizara ya Afya imekuwa *extra* inaongezewa, kila siku tunaona bajeti yake inaongezwa hospitali zinaboreshwa mambo yanafanywa vizuri. Sasa tufike hatua sasa ya kutaka kumuangasha mkono Mhe. Rais pamoja na watendaji kwa sababu kila mnachotaka mnapewa sasa hivi mlichobakia ni kusimamia kazi kufanya utekelezaji wale ambao mnahisi kama labda kuna watu wanatoa huduma mbaya au labda wanaingiza siasa katika huduma wafukuzeni kwa sababu suala la afya sio la kuchezea msiijali CCM msiijali CUF kama kuna mtu anacheza na afya lengo lake kumuangusha Mhe. Rais, kumuangusha Makamo wa Pili wa Rais, kuangusha Serikali nzima iliyokuwepo kwa kuitwa jina baya kwa watu watatu washughulikieni.

Kila siku tusije hapa kuzungumza masuala haya kwa haya fanyeni pelekeni watu wenu wachuzeni katika hospitali wanaoharibu watoweni wapo watu wengi wanaotaka ajira, haiwezekani kila siku tukaona Mhe. Rais anaweka fedha ana *invest* kwenye *health care*, halafu huku kuna watu wachache wanaangusha wananchi wanaumia, wananchi wanategemea Serikali Serikali inafanya lakini watu wachache kwa malengo yao wanaharibu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nitalitaka kuzungumza ni suala la UKIMWI ningemuomba Mhe. Waziri, akashirikiana na Wakuu wa Mikoa wote wa Unguja na Pemba kudhibiti haya madanguro wanaongeza ukimwi kwa hali ya juu Zanzibar UKIMWI mwingi

ukiangalia kila mwaka unazidi nchi ndogo itakuja kuteketea. Mhe. Waziri tungekuomba watu wa namna hii wanaofanya biashara zile wakamateni la si hivyo *generation* inayokuja itakuja kuumia Unguja watu kidogo tunataka tuwe wengi hatutaki kupungua.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka kulizungumzia zile gari ambazo zinatoa huduma wanaita *mobile car* wana jina lao wenyewe madaktari wanaziita, ningeomba gari zile kama zipo au hakuna Wizara ikanunua ili ikaweza kwenda sehemu ambazo hakuna hospitali au hakuna vituo vya afya karibu wakaweza ku-*pack* wakaita wananchi wakatangazia wakawapa huduma ya kuwapima pale presha, macho au kuwapa dawa. Vyenginevyo hali itazidi kuwa ngumu kuna baadhi ya sehemu ya vijiji hakuna vituo vya afya wananchi wanaumia, tungeomba mupate yale magari au kama mnayo muanze kupita kwenye vijiji kutoa *service* hizo kuwapa wananchi.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti ningeishauri Serikali imefika wakati sasa kutokana na nchi yetu ipo kwenye utalii zaidi na ina viongozi na ina wananchi ambao wanahitaji huduma ya haraka haraka *emergence*, kuna haja sasa ya Wizara ya Afya kufikiria kununua helikopter na ndege ya *emergence* itayoweza kusafirisha wagonjwa kupeleka Nairobi na sehemu nyenginezo. Tumegundua hapa Unguja tuna watalii tuna wananchi, kuna viongizi tunapopata tatizo inabidi tukodi ndege kutoka Dar es Salaam dola elfu 10 au 13 lakini leo Serikali yetu haitoshindwa kununua kama kaweza kununua mtu binafsi kwa nini Serikali ishindwe wakati *Private Jet* wanaomiliki haifiki dola miloni mibili. Sasa Mhe. Waziri vitu kama hivi ku- invest bilioni tano au kumi au nane helkopter na ndege hata kwa njia ya mkopo kama utakwenda kuongea na Serikali ambazo za ufadhili mulipe kidogo kidogo ni muhimu ndani ya Unguja kuwepo ndege moja na helkopter ambayo ya mambo ya afya, ili litakapotokezea tatizo kuweza kuondosha mgeni akakodi na pia mtapata fedha kwa kukodisha watu sio kwamba lazima itumike bure tu Mtu atakayetumia talipishwa lakini kwa bei nafuu lakini *service* ipo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka kumuhimiza Mhe. Waziri, hospiteli yangu ya Chaani Masingini, hospitali ile ina raia elfu tano mpaka elfu sita ambao Chaani Masingini, Ketwa na Mcheza Shauri wamezunguruka hospitali ile, tungeomba sana kule mnapokwenda kuomba msaada ikiwa mtajenga nyinyi wenyewe kituo kile muhimu sana mkijenge Mhe. Waziri, kina watu wengi zaidi ya watu elfu tano na hasa watu wazima ambao wanahitaji ile afya muhimu sana.

Nashukuru Mhe. Rais kukuwezesha wewe kujenga kituo cha Kikobweni ambacho kipo na mmezidisha lakini kituo cha Masingini kina umuhimu wake kuweza kukijenga upya ili watu wafaidike kuliko kwenda sehemu ambazo za Kivunge.

Mhe. Mwenyekiti, ningezungumza jambo jengine ambalo ninalo Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi alikamata juzi mashoga, kilichonisikitisha kwamba leo nasoma ripoti ya Mhe. Mkuu wa Mkoa kwamba Polisi wamefanya kazi yao vizuri, Mkuu wa Mkoa amefanya kazi yake vizuri wamepelekwa hospitali madaktari wametoa majibu kuwa wale sio mashoga, wakati wao wenyewe mashoga walikubali kwamba sisi mashoga na hichi kitu tunafanya. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri kwa wale madaktari waliofanya hivyo na wana hatari madaktari wa namna hii wanaweza kuja kukataa mambo muhimu ya Serikali kuficha watu ambao wahalifu wawafukuze, wawachukulie hatua wawakamate kwa sababu hali tumeshaiona imeshachafuka. Daktari wanatumiliwa kwa njia ya uongo wamepewa fedha wamebadilisha matokeo.

Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-wardy: Mhe. Mwenyekiti, mimi bado nina mambo kumi naomba dakika zangu saba zilizobakia,

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mhe. Nadir.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-wardy: Mhe. Mwenyekiti, ningeongelea kitengo cha kuzuia vitu faki, ningeomba kitengo hichi kichunguze kwa sababu sasa hivi ndani ya Unguja na Pemba kunaletwa vyakula vingi kutoka nchi ambazo za Ujerumani, UK, France, Canada, Italy na sehemu nyenginezo. Vyakula vile vime *contain* mambo ya nguruwe mafuta ya nguruwe na vitu vyengine, mfano mdogo Malaysia hivi karibuni walikamata *chocolate* za *dairy milk* zina mafuta ya nguruwe na nchi ambayo ina waislamu ni sawa sawa na unguja sasa kuna haja sasa kununua kifaa au kufanya utafiti kwenye vyakula vyote vinavyotoka nchi za ulaya nchi zenginezo ambazo si za kiislamu, ambazo hazina uhalali zikachunguza vyakula vile havina mafuta ya nguruwe au vitu vyengine ambavyo sisi hatufai kuvila.

Kwa sababu tukiangalia vile vile, ulizungumza suala la watu wanaoleta chakula ambacho hakina *date of expire*, mimi ninachotaka kuzungumza tusihadaike na tarehe kuna wafanya biashara wananunua vifaa vile na hasa China na sehemu nyengine wanauza wanazo machine za kutia tarehe maalum, sisi tunachotakiwa kuangalia ni kipimo chetu tunakiamini vipi kitakapofika Unguja, tupasueni polo pimeni msiangalie tarehe angalieni *level* ya chakula iko vipi kwa mujibu

wa machine yenu itakavyokwambieni. Kinaweza chakula kikawa feki matokeo yake ukaona *date* iko nyuma zaidi bado kuisha muda wake, tunachotaka mfanye utafiti kwa vitendo sio kuangalia tarehe.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mimi ninachotaka kuzungumza kwamba uweko mfuko maalum wa hospitali ya Mnazi Mmoja, *pocket money* iweko pale kwa ajili ya wagonjwa ambao inatokezea katika hospitali ya Mnazi Mmoja wanataka kutibiwa lakini wanaambiwa kitu kimekwisha kanunue nje, nnachoomba Mhe. Waziri, aweke mfuko maalum pale wananchi wasitoleshwe fedha kwa sababu Mhe. Rais kashakataza hicho kitu hakuna, kwani nini wananchi wanaambiwa kanunue *bandages* sijui imepungua shindano, tungeomba uwepo mfuko pale pale kitu kimepungua kwenye serikali basi, mfuko uwepo pale pale wasitoleshwe wananchi kwenda kununua. Lakini Mhe..

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Nadir Abdul-latif, muda wako umeisha naomba umalizie.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Ali Warday: Najua dakika tatu zangu zimebakia..

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, naomba umalizie kwa kuunga mkono hoja nimpe nafasi mwenzio.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Ali Warday: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana lakini narudia tena, kwamba watendaji tuwe wazalendo kwenye kutoa huduma ili tuwasa-port serikali ifanikiwe malengo yake. Na vile vile, ripoti hii nai-*support* asilimia 100 japo kuwa sijamaliza nilikuwa sitaki nii-*support* lakini imebidi unanilazimisha namshukuru Mwenyezi Mungu nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadir Abdul-latif nna imani muda mkubwa afya, mfuate Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa yale yaliyobaki ili atakusaidia zaidi nna imani hiyo. Mfuate na hayo uliyonayo yaandike mpelekee na imani na watendaji wake watayafanyia kazi. Mhe. Hamad Abdalla Rashid, mchagiaji wetu wa mwisho.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa kichinja mimba ya uchangiaji.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijachagia ningeomba kwanza nieleze machache ambayo sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tumetakiwa tukisema mambo tuseme ya ukweli na ya uhakika na pengine kama hatuna elimu tuitafute elimu tuelewe kile kinachoelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimesikia kauli hapa za wajumbe ambao wametaka na wametoa kabisa kwamba mgonjwa mtoto kafa tumboni siku saba, hajasafishwa ningependa tuelewe waheshimiwa kusafishwa kuna maana yake na matatizo yake, lakini na kuzalishwa pia kuna maana yake na matatizo yake, kusafishwa mama mtoto aliyekufa mtoto tumboni hasafishwi anazalishwa au anafanyiwa opresheni ya uzazi, kusafishwa yule mtoto ambaye aloharibika kwa utaalamu *abortion* huyo ndiye anayetakiwa kufanywa *evacuation* sasa tunapotowa kauli hapa tuzitowe vizuri, bila ya kujali kusikiliza matatizo ya wagonjwa mbona wao hawaelewi.

Ili mtu asafishwe awe kaharibu mimba, lakini mtu akiwa ana mtoto tumboni anatakiwa kuzalishwa aidha afanyiwe *caresarian section* au upasuaji au *induced* na madawa ya uchungu apate uchungu azae. Sasa katika hilo *priority* ya kwanza sio *operation* ya kwanza *induction* mama apate uchungu ili ajifungue mtoto aliyekufa, mtoto aliyekufa anazaliwa nilisema niseme hayo ili tuwaache wananchi wasije wakawa na uchungu na hospitali yao ya Mnazi Mmoja wakaona ni hospital ya uuwaji, sio kweli nikutoka kujua na kutokufahamu tu, ile dawa ya uchungu unaweza kupewa hata siku tatu bado inaendelea mama bado hajapata *contraption* za kutosha na ile njia ya uzazi ikafunguka akazaa. Sasa tuseme tabu hilo Mhe. Mwenyekiti, baada ya haja nakuja katika kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na Kamati ya Wizara hii kwa mambo ambayo wameyaona kitaalamu kabisa, na ambayo haya tupo pamoja na tukiyafanya kwa pamoja basi tutafika katika lengo letu na kuhakikisha kwamba Wizara ya Afya Zanzibar, inawasaidia wagonjwa na tunafika katika hatua ambayo serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein inafikiya na lengo lake iliyofikia.

Mimi nichangie machache tu, na naanza na nyumba za wafanyakazi kifungu cha 4 agizo la nne lile, naishukuru Kamati kwa kutoa agizo lile na mimi nasema kwamba naisaidia wizara pia kwamba ni muhimu kuwa na nyuma za wafanyazi karibu na maeneo ya hospitali. Ni tabu na ni matatizo kabisa hospitali kutokuwa na madaktari wanaokaa pale maeneo ya hospitali, kwa sababu hospitali ni mahali pa huduma za haraka na nyengine haidhuru za kawaida, lakini zinapokuja za haraka na madaktari wakawa hawakaii pale, basi tatizo linabakia pale pale na hii napenda kumuomba Mhe. Waziri, hata kule Pemba hospitali nzuri ya Abdalla Mzee, miye sifichi naumia roho kuona madaktari wanakaa Chake Chake na ningeomba Mhe. Waziri, Mkoani nyumba za kukodi madaktari zipo na kwa taarifa yake zimeshakodiwa lakini walikodiwa Chake Chake kwa njia tu ya kuitia harasa Serikali. Na ningependa kusema Serikali inaingia hasara kweli, naomba Mhe. Waziri na watendaji wako tukakodi nyuma Mkoani zipo kama hamzijui nichukueni nitakuonesheni nyumba za kukodi. *(Makofi)*

Na nasema hivi kwa nia moja tu, yakuokoa fedha za serikali ambazo kila siku zinatumika magari ya kukodi nashukuru waziri kajitahidi mpaka kapeleka gari za wizara sasa, lakini bado mzigo wa wizara unaelemewa na upotevu wa fedha tukakodi nyuma Abdalla Mzee, madaktari wakae pale ili wagonjwa wetu wapate huduma za haraka pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hilo niende kwenye changa moto zilizopatikana, agizo namba 5, na mshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa hatua kubwa na nzuri na bidii hasa wanazozichukua katika kutekeleza changamoto kila wanazozipata miye nashukuru wanazichukulia hatua na juzi nililalamika hapa lakini kweli kabisa, lakini tatizo linakuja pale na sisi utupe taarifa baada ya hatua. Mnapochukua hatua baada ya kukupeni changamoto turejesheni mrejesho kwamba pale baada ya tatizo lile, tumechukua hatua hii. Ili tuweze kuwaunga mkono, na tuweze kuelekeza kama kuna hatua zaidi na sisi tutapendekeza.

Mhe. Mwenyekiti, nende chap chap dakika ni kumi tu, wafanyakazi wachache mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri hapa heee kama kuna wafanyakazi wachache Pemba kunatisha, Mhe. Waziri, Pemba kuna nesi wanaingia kazini masaa 24, na kama unataka ushahidi nnao *roster* nnazo, masaa 24 na naomba katika huu uwajiri mpya nimepita juzi, kuna uajiri mpya

nimesikia nongo nongo sina uhakika katika muda ule inaonekana Pemba ni wachache mno, Unguja ni wengi mno Mhe. Waziri, nakuomba katika mgao ule kama si nusu basi angalau kasorobo, isiyekawa mia 200 kwa kumbi na mbili nakuomba Pemba kuna matatizo ya wauguzi hata ma *orderly* sasa hivi eeee ni jambo la ajabu *orderly* sasa anapika jikoni. Anavua *glove* anakwenda kupika kwanza kupikia wagonjwa Mhe. Waziri naomba unione hili. Vitongoji nenda kaangalie *orderly* wanavulishwa *glove* wanakwenda kupikia wagonjwa kwanza kwa tatizo kwa tatizo la wafanyakazi wachache.

Mhe. Mwenyekiti, niende mbele nakuja chap chap kwa sababu dakika ni kidogo, uambukizwaji wa wafanyakazi wakiwa ndani ya kazi napenda kupongeza Kamati imeliona hili, lipo Chake Chake na Mheshimiwa kwa masikitiko yangu makubwa yule mfanyakazi hana TB tu, ana TB na kitu kinaitwa *hepatitis* B *very infectious diseases* ni maradhi hatari ya kuambukiza *hepatitis* B, lakini la kusikitisha yule mfanyakazi bado anafanya kazi namuomba Mhe. Waziri, pamoja na mafao waliosema wajumbe wenzangu wapatiwe lakini pia tumpumzishe, nia yetu ni kutibu sio kuambukiza *hepatitis* B inaambukiza sana, tumpumzishe mfanyakazi wetu, tumpatie mafao yake kama alivyosema Mheshimiwa wenzangu mjumbe hapa ili tumpe moyo na hii yote inatokana na ule uhaba wa wafanyakazi tatizo la wafanyakazi Pemba narudia tena Mhe. Waziri hususan wauguzi ni zito kubwa halina mfano.

Jengine Mheshimiwa kwenye Kamati walipendekeza hapa kuajiriwe wataalamu tena wapate msisitizo hasa hasa madaktari mimi nasema Mheshimiwa hasa hasa wauguzi, wauguzi hospitali yoyote duniani inaweza kwenda bila ya madaktari lakini ikiwa hapana uuguzi nakuthibitishia Mhe. Mwenyekiti na Mhe. Waziri, hospitali madaktari watupu hawawezi kuiendesha, kwa nini muuguzi ndo mtu ambaye anakaa na mgonjwa masaa 24, muuguzi wa asubuhi anampa ripoti muuguzi wa mchana ripoti za wagonjwa lakini wa mchana anampa ripoti muuguzi wa usiku daktari anapita asubuhi tu, na hawezi kufanya chochote mpaka apate maelekezo kutoka kwa muuguzi mgonjwa huyu kalala hivi, ana matatizo haya katoka damu muhimu kapata tetesi vibaya ndo daktari anapata muongozo wa kutibu. Mheshimiwa narudia tena naomba wauguzi na kama hayo mafao mazuri basi na wauguzi wapewe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie mwisho kwa hospitali ya Chake Chake hospitali, hospitali ambayo mie inanitia huruma kweli nikifika pale nakaribia kulia naishukuru Kamati imeona tatizo la maji pale nimesema kupelekwe tank, Mhe. Mwenyekiti, hakuna hospitali haya moja Unguja na Pemba ambayo ina ma tank makubwa ya maji kama hospitali ya Chake Chake mimi naijua ndani ya nje nakubali waziri kasema kumewekwa *machine special* ya pale mimi narudia kusema kwamba ile *machine* ya *special* ipo toka zamani, tatizo ni usimamizi tu.

Nilikuwa Katibu wa hospitali ya Chake Chake, kuna *machine* pale lakini bado stil hospitali kuna machine ya dharura ya kuendea kwa *diesel* sio umeme ukizimika umeme yetu wenyewe ya hospitali ipo pale tatizo ni usimamizi mbovu wa upandishaji wa maji kuleta pale Chake Chake hospitali kuna tank mbili kubwa zinatosheleza kabisa Mhe. Waziri nakuomba twende pale tufanye usimamizi mzuri ili tuhakikishe wagonjwa wetu wanapata maji mtulivu wa kutosha, ili kukimbiza hii uambukizaji ili kuhakikisha kwamba maji yanatoka saa 24 baada ya hayo naipongeza hii hotuba vizuri nimechangia vizuri, na naomba na naipasisha kabisa kwa asilimia 100 naikubali haina tatizo twende na usimamizi tu, mzuri kuanzia maji mpaka kuwasimamia

wafanyakazi inaonekana dhahir kwamba haiwezekani *Global* wauguzi wake wanafanya vitu vizuri, wa Mnazi Mmoja wasifanye, hiyo haiwezekani.

Mhe. Waziri, haiwezekani *CT SCAN* ya Mnazi Mmoja inaharibika kila siku ya *Global* ya miaka mitatu haiharibiki, haiwezekani, haiwezekani vifaa vyetu vya Mnazi Mmoja vinaharibika vya *Global* haviharibiki haiowezenaki twendeni tukajipange tuondowe muhali tusimamie wafanyakazi wafanye kazi inavyotakikana. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamad Abdalla Rashid kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Afya na baadaye tumpishe Mhe. Waziri wa Afya kwa ajili ya ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na wajumbe.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Awali ya yote napenda nichukue nafasi hii, kumshukuru Mwenye ezi Mungu mwingi wa rehma aliyetujaaliwa uwepo wetu hapa.

Lakini pia nafasi ya pili nichukuwe nimshukuru Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uwezo wake Mwenye ezi Mungu aliyompa na kuweza kusimamia ipasavyo huduma za Wizara ya Afya.

Mheshimiwa sote ni mashahidi kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar jasho lake kubwa linapotea katika kushughulikia huduma ambazo zinawafikia wananchi ikiwemo huduma katika Wizara yetu ya Afya. Mheshimiwa nachukua pia nafasi adhimu kukushukuru wewe pamoja na Mwenyekiti mwenziwe lakini pia Mhe. Spika pamoja na Naibu Spika kwa uongozi wenu mnavyotuongoza kwa ukarimu, kwa hekma na busara katika Baraza letu hili hadi kufikia katika hatua hii tuliyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda nizungumze machache na mengi atayazungumza Mhe. Waziri wangu. Na naanza kuzungumzia kuchangia kwa kufafanua kidogo, yale waliyoyaeleza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na ninaanza na Mhe. Omar Seif Abeid (Mwakilishi wa Jimbo la Konde).

Mhe. Omar Seif alizungumzia kuhusu hospitali ya Chake Chake kwamba iangaliwe kwa kina na kwamba huduma zinapatikana vizuri lakini hospitali yenyewe haiko vizuri inatakiwa ipatiwe ukarabati. Mheshimiwa nataka nimueleze Mhe. Mwakilishi Omar Seif pamoja na Baraza lako Tukufu, kwamba Wizara yetu ya Afya imo katika hatua za kufanikisha matengenezo makubwa ya hospitali ya Chake Chake na matengenezo hayo yamesharidhiwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na tumesharidhiwa kupatiwa shilingi milioni mia nne kwa ajili ya matengenezo ya hospitali hiyo.

Kwa hiyo namuomba aridhike na asubiri matengenezo hayo yatakapopita ili tuone mafanikio makubwa yatakayopatikana kwa ukarabati huo. Lakini la pili alisemea sana kuhusu kituo chake cha afya kilichopo Konde, kwamba hakina alimtetea kuna kijana na huyu mara nyingi anamzungumza sana hata miye ameshawahi kunambiya kwamba anaomba arudishwe katika kituo kile ili atowe huduma, inaelekea kijana huyu ni kijana ambaye anatoa huduma ipasavyo katika kituo kile na anamuombea arudishwe. Mhe. Omar Seif nakuhakikishia kwamba tutakapomaliza tu kikao hichi, tutaanza kulishughulikia hili na kuhakikisha kwamba kama

hakuna matatizo mengine ya kiutumishi ambayo anafanya asirudishwe katika kituo kile, basi wizara yangu itachukua jukumu la kumrudisha kwa manufaa ya wananchi wa Konde.

Mheshimiwa suala lake la tatu lilikuwa linahusu vitendea kazi, alisema kwamba vitendea kazi katika vituo ikiwemo kituo chake cha Konde na akatolea mfano B.P machine kwamba ni mbovu na hakuna baadhi ya vituo. Mimi nataka nimueleze Mheshimiwa kwamba juzi kama mniliona katika ziara yangu nilokuwa natembelea Bohari ya Madawa katika mambo ambayo nimeyakuta pale na vifaa mbali mbali na hizi BP machine nimezikuta ziko kwa wingi kwa hiyo nilikuwa naomba mridhike kwamba, katika vituo ambazo hazipo kunawaomba wale ambao wanafanyakazi, wafanyakazi wa vituo vile kwanza wanaufahamu utaratibu wa kuviomba vifaa hivyo.

Kwa hiyo kama hawajaviomba tunaomba waviombe kwa sababu vifaa havipelekwi tu ovyo ovyo, ni lazima vipite kwenye utaratibu maalum na kwa bahati nzuri watendaji wa vituo wote wanafahamu utaratibu wa kuvipata vitu hivyo, sio tu kulalamika wakienda Wakilishi kwamba hatuna B.P machine, hatuna nini aa waombe ili waone kama watanyimwa vifaa hivi ambavyo vipo. Mhe. Mwenyekiti, jengine alilolisemea Mhe. Omar Seif ilikuwa ni kuhusu kituo cha Afya Mkia ng'ombe, Mheshimiwa ni kweli kwamba kituo hichi kina changa moto nyingi ikiwemo za usafiri kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

Wizara imeliona hili na tunalichukua kama ni pendekezo hasa kutokana na ugumu wa kulifikia eneo hilo kwa baadhi ya siku, hususan wakati wa masika. Wizara itaangalia kwa kina uwezekana kwa kutoa baadhi ya huduma za kituo cha Daraja la pili yaani PHSU+ kama tulivyofanya kwa baadhi ya vituo vya aina hii, kwa mfano huduma ya uzazi, na huduma ya maabara. Mheshimiwa lengo la serikali ni kufikisha huduma bora za afya katika vituo vyote ili wananchi wafaidike na huduma hii. Kwa hiyo tunakuhakikishia na tunalihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba tutafanya kila itakavyowezeka kuhakikisha vituo hivi ambavyo huduma zake hazijatulia tunazifikisha na ndio lengo la serikali na in sha llah tunamuomba Mwenye ezi Mungu ataujaalie tuweze kulifikia lengo hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nianze kumgusa kwa michango Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwakilishi la Jimbo Mgogoni. Mhe. Shehe Hamad alisema mambo mengi lakini mimi nitaka nimjibu jambo hili moja mengine atayajibu Mhe. Waziri wangu, Mhe. Shehe Hamad alisemea suala la wafamasia, kwamba hawako Pemba au waliopo wachache au hakuna kabisa.

Mheshimiwa napenda nilieleze Baraza lako Tukufu, kwamba kwa sasa kuna mfamasia mmoja na wasaidizi wafamasia kumi na mbili, ambao tayari washaajiriwa na wanafanya kazi Pemba, hata hivyo Wizara bado inaendelea na utaratibu wa kuajiri wafamasia wengine ambao, baadhi yao pia wataelekezwa na kufanya kazi Pemba katika uajiri wao.

Mhe. Mwenyekiti, lengo narudia kusema kwamba lengo la serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, ni kufikisha huduma bora za kijamii ikiwemo huduma za afya na wananchi na kwa karibu zaidi, hivyo wizara tutafanya kila litakalowezekana kuhakikisha tunafikisha, tunakamilisha, tunatekeleza lengo hili kwa niaba ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim Ayoub alisema mambo mengi, lakini pia aligusia jambo la kuhusu hichi, jambo p alilolizungumzia Mhe. Hamad Abdalla kwamba mtoto kafia tumboni na leo ni ya nane hajasafishwa, Mheshimiwa hili sitaki nilikusudia nilieleze kwa kadri madaktari wangu, wataalamu wangu kwenye wizara wanavyonielekeza lakini kwa sababu Mhe. Hamad Abdalla Rashid kalieleza kidogo mimi nilikuwa nataka nitowe tu tahadhari na indhari kwa wananchi ambao wanatusikiliza. Mheshimiwa wananchi wengi au baadhi yao wanakataa kufuata huduma za afya katika vituo vyetu vya Serikali kutokana tu na maneno maneno ya kuokota oktaba.

Mheshimiwa ni ukweli uliodhahiri huduma zinazotolewa katika hospitali zetu za Serikali ikiwemo Hospitali ya Mnazi Mmoja ni huduma bora na hazilinganishwi kabisa na huduma zinazotloewa katika hospitali zetu za *private* wananchi ambao hawaitakii mema Serikali yetu huokotaokota taarifa za kuokota ambazo nyengine hazina ukweli wakaanza kuzizungumza kwenye matanga, wakaanza kuzizungumza kwenye maharusi yetu, wakaanza kuzizungumza kwenye magari tukiwemo kwenye usafiri kwamba natolea mfano Hospitali ya Mnazi mmoja wanapigwa, wanapigwa makofi, wazazi wanapigwa vibao, wazazi wanachunguliwa, wazazi Mheshimiwa yake mengine huwa sio kweli ni maneno tuu ya kisanii ambayo wanayafanya wananchi kwa lengo la kuipotosha Serikali.

Wale ambayo wanazalia wanapata huduma za uzazi katika hospitali zetu za Serikali ikiwemo Hospitali ya Mnazimmoja wao wenyewe wanathibitisha kwamba wanapata huduma zilizo bora, nina kawaida ya kufanya ziara katika hospitali na hasa Hospitali ya Mnazimmoja na kumuuliza mzazi mmoja mmoja hebu nielezeni huduma mnazozipata hapa mnaridhika nazo, hawasemi na *sometime* huwa nawatoa madaktari wote na manesi nawauliza peke yao hawanambii mimi kama tunasimbuliwa tunapigwa lakini wanakiri kama wanapata huduma zilizo nzuri. Matokeo yake maneno maneno haya ya kuokota yanawafanya wale wananchi ambao ni masikini hawana uwezo wa kwenda katika Hospitali ya *Global*, hawana uwezo wa kwenda Hospitali ya Al Rahma, hawana uwezo wa kwenda hospitali zozote za kutoa pesa wachange mtu anachanga kwa kunieleza mwanamke ananiambia miye nimeanza kuchangia kuweka kibubu changu nikiwa na ujauzito wa mwezi mmoja nadundukiza pesa ili nihakikishe nakwenda kuzaa hospitali ya *private* kwa kuogopa kadhia iliyopo katika Hospitali ya Mnazimmoja.

Wanawafanya wasumbuke wapoteza pesa nyingi kwenda kufuata wakati huduma zile wanazipata katika huduma zile wanazipata katika Hospitali ya Mnazimmoja tena za bure kabisa. Nilikuwa nawaomba sana waheshimiwa mtu ajaribu aone baadaye ndiyo akatae, huduma zinazotolewa katika hospitzali zetu za Serikali ni nzuri, ni bora na zina mafanikio makubwa sana wasilinganishe huduma hizo zilivyokuwa zamani na sasa, sasa kuna mabadiliko makubwa katika Wizara yetu ya afya. Nawaomba sana wananchi mutumie vituo vyenu vya afya lakini pia mutumie hospitali katika kupata huduma za afya.

Mwisho napenda tuu nifafanue kidogo hii ya Mhe. Jaku kama alivyoeleza Mhe. Hamad Gerei kwamba si kama mtu mtoto akishafia tumboni pale pale utasafishwa au utafanywa nini, utaratibu wa wataalamu wanavyotueleza sisi ambao sio wataalamu huwezi kusafishwa mtoto yule anatakiwa azaliwe kwa njia ya kuzaliwa pale imeshindikana kabisa ndio wewe utafanyiwa *operation* azalishwe mtoto yule kwa njia ya *operation*.

Kuna hatua za hatua na ndio maana wataalamu wanampa siku nane au siku kumi wengine wanapewa hata wiki mbili nenda nyumbani kakae wiki mbili tumia dawa hii na hii baadaye njoo. wiki mbili zile ukiambiwa kakae nyumbani si kama umetelekezwa na madaktari isipokuwa anakupa muda anajua itafika wakati uchungu utakuja na njia itafunguka na wewe mwenyewe unaweza kumzaa salama kabisa bila ya *operation.* Sasa tusilazimishe kwamba kwa nini siku nane hajazalishwa siku nane aha madaktari nao wanautaratibu wao wamesoma, wamepata madegree, wamepata elimu ya kutosha, naomba tufuate maelekezo yao tusiwapoteshe wananchi wakafanya mambo ndio pale wananchi wanapokwenda kutafuta majani, akatafuta miti ambayo haipaswi kula akala matokeo yake yakamjia matatizo akapotoza maisha.

Mheshimiwa mwisho kabisa mimi napenda nichukuwe nafasi hii pia niwashukuru kwa dhati kabisa wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa ushauri na maelekezo yao ya kila siku wanayotupa kuhususiana na Wizara ya Afya. Waheshimiwa tunakiri kwamba maelekezo haya mnayotupa ushauri huu mnautupa na ndio ambao unatusaidia na hadi sasa hata nyinyi ni mashahidi kwamba kuna mabadiliko makubwa katika Wizara ya Afya.

Mheshimiwa naomba nichukuwe nafasi hii kukushukuru pia wewe kwa kunipa nafasi ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Afya, Mhe. Mahamoud Thabit Kombo naye aje amalizie.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nakushukuru na mimi nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe pamoja na watendaji lakini zaidi niwashukuru Kamati ya Ustawi wa Jamii pamoja na Mhe. Tatu Mohamed Ussi ambaye aliwasilisha yale maelezo kwa niaba ya Kamati nzima pamoja na wajumbe wake wote lakini naomba pia niwashukuru sana waheshimiwa wafuatao nitaomba niwataje walichangia moja kwa moja na pia nitawataja waliochangia waheshimiwa kwa maandishi.

Naomba nianze kumtaja

1. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
2. Mhe. Omar Seif Abeid
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
5. Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata
6. Mhe. Simai Mohammed Said
7. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
8. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
9. Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei)

Mhe. waliochangia wengine kwa maandishi

1. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
2. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
3. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame

4. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
5. Mhe. Suleiman Makame Ali
6. Mhe. Naibu Waziri wa Afya

Mheshimiwa kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti nikubali na kukiri kuyapokea yote yake tulioshauriwa, yale yalopendekezwa, yale ya kuendelea kufanyia kazi kwasababu hii ni wizara ambayo daima imo kazini na inatakiwa katika kazi saa ishirini na nne kwasababu mtu yoyote anaweza kuumwa wakati wowote hata sisi tuliokuwemo humu ndani mtu yoyote Mwenyezi Mungu atuepushie, atukinge, atulinde lakini wakati wowote unaweza ukaanguka na huduma ya mwanzo kabisa utakayohitaji binadamu ni huduma ya afya.

Pili naomba tupokee zile pongezi mlizotupa zote tunashukuru kwasababu pongezi hizi zinatatupa moyo sisi pamoja na madaktari, pamoja na wauguzi, pamoja na watendaji wetu wote na wale milowasema pia kwa ujuba, ujeuri naamini wamesikia wataendelea kujirekebisha na wale waliokuwa hawajajirekebisha na sisi tutaendelea kuwachukulia hatua nalitamka wazi hili mbele yenu maana mmewasema baadhi yao kwamba bado hawajirekebisha nao pia tunaendelea kuchukua hatua, hapa tulipo sio kule tunapotokea kidogo kuna *improvement* ambayo imeonekana.

Lakini jengine naomba nizipokee pia pongezi ambazo Mhe. Rais mumempa moja kwa moja na ninaamini atakuwa kazisikia mwenyewe na Inshallah tutazifikisha pongezi hizo. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yumo humu ndani na yeye atazifikisha pongezi hizo kwa wingi sana kwa Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wetu mpendwa kwa jitihada, juhudi, nguvu, fedha na mambo mengine yote anayoingiza katika hii sekta ya afya nakubaliana na nyie kwa asilimia moja kwa hili wala sikatai, wala sina sababu ya kukwepa maana mzigo uko mkubwa mbele kwasababu ikiwa Mheshimiwa Kiongozi wa nchi anaingiza kiasi kikubwa namna hiyo na ile sekta inatakiwa pia ionekane inabadilika kwa kiasi kikubwa na hiyo ndiyo jitihada yetu ambayo sisi tunaendelea kuifanya usiku na mchana kwa saa ishirini na nne. Sekta ya Afya hailali inafanya kazi saa ishirini na nne kwa hiyo hizo pongezi tutazifikisha.

Lakini kubwa zaidi naomba pia niwapongeze akina mama wawili ambao hamkuwataja hawa pia ni mstari wa mbele sana katika Wizara yetu ya Afya wa kwanza kabisa ni Mama Mwanamwema Shein mwenyewe hamkutaja huyu mama lakini huyu mama yuko mstari wa mbele sana kutusaidia kwa hali na mali na pindipo panapotozea tatizo lolote huwa anakuwa mbele sana kutusaidia, ni mama yetu mpendwa yeye pia anatokea katika fani hiyo hiyo ya Wauguzi na Wakunga na alishawahi kuwa Muuguzi Mkuu pale Hospitali ya Mnazimmoja. Kwa hiyo naomba tufikishe sana kwa upande wetu sisi Wizara ya Afya tufikishe sana pongezi zetu kwake.

Lakini pia naomba kumshukuru na kumpongeza Mama Asha Balozi ambaye pia amekuwa mstari wa mbele kabisa kutusaidia pale panapotokezea changamoto ama kasoro ya hapa na pale amekuwa mama huyu mstari wa mbele kabisa katika kutusaidia kwa hiyo nawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, nitajitahidi kutoka mengine mengi Mhe. Naibu Waziri ameshaeleza lakini nitajitahidi kwenda kwa yake muhimu ambayo yemeguswa na nitaanzia kwa mchangiaji wa mwisho kabisa Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerey) alipochangia na kuja kwa mwanzo.

Kwanza namshukuru sana Mhe. Gerey kwa mchango wake kwa kweli kutupa darsa hilo ndio darsa alilotua ni darsa kamili Mhe. Naibu Waziri amelieleza na mimi naomba kila unapopata fursa hii ya kunyanyuka uwe unatoa darsa, wewe bado ni mfanyakazi wa Wizara yangu ya Afya mpaka leo uko likizo bila ya malipo na usipotoa darsa nitakufuta kule maana watu wa likizo bila ya malipo waliochukua muda mrefu tunawafuta kabisa tunawaambia sasa hawa waondoke. Kwa hiyo uendelee kututolea darsa, uendelee kutupa darsa wewe umetoka huko umeingia katika kiriri cha siasa umo humu ndani kwa hiyo, wajibu wako na sisi kushirikiana pia katika kutoa elimu ya afya, nakushukuru sana kwa darsa uliotoa na niseme tu kwamba ni kweli pahala unapokuwa mgeni wakati mwengine lazima kidogo uliwe na hii ni ithibati popote unapokwenda ikiwa mgeni kidogo lazima upate kidogo changamoto.

Tulipokuwa tunahamia pale Hospitali ya Mkoani *staffs* wengi sana walitokea hapa Unguja kwasababu kulikuwa hakuna idadi ya kutosha ya *staff* Abdalla Mzee pale wakati Mhe. Rais alishatoa agizo kwamba tarehe fulani mimi nataka Hospitali ya Abdalla Mzee tuifungue alisema hivyo na sisi ilibidi tufanye kazi kwa agizo lile, kwasababu hospitali ilishakamilika sisi tuliwa tunahangaika kutafuta wafanyakazi, lakini tutakwenda kwa agizo hili popote walipo kuwepo hawa wafanyakazi tutaondoka nao.

Sasa tulipofika pale na mimi pia nilifika katika hiyo timu tulifika pale hata hoteli sisi tulikosa tulikuwa hatuna hoteli mimi nilitaka kukaa Mkoani tulikuwa hatuna hoteli pale tulikuwa tunakaa Chake Chake tunakuja pale tunafanya shughuli zetu tunarudi. Hoteli ya kukaa na hii mimi nitafurahi sana nikija mara ya pili twende pamoja uoninesha bwana hapa pako pa kukaa na ndiyo dhamira kuu ya agizo la Mhe. Rais kujenga pale nyumba za *staffs*, kwa sababu tulikodishwa pale nyumba moja kubwa hivi ambalo halijamalizika tukachukua sisi jukumu tukasema tunalimaliza na kadhalika tunafanya mambo yote pale, mwisho wa siku hatujafanikiwa mwenyewe akaghairi akasema sasa mimi sitaki nyumba yangu.

Na mnajua Waheshimiwa siasa iliingia kati tuambizane ukweli tusitafune maneno kuna siasa kali ambayo iliingia kati, mwenyewe anakupa nyumba akishakupa nyumba mumesainiana mkataba vizuri mshalipana anaondoka hapo anageuka anakwenda kulaumiwa kwenye familia yake anaambiwa wewe kwanini umewapa nyumba wale, sitaki kusema mengi zaidi lakini kuna mikataba ambayo mengine tulishatiana sain pale ilibadilika. Sasa kama waheshimiwa mnakuwa na taarifa hizo za pahala kama nyumba ya mtu ambaye yuko tayari ameridhika iko tayari kwa ridhaa yake kutukodisha basi sisi tuko tayari tutakodi. Kwasababu sisi madaktari tunapenda wakae pale sababu kuu tatu. Kwanza kunakuwa na *accessibility* ya saa ishirini na nne kwa yule daktari anapohitajika kwa *emergency* yoyote daktari yule anafutwa nyumbani anaamshwa kama kalala anatoka usiku anakwenda kufanya kazi ya kwenda kutoa matibabu.

Lakini ya pili tunatumia gharama kubwa katika zile *minibus* ulizoziona, nashukuru kwa kuziona zile *minibus* tumezinunua tunatumia gharama za petroli kwenda na kurudi wakati mwengine ishatokezea mara kadhaa daktari keshafika nyumbani kwake ndio kwanza katua kuna *emergency*. Ile gari inabidi irudi na nyie petroli bei yake mnaijua, kwa *trips* hizo petroli kiasi gani tunatumia nyie mtakuwa mnajua na lita ngapi zinatumika na gharama ambazo pesa zile zingeweza kutumika katika huduma nyengine moja kwa moja kwenye hospitali. Kwa hiyo uwamuzi wa kujenga hizo *flat* 96 yaani kutoka na vyumba 96 katika hizo *flat* zitakazojenga huo tayari umeshafanyika na tuko katika hatua nzuri.

Mhe. Shehe Hamad Mattar ameuliza mbona tokea Julai haya ni mambo ambayo yanaendelea bahati nzuri ule waraka uliokuwa unahusiana na ujenzi huo nimekuja nao tunafanya *feasibility* tukimaliza *process* hizi Wachina wanakwenda wakirudi, wanakwenda wakirudi, anakuja kupima wanachukua udongo wa pale wanaangalia ni kidogo *process* ambayo inachukua muda mrefu haianzi moja kwa moja.

Lakini tunashukuru upande wa SMZ mchango wetu alotwambia wachina tunakiwa tutoe sisi tayari pesa ile kasma tumeshaitenga kwenye bajeti. Kwa hiyo sisi tuko tayari hivi sasa tunawasukuma wenzetu wa Serikali ya Watu wa China ili msaada ule kwa upande wao ufike mapema zaidi na Mwenyezi Mungu akitujaalia tutafanikisha. Lakini kama kuna nyumba pale basi naomba waheshimiwa msikae kimya au mkasubiri mpaka kwenye viriri hivi mkazungumza mtujie, mtuambie, mtunong'oneze tuko tayari kuzichukua hizo nyumba.

Kuhusu wafanyakazi kugaiwa wafanyakazi wanaendelea kugaiwa vizuri katika wafanyakazi hawa kuna wafanyakazi wachache nao wanapelekwa Pemba, lakini tatizo kubwa tuliokuwa nalo Pemba na hili naomba Waheshimiwa Wawakilishi wa Pemba mtusaidie. Kuna tatizo kubwa sana Pemba na kule nilipokuwepo Pemba nilipiga hotuba kidogo nilipiga siasa na baadaye nikapiga na hotuba, pale nilipotembea Abdalla Mzee mara ya mwisho kuna madaktari wetu kama wanne vijana wabichi na wao hawakuowa bado, nikawambia pale Abdalla Mzee wakati nawahutubia na wakikuwepo wazee wengi siku hiyo nikawaambia fanyeni hawa madaktari wabakie hapa maana humu yameelezwa madaktari wengi wanaokwenda kule wanasema ndoa zao zitakuja kuvunjika inabidi warudi huku, mtu akipelekwa tu anakwambia anataka kurudi lakini anaokuja Unguja mbona hasemi anataka kurudi Pemba.

Mhe. Omar Seif Abeid hayupo naona amezungumzia *staffs* wake wa Konde *staff* wake wa Konde kweli amekwenda kusoma amemaliza amerudi na nashukuru amelitaja hilo na huyo *staff* nimecheki kweli yupo amesharudi sasa hivi tunafanya ufuatiliaji ili arudi kule Konde, sasa hapo akikataa nitamfuata na yeye mwenyewe tumwambie je, unaona mfano huu, naamini hatokataa lakini kuna tatizo hilo sasa sisi tuliokuwa tunapiga siasa kule tukawaambia wazee wa pale wawatayarishie mazingira mazuri wale vijana ambao hawakuowa ili wapate wake kule kule waweze kukaa pale pale kwa Pemba. Kwa hiyo naamini waheshimiwa wawakilishi hasa mnaotoka katika majimbo ya Pemba mtaweka vivutio vikubwa zaidi kwa vijana ili wabakie kule wasitake kurudi Unguja kwa sababu tatizo hilo lipo kweli.

Jengine Mheshimiwa maswala yote uliyochangia tumeendelea kuyapokea na kuyafanyia kazi vizuri. Kuna swali la Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil aliniuza kile kipengele cha hoja ya 38 ni kweli maandishi yako machache sana lakini katika maelezo yangu kama utakuwa umechunguza nilitoa maelezo mapana sana katika eneo hilo na eneo hilo zaidi linazungumzia kuhusu nidhamu, maadili, heshima ya wauguzi na fani yao na kile kinachofundishwa katika Chuo ch Afya nilieleza katika vyuo vyengine mbali mbali vyote. Kwa hiyo hayo yote kwa pamoja nilieleza katika maelezo yangu sio kwamba tulikusudia yawe machache lakini naomba yapokelewe kama yalivyokuwa na upana wake kwamba hili tunaendelea kulifanyia kazi suala la maadili tayari machapisho yashatolewa. Sheria ya Utumishi wa Umma inazungumzia kuhusu maadili na kuna kanuni ambazo tumezisaini juzi ziko katika Sheria ile ya Mnazimmoja kuna kanuni zake....

KUWEKA KANDO KANUNI YA MUDA

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri samahani kidogo naomba niwambie wajumbe kuwa muda wetu tumebakia na dakika tano na Mhe. Waziri bado hajamaliza majumuisho. Kwa hiyo naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ atoe hoja kwa kutengua kanuni ya muda.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naomba kutowa hoja kuweka kanuni ya 23 kando kanuni ya muda ili tumpe nafasi Mhe. Waziri wa Afya aweze kumaliza majumuisho na hatimaye Baraza tuweze kuipokea taarifa yake ahsante sana naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja imetolewa iamuliwe)

(Hoja imeamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo labda nilikuwa nataka kulitolea pia ufafanuzi ni kuhusiana na ile hoja ya nyumba za daktari *against* hivi vituo vya afya. Naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi sasa hivi vituo vya afya basi vilivyokuwepo vimeshatosheleza, mtatupa mzigo mkubwa sana serikali wa kuvihudumia vituo hivi. Sasa hivi kinachokosekana ni nyumba za daktari kwa sababu kila kituo kikiwa na nyumba ya daktari pembeni kituo kile kitaweza kufanya kazi saa 24, na huduma zile zitaweza kutolewa vizuri sana pale katika eneo hilo na kupunguza pia uzito mkubwa ambao unabebwa na hizi hospitali zetu nyengine. Mimi naomba nitoe mifano michache ya waheshimiwa mbali mbali ambao wamekuwa wakichangia katika eneo hili.

Naomba nimshukuru sana Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil, yeye amechangia nyumba ya daktari pale jimboni kwa Mhe. Simai Mohammed Said Tunguu. Ni mfano mzuri sana tena Mhe. Ali Suleiman Ali yeye na Mbunge wake pamoja na fedha za jimbo wamekuwa wakilishughulikia suala hili kwa karibu sana, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais katika jimbo lake. Sasa nawaomba waheshimiwa hata katika ahadi zenu mkitoa au kama kuna ahadi yoyote ama fedha hizi za maendeleo ya jimbo, basi mkitusaidia katika nguvu ya kupeleka kwenye nyumba ya daktari ambaye atakaa katika eneo hilo utakuwa umewachangia wananchi kiasi kikubwa sana kwa kile kituo kufanya kazi vizuri zaidi pale. Na kitakuwa kituo ambacho hata kama kinafungwa ifikapo saa kumi jioni ama saa kumi na moja jioni, lakini kitakuwa kituo cha saa 24 kwa sababu daktari anaishi pale pale anaweza kwenda kugongewa mlango akaja akakifungua kituo na mgonjwa akahudumiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye hoja ya Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ambaye yeye alizungumzia kuhusiana na hizi kadi za bima ya afya. Ni kweli sasa hivi kuna tatizo kubwa sana

hasa kwa wenzetu kule Tanzania Bara pia kuna tatizo. Siku hizi huwezi kwenda ukatibiwa moja kwa moja bila ya kupigwa simu kwanza kufanyiwa *verification process* ama kukubaliwa kupata kibali ile hospitali ikatoa huduma. Na huko kwa sababu yalifanyika mengi kama aliyoyaeleza Mhe. Nadir, *test* za kiajabu zilikuwa zikifanywa, vipimo vya kiajabu kwa sababu vipimo vile ni vya pesa nyingi ikawa ile huduma imebadilika badala ya matibabu sasa imekuwa biashara ya kifedha, imeondoka kwenye matibabu imekuwa biashara ya kifedha.

Kwa hiyo, hilo ni jambo moja wapo ambalo sisi madaktari wetu wanalielewa na sisi tunalifahamu na tunaliona, lakini zaidi linafanyika katika sekta binafsi. Upande wa sekta yetu ya serikali ni matibabu bila ya malipo kwa wananchi wote wa Zanzibar, matibabu bure. Kwa hiyo, hizo pamoja na huduma za uchunguzi mbali mbali panapokuwa na kasoro basi huombwa mgonjwa achangie na huchangishwa pale panapokuwa na kasoro, lakini panapokuwa na huduma zile zinapatikana, mfano *MRI* sisi ndio nchi pekee duniani tunaotoa huduma za *MRI* bure wengine wote wana-*charge*, huduma za *CT scan* hutoa bure na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, pia tunaendelea kuwasisitiza madaktari wetu wawe makini zaidi wanapoandika hasa *prospection* za uchunguzi bila ya kuzingatia tatizo la mgonjwa hasa. Kwa hiyo, tunaamini madaktari wetu pia wataendelea kuwa makini zaidi na madaktari wa zamani wataendelea kuwasaidia madaktari hawa vijana ili kuwaelimisha katika nyanja hiyo, wapi kuandika uchunguzi na wapi hakuna haja ya kuandika uchunguzi. Naomba mapendekezo ya Mhe. Nadir na mimi nitayachukua niyafikishe serikalini pia, maana mapendekezo makubwa na mazito haya ya ndege na ya *helicopter* na mambo mengine, hii ya *Emergency Evacuation System*. Kwa hiyo, na mimi inshaallah nitayafikisha kunakohusika.

Mhe. Mwenyekiti, jengine naomba niweke *hansard* yangu sawa kuhusiana na ile chanjo leo asubuhi, tumepata taarifa kwamba chanjo zile zimewasili tayari za *BCG*, zimeshawasili Zanzibar na jana zimeanza kutolewa moja kwa moja. Kwa hiyo, taarifa hiyo naomba niiweke sana kwamba sasa hivi chanjo cha *BCG* zipo Zanzibar na wale wote waliokosa chanjo hizo ama watoto wao kutozipata basi wafike kwa ajili ya kupatiwa chanjo hizo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubali yale yote aliyonambia Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) pamoja na yale ya kituo chako, pamoja na kituo cha huko Kijitoupele, Magirisi una vituo vingi pale kwako. Kwa hiyo, yote hayo nimeyapokea na tutayafanyia kazi kwa pamoja na naamini jirani yako Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil umepiga debe vizuri sana kayasikia na maombi yako atayakubali na sisi tutaendelea kupiga debe pamoja kwa maombi hayo tuje kwa pamoja. Tukiweka nguvu zetu kwa pamoja basi naamini tutafanikiwa, pamoja na Mhe. Mbunge wako ambaye pia anaweka nguvu zake pale.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali pia alieleza kuhusiana na habari ya ukuta, naomba tuwapongeze sana kwa kweli tunaona jitihada zenu na sisi tutaendelea kuwaunga mkono na bahati nzuri wale watendaji ambao wanafanya kazi na wewe kwa karibu sana leo wote wako juu kule, unawaona wamefika. Kwa hiyo, na wao pia wameshalisikia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimkubalie Mhe. Simai Mohammed Said na kuendelea kumshukuru kwa mawazo yake na kwamba tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja na kwa karibu sana. Lile wazo la kusafisha kule nyuma ni wazo zuri sana, sisi tutaendelea kushirikiana na wewe, uongozi

wa Mnazi Mmoja upo hapa tutaendelea kushirikiana na wewe, wananchi wako wakijitokeza kwa wingi ni jukumu letu sote mwisho wa siku pale tunapatumia sote hawatumii wafanyakazi wa Wizara ya Afya tu ni wananchi wote. Kwa hiyo, sisi tunakushukuru sana Mhe. Simai Mohammed Said kwa *offer* yako ulioyotoa na tutakwenda pamoja na tutafanya kampeni maalum ya kusafisha pia ufukwe wetu mzima kuanzia kule Kizingo kwa Mhe. Ali Karume mpaka huku Serena mwisho itakuwa ni jambo la busara sana na hekima na litatuletea faraja sote.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nikubaliane na wewe kwamba kada ya X-*ray* wafanyakazi ni wachache sana, hawa *radiologists* ni wachache sana kwa Zanzibar tunao *radiologist* mmoja tu mpaka sasa hivi na mmoja yuko masomoni. Hawa *radiographers* pia nao ni wachache sana ndio maana tunapeleka sasa hivi kuwasomesha wengi zaidi. Kwa hiyo, kada hii katika kada zinazokabiliwa na upungufu mkubwa sana ni kada mbili Zanzibar. Ya kwanza ni hawa *radiologists* na *radiographers* na bahati nzuri Mhe. Sira Ubwa Mamboya ni mtaalamu mmoja wapo aliyepitia katika fani hiyo. Katika udaktari wake yeye ni mtaalamu katika fani hiyo na amekuwa akitusaidia sana kutupa ushauri pamoja na kutupa ushauri wa mafunzo. Lakini nataka kusema kwamba kada ya pili ni ganzi na usingizi na mtaalamu wetu ni mmoja tu Zanzibar nzima bingwa ambaye amesomea yule pale amekaa juu Dkt. Jamala Adam Taib. Yeye fani yake ni *anesthesiologists*. Mhe. Jaku alimpamba sana maana ni rafiki yake na naomba niseme kwamba alifurahi sana alipokuwa Mhe. Jaku anazungumza nilikuwa nikimuangalia mimi kwa yale anayozungumza kwamba mengi ni ya kweli yako juu ya mstari. Kwa hiyo, ni fani hizi mbili ambazo sasa hivi tumeweka nguvu kubwa sana namshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ametupa msukumo mkubwa sana wa *training* katika fani hizi mbili na fedha pia kupitia Waziri wa Fedha na Mipango tumeshapata na vijana zaidi ya 22 katika fani hizi, jumla wako masomoni wako masomoni hivi sasa.

Pia mheshimiwa amezungumzia kuhusiana na mambo ya utaratibu wa usafi, utaratibu wa kuingia hospitalini ukienda baadhi ya hospitali kule nchi zilizoendelea wanazile *sanitize* ziko ukutani zimewekwa za kupunguza *infection* na kadhalika. Hayo tumeyapokea na kwa upande wetu wa Mnazi Mmoja tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni la Mhe. Jaku Hashim Ayoub pongezi zake tumezipokea. Mimi nakubaliana na wewe Mhe. Jaku maneno mazuri ni sadaka, nakubaliana na wewe kabisa kwa sababu wakati mwengine maneno mazuri yanamponya mtu anakuwa hata hahitaji dawa, kwa sababu ametoka na matatizo yake mengine anafika hospitali yeye anahisi kwamba anaumwa kumbe anatoka na matatizo mengine. Na kweli maneno laini humtoa nyoka pangoni, kwa hiyo ndio maana hata mimi nakuwa na maneno laini sana kwako wewe pia hivyo hivyo, pale unapokuwa unapanda jazba wakati mwengine unakuja juu, unapokuwa na moto, unapotoka machozi kwa ajili ya wananchi, yale yote sisi huwa tunayapokea na tunafanya kazi pamoja kwa sababu lengo na dhamira kuu ni kumtumikia mwananchi na sote tuko kwenye eneo hilo hilo na nia hiyo hiyo.

Kwa hivyo, mimi naomba niseme kwamba mashirikiano yetu na wewe yatazidi zaidi na lile la kuzidisha elimu hasa katika ugavi wa dawa, lile tumelipokea na tutalifanyia kazi na tutafanikisha hawa ma-*pharmacists* wetu wanakuwa na mawasiliano na madaktari. Ili daktari anapoandika dawa fulani hata katika *pharmacy* dawa ile isipokuwepo ikiwepo mbadala wake basi yule

pharmacist aweze kuwasiliana na yule daktari ili yule mgonjwa apewe mbadala wake aweze kupona na tuweze kuwa tumemtumikia mgonjwa vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim Ayoub pia ulizungumza suala la yule mtoto kukaa tumboni, Mhe. Hamad Abdalla Rashid amelijibu vizuri sana hilo. Mhe. Naibu Waziri wa Afya amelijibu vizuri sana na mimi nimeomba haraka haraka hapa elimu nipate zaidi. Nimewaomba kule kuna wataalamu mabingwa wako juu pale na wao wakaniambia mpaka siku 14 yule mtoto anaweza kukaa bila ya wasi wasi tumboni aliyekuwa ameshakufa, mtoto aliyekuwa ameshakufa anaweza kukaa maiti haozi. Na mtoto huyu aidha kama alivyosema Mhe. Hamad Abdalla Rashid anatakiwa atolewe kwa kuchanwa ili atolewe ama kuna maji ya uchungu ambayo anaingizwa kulifanya lile fuko lijisukume kwenda chini ili azaliwe kwa kawaida.

Ni kweli kabisa mimi mwenyewe nishapambana nalo kuna mama siku hiyo alikuja pale wizarani analia kaambiwa mtoto wake ameshakufa wiki moja iliyopita, yule mama analia akahisi na mtoto wake pia atampoteza. Hilo ni kweli kabisa na mimi nikashtuka nika-*panic*, kwa sababu huo ni utaalamu wa wenyewe sio. Kwa hiyo, hizi sitaki kuziita *drip* lakini mambo hayo yapo ya wagonjwa wakati mwengine kutishana kwa sababu sisi hatuna taaluma zile. Kwa hiyo, naamini Mhe. Jaku leo utakuwa umepata taaluma na wewe yakujua. Sasa akipindukia wiki mbili na wewe sasa hapo itabidi uje ushauri tena utasema aah! huyu kapindukia wiki mbili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kutoa suala la *dialysis*. Huduma hizi za *dialysis* ndio kwanza tumeanza naweza kusema tuko kwenye *stage* za mwanzo za kufanya *test* na kuona wagonjwa wale wanaokuja, inshaallah mpaka sasa hivi hakuna *infection* yoyote iliyokuwa imetokezea, ila hili la *ultrasound* akina mama na naomba leo nitoe elimu kidogo. Akina mama wanapenda sana wakiwa wajawazito kupigwa *ultrasound* kupata kujua hali ya mtoto kila baada ya muda, lakini madaktari wanasema ile ni mionzi sio mizuri kwa mtoto. Kwa hiyo, ile *ultrasound* uwe unapigwa pale inapobidi baada ya kufanyiwa *test* nyengine pamoja na ile ya kusikiliza hivi, kuna kama kile kikombe nimekisahau jina sasa hivi huwa wanaekewa kusikilizwa *movement of the body, heartbeat* na kadhalika. Lakini daktari ama muuguzi akigundua kuna tatizo ndio unapigwa *ultrasound*. Wanavyotwambia wataalamu wa hii mionzi mtoto akipiga *ultrasound* wakati mwengine anakuwa ananyongonyea mle ndani kama anapata maumivu fulani.

Kwa hiyo, si jambo ambalo sisi tunalipenda sana au lifanyike mara kwa mara, ndio maana hizi kliniki za *ultrasound* zinakuwa wakati mwengine wiki mara moja au wiki mara mbili wanapangiwa wale kina mama wote ambao wanahitaji huduma ile, na sio kila mama mjamzito anafanyiwa *ultrasound*, sio. Wengine naamini hapa walijifungua bila ya kufanyiwa *ultrasound* hata mara moja, na wengine tulipozaliwa sisi wazee wetu kulikuwa hakuna *ultrasound* kwa hiyo hakuna aliyefanyiwa *ultrasound*. Naomba niendelee.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuhusiana na suala la Mhe. Nadir nadhani alizungumzia pia suala la chakula na kutia tarehe vipimo. Kwa kweli *ZFD* wanaendelea na kazi yao, nadhani hili tuwaachie kwa kweli wanafanya kazi nzuri katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni la Mhe. Shehe Hamad Mattar yeye alisema tuzidishe vivutio kwa madaktari, hili jambo kwa kweli ni muhimu sana sisi tunajitahidi na Mhe. Rais mwenyewe

amekuwa akilisimamia hili kidete. Tunaendelea na Mheshimiwa kiongozi wa nchi yeye mwenyewe alilisimamia hili kwamba kada hizi maalum wapewe vivutio. Kwa hiyo, vivutio vinaendelea ila tutazidisha kila fursa itakapotokezea, uwezo wa fedha utakavyoruhusu basi tutazidisha. Wenzetu pia nchi nyengine wamezidisha za madaktari wao ndio wana vivutio katika hizi nchi za *SADC* wengine wamezidisha zaidi sasa hivi vivutio kwa madaktari, lakini ili ufike huko nako lazima uwe pia mzuri sana kwa sababu ushindani nao ni mkubwa sana.

Wafamasia waende ngazi ya *degree* kwa kweli hili tumelipokea, tumeandaa sasa hivi mpango maalum wa wizara tunaita *training master plan long term* ili tuwe na mpango wa mafunzo kujua kwamba mwaka huu tutahitaji kada fulani na idadi fulani. Mwaka ujao tutahitaji kada fulani na idadi fulaini ili Mwenyezi Mungu atakapotujaalia siku kama hospitali ya Binguni itakapofunguliwa ile kubwa ya rufaa pale tena tusianze kuhangaika kuanza kutafuta wafanyakazi, tuwe na kada zote hospitali inafunguliwa siku ile kada zote zimo mle ndani. Kwa hiyo, sasa hivi tumeandaa mkakati maalum na sio hizi *field* za *IMD* ama *pharmacy* na *specialization* katika kada ya mpango mzima wa mafunzo ya wizara yote hayo yatakuwemo, pamoja na mpango huo utakapokamilika umeshaanza kufanyiwa kazi sasa hivi wanafunzi wameshaanza kwenda lakini tunataka tuwe na mpango wa muda mrefu ili hospitali zetu nyengine zote zitakazofunguliwa baadae ziwe hazina shida ya madaktari wala utaalamu maalum katika maeneo hayo.

Kisanduku cha maoni tumepokea na hicho tutakiweka lakini naomba nyie muweke maoni isipokuwa tatizo moja la kisanduku cha maoni ni lifuatalo. Katika sheria yetu ya utumishi na katika sheria zetu za sekta ya afya ushahidi ni jambo moja muhimu sana. Kwa hiyo, hata ukitia maoni yako yanaweza kufanyiwa kazi *general* lakini kama kuna jambo ambalo wewe labda umeshitaki ama umetendewa na mtendaji ama mfanyakazi ama muuguzi ama daktari na wewe hukuweka jina lako pale lile haitoweza kutumika dhidi yake yeye kama ushahidi, mpaka uweke jina lako na uwe tayari kutoa ushahidi. Hiyo ndio sheria yetu inavyotutaka na sheria hiyo ipo pia katika Baraza la Madaktari, sheria hiyo ipo pia katika Baraza la Wauguzi na Wakunga. Naomba hilo litambulike na lieleweke vizuri sana. Mhe. Mwenyekiti, na katika sheria kuu ya utumishi pia sheria ya kutoa ushahidi ipo.

Mhe. Mwenyekiti, nimelieleza lile la hospitali ya Abdalla Mzee ni wataalamu wangapi wameendelezwa mpaka sasa hivi. Naomba niseme haijapata kutokezea katika historia ya Zanzibar haijapata kutokezea tukiwa kwa wakati mmoja tuna wataalamu 155 wa kada mbali mbali za afya wakiwa masomoni nchi mbali mbali. Haijapata kutokezea 155 wako masomoni majina ninayo hapa na kada zao mbali mbali wanazosoma pia nazo zimetajwa. Sasa hivi tunataka twende kwa mpango maalum ili kila wanaporudi wanasambazwa katika yale maeneo ambayo wanahitajika. Lakini Mhe. Shehe Hamad Mattar tumelipokea na pia tutaendelea kulifanyia kazi kwa upana wake zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kumeelezwa kwamba fedha ni jambo moja lakini kutumia pia ni jambo jengine, usimamizi katika fedha unahitajika. Ni kweli kabisa tuna ile *procurement management a unit* lakini mara nyingi inabidi kama viongozi tushuke chini kuangalia je, tumepata vitu halisia, hapa fedha zetu hazijaliwa, hapa kama alivyosema Mhe. Hamad Abdalla Rashid hatujaathirika Mkoani Pemba na kadhalika, hapa hatujakodishwa nyumba kwa bei kubwa sana. Kwa hiyo, hayo tumeyapokea na tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niko mwisho mwisho tena. Mhe. Omar Seif Abeid yeye ametaja kuhusiana na kesi. Kesi hizi ni nyingi ziko sita hapa lakini ziko na nyengine za ziada na sitaki kuzitaja zote, kwa sababu tutapoteza muda, isipokuwa tunaweza kukaa baadae tukapitia. Ziko kesi kadhaa, kesi ambazo wameshapewa onyo, kesi ambazo wamenyanganywa leseni, ukishanyanganywa leseni maana yake huwezi kufanya kazi si Zanzibar si Tanzania Bara si kwengine kokote kwa sababu leseni yako ndio inakuwezesha kufanya kazi hasa ya uuguzi. Kuna kesi za walioghushi vyeti watatu, wao wameghushi vyeti wanasema ni wauguzi wamefika pale wamekabidhiwa kazi hajui kutia *drip*.

Sasa pale unajiuliza kweli huyu muuguzi? Naomba sana Waheshimiwa wakitaka kupeleka watoto wenu hasa mutusaidie majimboni wachague vyuo ambavyo vinatambulika kuwapeleka kusoma, tunawaomba sana muchague vyuo ambavyo vinatambulika. Kuna watu hapa wamesharudi na ma-*degree* zao vyuo vyao havitambuliki, wengine wamepata matatizo, wazazi wametoka machozi kwa sababu wamepoteza fedha miaka minne, mitano, sita, saba wengine wamerudi watoto wao hapa vyuo havitambuliki. Naomba watuulize tunao wataalamu, tunao mabingwa wako pale vyuo ambavyo vinatambulika ili mtoto akipelekwa arudi. Kwa sababu hawa wengine wameghushi wengine vyeti vyao havitambuliki.

Kuna vyuo huko mpaka vichochoroni Tanzania Bara, watoto wanakwenda kusoma wanarudi wanakuja kutafuta kazi hapa vile vyuo havitambuliki kwa hiyo inakuwa matatizo. Hawa wote wengine wameachishwa kazi, wengine wamenyang'anywa leseni, wengine wamepewa adhabu ya kimaandishi, wengine onyo kali na wengine kesi imepelekwa mbele mahakamani, zipo hapa sitaki kuzitaja zote.

Jengine kuna kesi moja hii nitaitaja kidogo, kesi hii ilikuwa ngumu sana na katika *experience* yangu ya Uwaziri wa Afya kesi hii ilikuwa ngumu sana. Kesi hii ilibidi tuzipe onyo *shift* tatu na kila *shift* ilikuwa ina wafanyakazi wanane. Kwa hiyo, wafanyakazi 24 wote tuliwapa onyo na kesi hii ilikuwa mwanamke kajifungulia mlangoni wakati anaingia pale *maternity* watu walikuwa wanabadilishana *shift*, wako *busy* wanabadilishana *shift* yule mama ameshakuja na uchungu pale wamechelewa kumpokea akazalia hospitali lakini mlangoni sio ndani.Wale wote tuliwapa onyo kwa sababu hata kama mnabadilishana *shift* mkabidhiane *shift* watu wawili wengine waendelee na kazi. Kwa sababu katika kubadilishana *shift* mgonjwa na mwananchi wa kawaida hatakiwi kuathirika. Sasa hilo lilitokezea na tumechukua hatua kali dhidi yao na tumesema ikitokezea tena basi wote hapo tena tutakuwa tumepoteza pesa zetu za masomo za kuwasomesha miaka yote potelea mbali.(*Makofi*).

Mheshimiwa jengine ilizungumzwa kuhusu wafanyakazi walioathirika na *TB*, wale tutahakikisha mafao yao wanapatiwa kwa wakati, tiba kamilifu watapewa na kuhakikisha kwamba hawana *TB* kabisa iliyobakia, hata kama *TB* sugu basi hilo tutaendelea kulishughulikia.

Mheshimiwa yako mengi kweli kweli hapa lakini najaribu kuyafupisha. Mashine za kupimia *pressure* zimeshaelezwa, kutoa elimu tumeshalieleza. Kwa hiyo, naomba niseme yaliyobakia yote tumeyapokea na tutaendelea kuyafanyia kazi. (*Makofi*).

Nawaomba sana Waheshimiwa waendelee kuwa karibu nasi kwa sababu sekta hii isiambiwe Waziri wa Afya tu, Mahmoud Thabit Kombo au ya Harusi Said Suleiman, Naibu Waziri wa Afya; sekta hii ni yetu sote inatuhusu sisi sote, tukishirikiana itakuwa nyepesi sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache na kwa heshima na taadhima nakushukuru sana kwa muda wako naomba sasa kutoa hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri, sasa naomba Waheshimiwa Wajumbe niwahoji ripoti imepokelewa nawashukuru sana. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe kwa utulivu wenu lakini pia na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri wa Afya na watendaji wake wote pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na wajumbe wake wote kwa kufanikisha yale maagizo yote yaliyoletwa hapa na waziri kwa jitihada zao wameyatekeleza kwa kiasi fulani. Lakini nataka nichukue nafasi hii kumkumbusha Mhe. Waziri na yale yaliyobaki katika kipindi kijacho basi yawe yamekamilika kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha napenda niwatangazie kwamba, kuna taarifa za barua zilizotolewa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuhusiana na suala la uzinduzi wa maonyesho yatayofanyika Kizimbani, lakini zilikuwa zina hitilafu hazikuonesha mgeni rasmi wala muda. Kwa hiyo, mgeni rasmi atakuwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohamed Shein na muda wa hiyo shughuli ni saa tatu kamili za asubuhi.

Pia nimepewa taarifa inayohusu watakaohudhuria kwa upande wa mawaziri naomba niwataje ili kesho waungane na Mhe. Rais.

1. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
2. Mhe. Waziri wa Afya
3. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
4. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
5. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum) na
6. Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiye na Wizara Maalum) *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe napenda na mimi nichukue fursa hii kuwashukuru nyote mliochangia na Mhe. Waziri na majibu yake naomba niakhirishe kikao hiki mpaka kesho tarehe 10/10/2017 saa 3:00 asubuhi. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

(Saa 2:08 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 10/10/2017 saa 3:00 asubuhi)